

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TATU

Kikao cha Nane – Tarehe 6 Novemba, 2008

(Mkutano Ulianza Saa Tatuh Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samwel J. Sitta) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:-

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya kwa Mwaka 2007.

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ninayo orodha ndefu sana lakini ni dhahiri hatuwezi kuwafikia wote kwa hiyo nitafanya mchanganyiko wa kawaida kwa kutumia vigezo mbalimbali vinavyotenda haki. Naanza na Mheshimiwa Haroub Masoud.

MHE. HAROUB SAID MASQUD: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nashukuru kupata nafasi hii ya kwanza kumwuliza swali moja la papo kwa papo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kwa kuwa Tanzania ni nchi yenye neema kubwa, inapata mvua za kutosha, ina mito, ina maziwa, ina ardhi kubwa na nzuri kabisa lakini hadi hivi sasa tunavyozungumza hali ya kilimo cha Tanzania iko duni sana ukilinganisha na nchi za Uarabuniambazo zina majangwa wanapata mvua miaka miwili au mitatu mara moja lakini vipando vyake ni vingi sana vizuri na wanasaferisha nje ukilinganisha vilevile na nchi ya Misri ambayo kuna Kamati moja hapa ilipelekwa wakati wa Mheshimiwa Lowassa akiwa Waziri ikajionea yenye hali ya Misri wanavyolima vipando mbalimbali kwenye mchanga mtupu.

Je, Waziri Mkuu atakubaliana na mimi kwamba ni vyema kama hatuna uwezo huo tukawapeleka watu wetu nchi hizo wakajionea na wakasoma ili watuletee Maendeleo katika nchi yetu?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Haroub kwamba nchi yetu ina neema kubwa sana kwa maana ya ardhi nzuri na mara nyingi nimekuwa nikisema hapa. Wataalam wanatuambia tuna hekta zaidi ya milioni 44 nzuri lakini ni asilimia ndogo sana kama kumi ndiyo inayotumika. *Irrigation* nayo hali tuna hekta karibu tu milioni 30 lakini ni hekta laki tatu ndizo zinazolimwa.

Kwa hiyo ni kweli kabisa anachokisema Mheshimiwa Mbunge. Lakini Waswahili walisema penye miti mingi hakuna wajenzi. (*Makofii*)

Lakini nataka niseme kwamba kama taifa tumepita katika hatua mbalimbali katika kujaribu kutafuta mbinu mbalimbali za kufanya taifa letu lisonge mbele lakini kila wakati kunakuwa na wakati ambao ni *unique* wakati huo. Awamu hii ya nne kitu ambacho tumedhamiria kukifanya kwa dhati kabisa ni kukuza sekta ya kilimo na kwa hili naomba niliseme wala huhitaji kwenda huko Uarabuni kwa sababu huna utakachojifunza. Utakwenda jangwani, utashangaa na kubung'aabung'aa pale.

Mimi nadhani sisi tujikite kwenye hali halisi iliyopo sasa. Ndiyo maana niliamua kwa makusudi kabisa nikawa na kongamano la siku tatu na Mikoa sita ambayo naamini inaweza ikatupeleka mbali sana. Kigoma, Rukwa, Ruvuma, Mbeya, Iringa na Morogoro Tumekubaliana kwamba ni lazima tusukume kilimo kwa kila hali na ndiyo maana maelezo niliyoyatoa kwamba tuondokane na kilimo cha jembe la mkono twende kwenye kilimo ambacho kina tija.

Sasa upo msukumo mkubwa sana kwa maana ya matumizi ya matrekta madogo lakini vilevile matrekta makubwa pamoja na kilimo cha umwagiliaji maji. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Haroub kwamba mwaka unaofuata nadhani utaona zitakuwepo dalili za kuongezeka kwa uzalishaji wa chakula hili na hakika lakini kubwa zaidi hata mfumo wenyewe wa kuendeleza sekta ya kilimo utaona nao tutakuwa tumeubadili sana kwa maana ya matumizi ambayo ni bora zaidi.

MHE. MAGDALENA SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niweze kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali. Kwa kuwa hivi karibuni taifa letu limekumbwa na tatizo kubwa la kuvuja kwa mitihani ya darasa la saba na mbaya kuliko yote ni Baraza la Mitihani la Taifa yaani *NECTA* kuchapisha vyeti feki na kuvisambaza mashulenii Serikali inasemaje kuhusiana na hali hii ambayo ni hatari kwa taifa letu?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa dada yangu swali lake zuri sana. Kwanza ni aibu, unajua kwa taifa kukaa mnaulizana maswali juu ya uvujaji wa mitihani si jambo zuri hata kidogo ni aibu sana.

Lakini kwa sababu mambo yanatokea inabidi tuseme na naomba niseme kwamba katika mitihani hii ambayo imetuletea matatizo yapo mambo mawili ambayo yamejitokeza pale. Moja ni kweli kwamba upo mtihani wa hesabu ambao ulivuja lakini uligundulika siku moja mbili kabla ya siku wenyewe na ndiyo maana hatua zikachukuliwa za kufanya mtihani ule uchelewe kidogo zaidi ili kufanya marekebisho yanayohitajika na kuutoa tena.

Lakini kwa maana ya masomo mengine ya historia, civics, geograph na masono mengine ni wajanja tu waliona watumie mwanya huo wakaanza kuchapisha makaratasi wakaanza kuyauza tena kwa fedha nyingi kwa madai kwamba ni mitihani itakayofanyika. Sasa ni aibu kwa mzazi ambaye unataka utumie fursa ya namna hiyo kumwezesha kufaulu mtihani kwa kutumia njia kama hii ya kununua mitihani ambayo inauzwa kinyemela ni aibu sana. Kwa hiyo, mimi rai yangu kwa Watanzania kwa hili ni:-

Kwanza sisi wenyewe kama wazazi tuone kwamba uchafu wa namna hiyo tusikubali na tuwe watu wa kwanza kutoa taarifa unapoona jambo kama hilo limetokea. Lakini kwa upande wa pili tumekubaliana na Waziri wa Elimu na Mafunzo ni lazima kwa kweli chombo chetu cha Baraza la Mitihani nacho tukiangalie kwa macho makali zaidi. Tutachukua hatua zozote zinazostahili ili kuboresha utendaji lakini vilevile kuboresha mbinu za kutunga mitihani. Sasa inawezekana katika hatua hizo na vyeti wanavyotoa pengine vinaweza vikawa ni feki. Kwa hiyo, tatizo lipo hapo kwenye chombo chetu na tutajitahidi kuhakikisha kwamba jambo hili sasa linasimamiwa vizuri kwa lengo la kuhakikisha kwamba taifa hatuingii tena kwenye mijadala ya aibu kama hiyo.

MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Shirika la Ndege la Tanzania ni Shirika ambalo linabeba bendara ya taifa na linasaidia sana kutangaza utalii wa nchi hii. Lakini Shirika hili sasa hivi ni hoi bin taaban. Je, Serikali ina mpango gani mahususi wa kuliokoa Shirika hili ikiwa ni pamoa na kuangalia upya Menejimenti ya Shirika hili kwa sababu hali ya ATCL sasa hivi ni mbaya sana?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo ya swali la Mheshimiwa Chegeni. Kwanza tukubali kwamba ATCL haipo katika hali nzuri, huduma zake zinashuka na kwa kweli ni mfululizo wa matatizo ya Kampuni hii na ndiyo maana Serikali ikachukua hatua wakati ule ya kuamua kwa kweli kuvunja mkataba tulionao na Kampuni ya Ndege ya *South Africa* kwa matarajio kwamba sasa Serikali ichukue jukumu la kuimarisha chombo hiki upya. Ninachowenza kusema tu kwamba Serikali ilishafanya maamuzi ya msingi kuhusiana na Kampuni hii na tumefanya mazungumzo na Serikali ya China kupitia Kampuni yake ambapo tupo katika hatua za mwisho kutiliana *Memorandum of Understanding* na baadae mikataba namna ya kuimarisha Kampuni hii ya ATCL. Nimwombe tu Mheshimiwa najua ana uchungu na sisi wote tunauchungu

lakini naomba uvumilie kidogo tufikie mwisho wa zoezi hili baada ya pale naamin *ATCL* itaibuka tena vizuri.

MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini suala la kwamba tunafanya kazi, tunaendelea kulitatua ni suala la muda mrefu sasa hivi.

Sasa sielewi kwa kweli ikiwa Watanzania sisi tunapanda *ATC* kwa wasiwasi mkubwa sana. Kuna wakati haina mafuta inafuta safari zake. Kwanini sasa Serikali isiwezeshe kulipatia fedha walau iweze kufanya *operation* zake. Maana yake sasa hivi hata mafuta ya kuendeshea hayapo?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ni hatua za dharura anazozungumza Mheshimiwa Chegeni. Tumejitahidi sana lakini kwa matatizo yaliyoikumba *ATCL* tunahitaji pengine kulitazama jambo hili kwa upana zaidi. Tulijitahidi hatua za mwanzoni mimi mwenyewe nilisimamia kikao tukakaa tukatazama matatizo yake. Walikuwa na matatizo makubwa sana ya malimbikizo ya madeni kutoka Afrika Kusini ya mafuta tukajitahidi tukayalipa kwa matarajio kwamba inaweza sasa ikaibuka kuanza kufanya kazi yake. Lakini si rahisi kwa sababu matatizo ni mengi mno ndani yake ndiyo maana tunajaribu kulitazama kwa upana zaidi tuweze kuja na mpango ambao utafufua kampuni kwa namna ambayo ni endelevu zaidi badala ya kushughulikia matatizo ya muda mfupi.

MHE. ALOYCE B. KIMARO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swalii. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwanza niipongeze Serikali yako nikiwa na maana Serikali ya awamu ya nne kwa kutoa kipaumbele kwa elimu kwa kuanzisha shule nyingi za msingi, sekondari na vyuo vikuu. Tatizo ni vitabu hasa vitabu vya kiada. Shule za msingi wanafunzi wanatumia kitabu kimoja kwa wanafunzi kumi; lakini vitabu kwenye makampuni viro. Sasa unaonaje ukianzisha utaratibu wa Wizara ya Elimu kununua hivyo vitabu na kusambaza mikoani badala ya utaratibu wa sasa?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, analolieleza Mheshimiwa Kimaro kwa upande mmoja ni kweli. Lakini nadhani tukubali kwamba hali ya upatikanaji wa vitabu kwa maana ya uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi sivyo ilivyokuwa miaka kadhaa iliyopita. Tumejitahidi sana kupunguza ile tofauti lakini pamoja na kupu nguza tofauti hiyo bado ni kweli tunakubali hatujafikia uwiano wa moja kwa moja kwamba mwanafunzi ana kitabu kimoja na hiyo ndiyo ingetakiwa kuwa lengo kubwa. Sasa tatizo liko wapi? Tatizo kwa upande mmoja ni la kifedha, lakini kwa upande mwingine ni taratibu zetu sisi wenyewe. Analolisema Mheshimiwa Kimaro ni kweli kabisa, ukienda kwa uchapishaji wa vitabu vitabu viro vingi sana.

Lakini fedha hizi zinatoka Wizarani kwenda kwenye Halmashauri zetu. Halmashauri zetu ndizo zinazotoa kandarasi za kununua vitabu na hapo ndipo kwenye tatizo. Kwa sababu wakandarasi wengine si waaminifu sana kwa hiyo wakati mwingine

wanaiingiza Serikali katika matatizo ambayo si ya lazima sana. Ukiondoa hilo bado hata ubora wa viabu wenyewe nao unatia shaka sana.

Vitabu ambavyo vimethibitishwa vipo lakini Wakandarasi hawa mara nyingi wanakwenda kununua vitabu vingine vya mitaani vimetengenezwa katika hali duni sana na ndiyo maana unakuta vitabu badala ya kukaa kwa muda mrefu muda mfupi sana. Kwa hiyo, tumekubaliana na Wizara ya Elimu na Mafunzo kwamba tutafute utaratibu ambao utatuwezesha kuwa na uhakika. Kwanza upatikanaji wa vitabu vyenye ubora unaotakiwa lakini pili usimamizi mzuri ili vitabu vingi zaidi viweze kupatikana hata kwa fedha tuliyonayo sasa. Kwa hiyo, nadhani tukikamilisha zoezi hilo inawezekana tukaongeza ubora wa huduma inayotolewa sasa kuliko ilivyo hivi sasa.

MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Swali langu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kuhusu huu Muswada wa Sheria pia na kuridhia Mkataba wa Haki za Watu wenye Ulemavu Duniani. Nimetumwa na jamii ya watu wenye ulemavu. Tumekuwa tukishiriki kwenye Mikutano kwa kweli. Lakini wanasikitika sana. Katika Mkutano wa Bunge uliopita tuliahidiwa kwamba kwenye Mkutano huu Sheria na Muswada utaletwa kwa hiyo suala langu ni hilo naomba Waziri Mkuu awatangazie watu wenye ulemavu wenyewe wamsikie.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba tu nimwahidi dada yangu Zuleikha kwamba tutajitahidi sana Bunge lijalo tulete Azimio lile tuweze kuridhia na tutaona uwezekano vilevile wa Sheria hiyo kupitishwa. Nakushukuru sana kwa kutukumbusha.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu kero kubwa ya wananchi wa mji wa Kahama na nina hakika na wananchi wa Mji wa Shinyanga kwa muda mrefu imekuwa ni maji. Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria hadi Mji wa Kahama na Shinyanga ulioanza takriban miaka minne iliyopita ultazamiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka uliopita. Taarifa za Serikali zinasema maji tayari yameshafika Kahama na Shinyanga. Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Miji hiyo Mradi huu utazinduliwa lini na maji yataanza kutiririka lini katika Miji ya Shinyanga na Kahama?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo mafupi kwa ndugu yangu Mheshimiwa Lembeli. Kwanza ni jambo jema wenzetu wa Mkoa wa Shinyanga na hasa maeneo haya ambayo mtapata bahati ya maji. Kwanza tuishukuru Serikali kwa mpango wake huo mzuri na mkubwa sana ambao tunaamini baada ya kuzinduliwa utatoa faraja kubwa sana kwa Watanzania. Kweli mradi ule umekamilika lakini bado kuna masuala kidogo ya kiufundi yanayokamilishwa kabla ya utaratibu wa uzinduzi haujakamlika. Lakini tunajitahidi tuweze kuifanya kazi hiyo mapema iwezekanavyo na sisi tunatambua adha iliyopo kwa wananchi lakini tunataka tuwahakikishie kwamba ahadi yetu ya kuhakikisha mradi ule unaanza kufanya kazi haraka iwezekanavyo ipo pale pale.

MHE. HAJI JUMA SEREWEJI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniruhusu kuuliza swali. Kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Kikao cha Kumi Mbili alilikutubia Bunge hili Tukufu na kueleza kuwa fedha za *EPA* zitaelekezwa kwenye sekta ya kilimo kwa pembejeo pamoja na wakulima kukopeshwa fedha hizo. Je, kwa upande wa Zanzibar wakulima watafaidika na fedha hizi? Hapo sasa. (*Kicheko*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, nilitamani nimueleze Mheshimiwa Haji kwamba kama kulikuwepo na wafanyabiashara kutoka visiwa vya Zanzibar amba walihusika na zoezi hili jibu lilikuwa ni rahisi sana kwamba fedha ile iliyokuwa imetokana na wafanyabiashara hao tungenesema hiyo moja kwa moja iende upande huo.

Lakini sina maelezo mazuri kwa hiyo; nirudi kwenye swali lake. Utakumbuka tulipokuwa Ngurdoto suala la kuendeleza sekta ya kilimo lilijitokeza vilevile si hasa kwa maana ya fedha za *EPA* lakini kwa maana ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuangalia ni namna gani mpango wa kuendeleza sekta ya kilimo utakavyowekwa katika mpango wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kwa hiyo swali lako nalijibu kwa upana wake tu kwamba eneo hilo linafanyiwa kazi. Kama ni fedha za *EPA* au kama itatoka kwenye Serikali yetu pengine si la msingi sana kikubwa ni kwamba sekta hiyo kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na yenyewe tuiendeleze kama ilivyo kwa upande wa Tanzania Bara. (*Makofi*)

MHE. HALIMA MOHAMMED MAMUYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali. Mheshimiwa Waziri Mkuu utakubaliana na mimi kwamba usafiri wa Reli ni usafiri amba Watanzania wengi na hasa wale wa vijijini ambako barabara hazifiki makwao unawasaidia na ndiyo usafiri muhimu kuliko aina zozote za usafiri kama barabara wala ndege. Lakini wafanyakazi ni kiungo muhimu sana katika utendaji wa kazi ya kutoa huduma katika sehemu hii ya reli.

Napenda kukuuliza kwamba unafahamu kwamba hadi leo wafanyakazi wa reli hawajalipwa mishahara yao na leo ni tarehe sita ya mwezi wa kumi na moja na wafanyakazi hawa wajapata mishahara yao?

Lakini la pili Mheshimiwa Waziri Mkuu unaweza kutueleza nini kuhusiana na ahadi ya Kampuni ya *RITES* kwamba wataongeza mishahara hiyo badala ya Serikali kuendelea kuiongeza?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, mimi najua dada yangu anafahamu kwamba nalielewa sana juu ya *TRL*. Mimi ndiyo nilikuwa mtu wa kwanza kuokoa jahazi wakati mambo yalipokuwa yameharibika sana na tangu wakati huo tumeendelea kulifuatilia jambo hili mpaka jana nilikuwa nahangaika na *TRL*.

Ninachoweza kumwambia Mheshimiwa Halima ni kwamba nafahamu kumekuwa na tatizo hilo, ahadi tulioitoa na tukaitekeleza kama Serikali ilimalizika mwezi wa nane na baada ya hapo tukatarajia kampuni hiyo ingeweza ikateleza jukumu lake ipasavyo lakini bado kutohana na sababu mbalimbali haijaweza kufanya hivyo.

Nikuahidi kwamba Serikali imelichukua tena suala hilo tunalifanyia kazi na tuna hakika wafanyakazi wa *TRL* hawatakosa mishahara hata kidogo.

Lakini kwa kweli changamoto kubwa kwa Serikali sasa ni kuona tutaendelea na bandika bandika namna hii ya vilaka mpaka lini? Ni lazima ifike mahali kampuni hii iweze kutekeleza majukumu yake inavyotakiwa. Kwa sasa hakuna tatizo na tutajaribu kuona kama hiyo nyongeza unayoisema kama tunaweza kuimarisha kama unavyotaka.

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nimuulize Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu tarehe 10 Septemba, 2008 kwenye Gazeti la Nipashe la siku ya Jumatano Mheshimiwa Waziri wa Elimu Profesa Maghembe alinukuliwa akieleza kwamba wazabuni wote wa shule za sekondari wamelipwa.

Taarifa nilionayo ni kwamba wazabuni wengi katika sekondari nyingi katika nchi yetu, mathalan *Karatu High School*, sekondari zote za Kilimanjaro, Mbeya wazabuni hawajalipwa.

Je, Serikali inatoa kauli gani ili hawa watoto wetu ambao wanалишва na wazabuni wasiathirike kwa sababu mwanafunzi kukosa chakula kutamuathiri pia kwenye akili na pia kwenye masomo yake.

Lakini vilevile wazabuni hao wanaathirika kwenye biashara zao na Waziri ametoa tamko kwamba wamelipwa jambo linaloashiria kwamba labda utafiti wa kina haujafanyika. Serikali inatoa kauli gani katika suala hili ambalo sasa hivi linakuwa na utata?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ukiwa unadaiwa na watu 800 ukajitahidi ukalipa watu 400 bado hujatatu tatizo na ndivyo ilivyotokea kwa wakandarasi wanaolisha vyakula kwa watoto wetu. Tulijitahidi sana kama Serikali lakini uwezo tulionao wakati huo na kwa sababu suala la uhakiki lilikuwa bado linaendelea tuliweza kulipa wale ambao tulikuwa tumeridhika kwamba wanastahili sehemu kubwa ikabaki bila kukamilika na ndiyo tunayoikamilisha sasa.

Lakini vilevile wakati tunalihangaikia hili. Wapo wengine tena tuliendelea kulimbikiza madeni yao na ndiyo changamoto ya pili ambayo sasa inatukabili katika zoezi hili. Ninachoweza kuomba tu na hasa wakandarasi hawa kama unavyosema tusiwaadhibu watoto hawa katika mazingira ambayo si lazima sana. Mimi nadhani watuamini tunajitahidi sana mimi kama kiongozi wa shughuli za Serikali kuhakikisha kwamba deni hilo lililobaki linalipwa na tunataka tujaribu kuwahuisha kwa kadri itakavyowezekana ili tuweze kwenda sasa bila mtiririko mkubwa wa madeni ya siku za nyuma. (*Makofi*)

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu; ninamwomba aliingilie kwa namna ya pekee kwa sababu hofu yetu ni kwamba madeni haya yanayosemwa ni makubwa na nitoe mfano tu ili Bunge lako liweze kuelewa uzito wa tatizo.

Unapozungumzia kwa mfano shule ya Weruweru wazabuni wanadai milioni 80, shule ya Ashira wanadai milioni 160, shule ya Umbwe wanadai milioni 200 ningeweza kuorodhesha nyingi tu ambazo nimeweza kukusanya.

Tatizo hili ni zito na walicolalamika wanaeleza kwamba sasa wanaambiwa na wao wajitahidi hivyo hivyo kuminyaminy waapeleke chakula hata kidogo na watoto kiwango cha chakula kinapunguzwa. Athari hii ni kubwa na naomba Mheshimiwa Waziri yeze binafsi aliingilie kwa sababu taifa likiathiriwa kwenye elimu ndiyo limeangamia.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba tu nirudie nilichosema kwa Mheshimiwa Slaa, tunalifanyia kazi kwa kadri tunavyoweza. Ni jambo moja la hovyo na Mheshimiwa Profesa alikuwa ananiambia kwamba tunalo tishio la mgomo kwa wakandarasi, sikulala usingizi kwa sababu najua wakigoma itakuwa ni mbaya sana kwa watoto wetu maana shule ni nyingi sana na ndiyo maana nimewasihi sana nikasema hebu wafanye subira kidogo wacha tuone kwa sababu sasa Bunge limemalizika, tutakuwa na muda wa kutosha wa kulisimamia ili tuweze kutoa kauli ndani ya muda mfupi ujao kwamba sasa Serikali imelifikisha tamati na wakandarasi tuweze kuwalipa na tutajitahidi kulifuatilia kwa karibu sana.

MHE. JOHN P.LWANJI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu tulizoea kusikia habari za tuzo kama *Nobel*. Lakini kuanzia mwaka jana na mwaka huu tumeshuhudia tuzo moja nono sana inayotolewa na mfanyakishara wa mtandao wa kampuni ya ZAIN Bwana Mo Ibrahim.

Sasa kutoa tuzo kwa Marais wastaafu waliojaribu ku-*promote* utawala bora.

Sasa mimi napenda swalı langu lijikite kwenye hiyo tuzo yenewe ambayo ni shilingi dola milioni tano za mkupuo halafu dola laki mbili kila mwaka.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, swalı langu ni hili; hivi Viongozi wa Afrika kwa nini wasimshauri huyu mtu kwamba tuzo za kwanza ziende kwa Serikali ya nchi hiyo ambayo huyo Rais ameshinda, halafu tuzo ya pili basi apewe yeye?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri njia rahisi niseme tu, nimepokea ushauri wako, tutaufanya kazi maana siwezi nikaendelea zaidi ya hapo. Ahsante sana.

MHE. AHMED A. SALUM: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalı kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Jeshi la Sungusungu linafanya kazi vizuri sana katika nchi yetu ya Tanzania na Serikali inawatambua kwa kazi wanayoifanya kuleta amani katika maeneo yote ya nchi yetu ya Tanzania.

Lakini, Jeshi la Sungusungu linapokuwa linafanya kazi, wanatambulika vizuri. Wanapokuwa wanakamatwa wale watuhumiwa kwenda kwenye vyombo vingine vyaa sheria, suala hili linageuka na Sungusungu wanapata adhabu kubwa kweli kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa nini sasa Serikali isifikirie kuleta Muswada ili tuipitishé sheria rasmi, iweze kuwatambua, kutenga na kuweka maeneo yao ya utendaji wa kazi wakishirikiana na Serikali za Vijiji, Kata na Wilaya ili sasa waweze kufanya kazi bila utata wowote? (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swalı la Mheshimiwa Ali kama ifuatavyo. Ni kweli kabisa kwamba Sungusungu ambao ni walinzi wa jadi wanafanya kazi nzuri sana na mimi ni shahidi kwa sababu na Rukwa wapo. (*Makofi*)

Lakini tatizo letu kubwa na chombo hiki imekuwa ni namna wanavyotekeleza wajibu wao. Ni Jeshi la Jadi, kwa hiyo wanaendesa mambo yao kijadi na mara zote utakuta taratibu zao ni zile ambazo wakati mwingine hazizingatii mipaka ya kisheria ambayo inatakiwa kufuatwa na ndio maana mara zote imeonekana kama vile kuna mgongano kati ya chombo hiki cha jadi na sheria za nchi au vyombo vingine vyaa kisheria. (*Makofi*)

Kwa hiyo, sasa hivi tunachojaribu kufanya chini ya mpango huu mpya wa Polisi Shirikishi au Ulinzi Shirikishi ni kuvikusanya vyombo vyaa aina hiyo kuwa ni sehemu ya mfumo wa mpango huo ili viweze kuvezeshwa kupewa mafunzo ya namna ya kutimiza majukumu yao ili kuepusha hii mikwaruzano ambayo inajitokeza mara kwa mara.

Lakini, bado rai yake ni nzuri kwamba pengine mkiishamaliza zoezi la namna hiyo, mmefika mahali mmeridhika na kazi zao na utendaji wao, iko haja ya kutafuta mfumo wa kisheria pengine wa kutambua baadhi ya majukumu yao na kuwepo kwao ili waweze kuwa ni watu ambao tunaweza tukawaongoza kwa taratibu za kisheria. Kwa hiyo, mimi nafikiri wazo lake ni zuri, tutakuwa nalo katika shughuli nzima ya Ulinzi Shirikishi. Naamini kuna siku tutafika mahali tutatekeleza azma yake ya kutaka pengine tuwe na sheria inayovitambua vyombo hivi mahsus. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu umeisha. Kwa niaba yenu, napemda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi anavyojibu maswali kwa uwazi bila kuficha ficha kitu, na pale jambo ambalo linakuwa halijaiva, anatuarifu kwamba atalifanya kazi. Hili ni jambo zuri sana. (*Makofi*)

MASWALI NA MAJIBU

Na. 97

Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mpwapwa Kuwezeshwa na Kuboresha Miundombinu Yake

MHE. GEORGE M. LUBELEJE aliuliza:-

Kwa kuwa, kwenye Bajeti ya mwaka 2007/2008 Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa ilitengewa Sh. 768,005,000/= kwa ajili ya matengenezo ya barabara; na kwa kuwa, ipo mamlaka ya Mji Mdogo wa Mpwapwa:-

- (a) Je, mamlaka ya Mji Mdogo wa Mpwapwa imetengewa fedha kiasi gani kwa ajili ya matengenezo ya barabara na mifereji ya maji machafu/mvua hasa maeneo ya Mpwapwa Mjini; Ving'hawe, Igovu, Mwanakianga, Mji Mpya na Ilolo?
- (b) Kwa kuwa, Mji wa Mpwapwa unakua kwa kasi. Je, Serikali haioni kuwa, ipo haja ya kuboresha miundombinu ya barabara kwa kujenga kwa kiwango cha lami barabara za Mpwapwa Mjini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA
NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mpwapwa imetengewa jumla ya shilingi milioni 94.54 kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi milioni 69.54 ni kutoka Mfuko wa Barabara (*Road Fund*) na kiasi cha

shilingi milioni 25.0 kutoka Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa. Kiasi hicho cha fedha kimetumika kuimarisha barabara za mamlaka ya Mji wa Mpwapwa kwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Ujenzi wa mifereji ya kupitishia maji ya mvua kwa mawe na saruji yeny urefu wa mita 1078 katika maeneo ya Igovu, Mjini Kati, Uwanja wa Mgambo na *Police Quarters*.

(ii) Makalvati 9 ya slabu zenyenye nondo yamejengwa katika maeneo ya Mjini Kati, Polisi na eneo la Benki.

(iii) Barabara zenyenye urefu wa kilomita 12 zimechongwa kwa Greda katika maeneo ya Mji Mpya, Mjini Kati na Igovu.

(iv) Changarawe imemwagwa, kusambazwa na kushindiliwa katika maeneo ya Mpwapwa Mjini.

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Mji wa Mpwapwa unakua kwa kasi kutokana na kuongezeka kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi hususan kupatikana kwa madini ya vito vya thamani Wilayani humo hivyo kuvutia wageni wengi. Ipo haja ya kuboresha miundombinu hususan barabara kwa kiwango cha lami katika kuuweka mji katika hali ya kuvutia na kuhimili mahitaji ya miundombinu yanayokua. Kutokana na ufinyu wa Bajeti Serikali inatekeleza zoezi hilo kwa awamu kwa kuanza kuboresha miundombinu ya barabara kwa kiwango cha lami katika miji mikuu ya Mikoa na Manispaa mbalimbali nchini na baadaye itafanya hivyo katika miji ya Wilaya ukiwemo Wilaya ya Mpwapwa.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa Bajeti ya Halmashauri ya mwaka 2008/2009 Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 48.8 kwa ajili ya kuboresha barabara za Mpwapwa Mjini. Serikali itaendelea kuboresha Barabara za Mji wa Mpwapwa ili ziendelee kuwa katika kiwango cha kuridhisha.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali ya nyongeza. Kwa kuwa, Serikali imekiri kwamba Mji wa Mpwapwa unakua na watu wanaongezeka; na kwa kuwa kuna Mamlaka ya Mji Mdogo ambao unahitaji kama nilivyoomba kwamba hizo barabara ziboreshwe kwa kujengwa kiwango cha lami; na kwa kuwa Mji Mdogo unahitaji Soko la Kisasa na wafanyabiashara wanafanya kazi katika mazingira magumu.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba kwa kuwa uwezo wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kupata mapato yake, yaani *own source* ni kidogo sana. Je, Serikali itakuwa tayari kuiongezea Bajeti ili tuweze kuboresha miundombinu ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Soko Jipy?

Kwa kuwa katika swali langu la nyongeza la pili, ombi la wananchi wa Mpwawa ni kujenga barabara ya lami; na kwa kuwa Serikali imekiri kwamba uwezo ni mdogo kwa sababu ya ufinyu wa Bajeti. Je, Serikali itakubalina nami kwamba ianze kujengwa kwa awamu badala ya kusubiri tumalize miji yote ndiyo uje mje mjenge Mji wa Mpwapwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Lubeleje kwa namna anavyopigania Maendeleo ya Mji wa Mpwapwa; na kama nilivyoeleza hapa, kwa kweli kuna shughuli nyingi sana za kiuchumi ambazo zinaendelea kule, kitu ambacho kinaleta haja hii ambayo anaileta hapa.

Lakini anapendekeza hapa kwamba tutamke hapa kwamba tunaweza kuongeza Bajeti. Kitu ambacho kilishapitishwa hapa na kwa kweli haitawezekana tena mimi nikatamka hapa nikasema kwamba Bajeti hii inaweza ikaongezwa. Kwa hiyo, mimi ninachofikiria ni kwamba ni muhimu kitafanyika hapa, ni kutumia kiasi hiki ambacho kimetamkwa hapa walau kuweka miundombinu inayofanana na hali halisi ya pesa.

Kwa mfano, Mji wa Mpwapwa kwa hela hizi zilizopelekwa pale, wakitumia moramu, wakashindilia vizuri, ikatengenezwa pale, mwekezaji ye yeyote anayetaka kuwekeza katika Mji wa Mpwapwa ataona umuhimu wa kufanya hivyo. Kwa hiyo, hili jambo tunapongeza kwamba wanashughulika nalo, lakini tunafikiri kwamba kusema kwamba tunaweza tukatoa hela kwa ajili ya lami hapa haitawezekana.

Mheshimiwa Spika, la pili, anasema kwamba kwa maana hiyo hiyo tunganeza kidogo kidogo kuweka lami. Mheshimiwa Spika, jana nilikuwa najibu swali hapa kwamba kilomita moja ya lami inakwenda zaidi ya shilingi milioni 500. Mji wa Mpwapwa una mtandao wenye kilomita 40 za barabara. Kwa hiyo, nikitamka hapa kwa niaba ya Serikali kwamba tutafanya hivyo, nitakuwa sisemi kweli. Ninachowezza kusema hapa ni kwamba tuangalie jinsi ambavyo tunaweza tukaendelea na utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, utaratibu tulionao ni kwamba sasa hivi tunaangalia Miji Mikuu ya Mikoa na kuangalia namna tunavyoweza kuunganisha na Wilaya zetu, ndio utaratibu ambao tunautumia kwa kisera kwa sasa hivi.

Na. 98

Gharama ya Walimu Kufuata Mishahara Yao Wilayani

MHE. ERNEST G. MABINA (K.n.y. MHE. KABUZI F. RWILOMBA)
aliuliza:-

Kwa kuwa walimu na watendaji wengine katika Kata na Vijijini wanakaa mbali na Makao Makuu ya Wilaya na wanaposafiri kufuata mishara yao hulazimika kulala huko na wakati mwingine hutumia robo ya mishahara yao kwenye nauli na malazi:-

Je, ni lini Serikali itafikiria kuweka angalau 10% ya mshahara kama nyongeza ili kufidia gharama wanazopata wanapofuata mishahara?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa walimu na watendaji wengine katika Kata na Vijiji wanakaa mbali na Makao Makuu ya Wilaya. Hivyo wanapaswa kufuata mishahara yao katika benki ambazo ziko katika Makao makuu. Aidha, ni kweli kuwa zipo gharama za kufuata mishahara yao katika benki. Hata hivyo, Serikali ilishaweka utaratibu mzuri wa namna ya kutoa mishahara. *Payroll* inafuatwa Hazina kati ya tarehe 14 – 18 ya kila mwezi. Aidha, mishahara inalipwa kuanzia tarehe 23 ya kila mwezi. Vile vile kwa ujumla umekuwepo ushirikiano mzuri kati ya Meneja wa Benki na Halmashauri kwa kuwaweka madirishani *cashiers* wengi ili kupunguza msongamano. Hivyo kila mtumishi anakwenda Benki kwa wakati wake.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuitisha mishahara ya watumishi benki ndiyo unaotumika kwa sasa. Serikali hupandisha mishahara ya watumishi wote wa Serikali kwa utaratibu iliyojiveke. Hivyo Serikali haina wazo la kuongeza asilimia 10% ya mishahara kusaidia gharama wanazopata watumishi hao wanapofuata mishahara.

MHE. ERNEST G. MABINA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, kwa kuwa Serikali imekubali kwamba tatizo lipo na utaratibu uliopangwa, kwa kweli walimu wanasumbuka sana.

Je, Serikali ina utaratibu gani angalau kuwawezesha kuwaongezea marupurupu ya aina yoyote katika mishahara yao ili waweze kufaidika hata kama wakienda kuchukua mishahara wasipate tabu ya kuweza kusumbuka kila siku?

La pili; kwa kuwa Serikali imeanza kuwachezea walimu, ni sawa sawa na mtu umejipaka mafuta ya kunukia, ukaenda kwenye mzinga wa nyuki, mchana juu linawaka. Halafu ukaenda kuchokonoa katika mzinga wa nyuki. Serikali inasemaje kwa kuwachezea walimu hawa?

SPIKA: Hebu rudia hilo la pili, kuchazea. Siyo kweli!

MHE. ERNEST G. MABINA: Mheshimiwa Spika, nasema kwamba kwa kuwa Serikali imeaanza kuwachezea walimu kwa kuwanyima haki yao ya msingi hasa katika mishahara yao, ni sawa sawa na mtu umejipaka mafuta mazuri ukaenda mchana jua linawaka na ni kali, ukaenda kwenye mzinga wa nyuki, ukaanza kuchokonoa. Matokeo yake unategemea nini?

SPIKA: Hata usipojipaka mafuta, ukienda kwenye mzinga wa nyuki, utaumia! Lakini toa majibu Mheshimiwa Naibu Waziri! (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, mapendekezo yanayoletwa hapa na Mheshimiwa Mabina ni ya kuongeza marupurupu kwa ajili ya walimu, na utaratibu unaotumika hapa Bungeni na Serikalini kwa ujumla ni kuangalia marupurupu ya watumishi wote wa Serikali kwa ujumla wao.

Kwa hiyo, huu ndio utaratibu unaotumika. Hapa siwezi kutamka hapa sasa hivi nikasema kwamba marupurupu yanaongezeka kwa sababu Bajeti yenyewe imeishapita. Kwa hiyo, kama tunazungumza habari ya kupendekeza kwamba tuongeze marupurupu ya walimu pamoja na watumishi wengine ni pamoja na kuangalia Bajeti inayokuja, lakini si Bajeti hii tena.

Mheshimiwa Spika, sasa hili la pili, najua kwamba Waziri wa Elimu yuko hapa. Ni hili swalii la kwamba walimu wamechezewa. Mimi sikumbuki ni lini walimu walichezewa, lakini naomba niishie hapo kwa sababu sikuweza kulielewa vizuri. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, maelezo ya ziada!

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru kwa kunipa hii nafasi na nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Napenda kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kujibu swalii la pili la Mheshiiwa Mabina kama ifuatavyo:-

Kwanza, katika mwaka 2007/2008 jumla ya walimu 38,505 walipandishwa madaraja. Kati ya hao, walimu 36,493 walirekebishiwa mishahara yao. (*Makofii*)

Walimu ambao hawakurekebishiwa mishahara katika hao ni walimu 2,012 ambao hawakurekebishiwa kwa sababu za vifo, kustaaifu na sababu za aina hiyo. Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hakuna mwalimu ambaye amechezewa katika mshahara wake. (*Makofii*)

Na. 99

Changamoto zinazoikabili Tume ya Pamoja ya Fedha

MHE. MZEE NGWALI ZUBERI aliuliza:-

Kwa kuwa moja ya changamoto zinazoikabili Tume ya Pamoja ya Fedha ni kutofahamika vizuri Watendaji Wakuu wanaotoa maamuzi katika Serikali zote mbili za Muungano;

- (a) Je, Serikali haioni kuwa hicho ni kikwazo katika ufanisi wa Tume?
- (b) Je, hali hiyo haiwezi kuleta malalamiko makubwa kwa wananchi?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. YUSSUF OMAR MZEE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Jimbo la Mkwajuni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Tume ya Pamoja ya Fedha ni chombo cha Muungano ambacho kina Viongozi na Watendaji kutoka pande zote mbili za Muungano. Chombo hiki inatekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na na Wizara ya Fedha na Uchumi ya Serikali ya Muungano na ile ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mashirikiano hayo ni kwa lengo la kufanikisha majukumu ya Tume.

Aidha, Kamati inayosimamia masuala ya Muungano iliyo chini ya Makamu wa Rais inatekeleza majukumu yake kwa kuwashirikisha Watendaji Wakuu wa sekta mbali mbali za pande mbili za Muungano, pamoja na Watendaji wa Tume ya Pamoja ya Fedha.

Kwa mtazamo huo, Watendaji Wakuu wanaotoa maamuzi katika Serikali ya Muungano na ile ya Mapinduzi ya Zanzibar wanaifahamu vizuri Tume ya Pamoja ya Fedha. Kutohana na hali hiyo, hakuna kikwazo katika ufanisi wa Tume.

(b)Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba taasisi yoyote ambayo inatekeleza majukumu yake kwa faida ya wananchi, ni vyema wananchi wakazifahamu shughuli za taasisi hiyo mapema iwezekanavyo kwa lengo la kuepuka malalamiko. Kwa kutambua hilo, Tume ya Pamoja ya Fedha kuititia Bajeti yake, hutenga fedha kwa ajili ya kutoa elimu kwa wadau na wananchi kwa ujumla.

Elimu inayotolewa inalenga zaidi kuwaelimisha wananchi juu ya mapato na matumizi ya Serikali ya Muungano pamoja na majukumu mengine ya Tume kama yalivyoainishwa katika Katiba na sheria ya Tume Pamoja ya Fedha. Kwa kuwa chombo hiki ni kipyta, ni dhahiri kwamba itachukua muda kwa majukumu yake kufahamika kwa wananchi kwa ukamilifu.

MHE. MZEE NGWALI ZUBERI: Nashukuru kwa kunipatia nafasi kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Tume ya Shellukindo imebainisha changamoto nyingi zikiwemo baadhi ya Wakuu wa Taasisi hawailewi vizuri, sheria ni vikwazo vile vile na hata Tume yenye haina ofisi ya kufanya kazi.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atalizungumzaje hili?

Mheshimiwa Spika, halafu lingine kuwa Watendaji Wakuu kweli wanaweza wakaifahamu hii Tume vizuri sana. Lakini inapofikia maamuzi wanakuwa ni kikwazo au wana kigugumizi katika kutoa ule uamuzi.

Je, kwa hili analizungumziaje Mheshimiwa Naibu Waziri?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. YUSSUF OMAR MZEE): Mheshimiwa Spika, la kwanza, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba changamoto zipo kwa sababu hiki chombo ni kipyä na bila kuwa na changamoto, hata utekelezaji wake wa kazi hautaweza kupimika. Lazima wawe na changamoto ili waweze kuzitekeleza kwa ufanisi zaidi ndipo tuweze kupima mafanikio ya chombo hiki.

Lakini, kwa upande wa ofisi, nataka nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba chombo hiki, ofisi wanayo, wanayo ofisi pale Dar es Salaam na wanayo ofisi kule Zanzibar. Namwomba Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakapomiliza shughuli za Bunge, basi akubaliane nami tufuatane nikamwonyeshe hizi ofisi za Tume.

Mheshimiwa Spika, la pili, suala la maamuzi, nataka niseme tu kwamba maamuzi mengine ambayo yanapaswa kutekelezwa na Tume hayako katika mamlaka yao. Tume kazi yao ni kutoa ushauri kwa Serikali mbili hizi na maamuzi mengi yanapaswa kutekelezwa na Serikali hizi mbili, Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Namwomba Mheshimiwa Mbunge aangalie na asome vizuri sana sheria iliyounda Tume ya pamoja na katiba ili afahamu kwamba maamuzi mazito yanafanywa na Serikali mbili, siyo na Tume.

Na. 100

Umaskini wa Watanzania

MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA aliuliza:-

Kwa kuwa, Uchumi wa Tanzania umekua, na wananchi wengi bado ni maskini.

(a) Je, hali hiyo inasababishwa na nini?

(b) Je, Serikali inawezaje kukuza Uchumi na inashindwa kuondoa Umaskini?

(c) Je, nini kifanyike kurekebisha hali hiyo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. YUSSUF OMAR MZEE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Devota Likokola, Mbunge Viti Maalum lenye sehemu (a) (b) na (c), naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba uchumi wa Tanzania unaendelea kukua. Ukuaji wa Uchumi wetu huchangiwa na sekta mbalimbali zikiwemo kilimo, madini, maliasili, viwanda, ujenzi, utalii, huduma za fedha na kadhalika. Ukuaji wa kila sekta kwa ujumla wake na kwa kipindi husika ndio hutoa tafsiri ya kukua kwa uchumi wa nchi. Kwa upande wa umaskini wa wananchi walio wengi, tafsiri yake ni wananchi wengi kuonekana kuwa na upungufu au ukosefu wa mahitaji ya msingi kama vile chakula, malazi, mavazi pamoja na huduma za jamii. Sababu kubwa inayosababisha umaskini wa wananchi wetu ni ukosefu wa kipato kinachowawezesha kukidhi mahitaji hayo muhimu.

Baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Likokola, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Hali hii ya umaskini ya wananchi walio wengi inasababishwa zaidi na mambo ya msingi yafuatavyo:-

(i) Zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania wanategemea kilimo katika maisha yao ya kila siku na uzalishaji wao ni mdogo. Hivyo kuchangia kuwa na mapato mdogo.

(ii) Ardhi inayotumiwa na wananchi wetu kwa kilimo ni asilimia kumi (10) tu ya ile ambayo inafaa kutumika (44 mil. Hekta) kwa shughuli hiyo.

(iii) Hekta 289,000 tu ndizo zinazotumiwa kwa kilimo cha umwagiliaji.

(iv) Wakulima wetu wengi wanatumia zaidi majembe ya mkono kulimia.

(v) Mazao yanayozalishwa huuzwa nje yakiwa malighafi badala ya kuuza bidhaa zinazotokana na mazao ya kilimo.

(vi) Matumizi ya pembejeo na hasa mbolea bado hayajafikia mahitaji.(b)Uchumi wa Tanzania bado haujakua kwa kiasi ambacho utaondoa umaskini na hasa umaskini wa kipato kwa wananchi wetu. Hata hivyo, ili tuondokane na umaskini juhudzi za wananchi wenyewe zinahitajika katika kujituma. Kazi kubwa ya Serikali ni kutoa miongozo pamoja na kuhakikisha kuwa miundo mbinu iko katika hali ya kuridhisha. Kwa msingi huo, Serikali haijashindwa kuondoa umaskini bali suala la kuondoa umaskini ni mchakato unaoendelea na unahitaji juhudzi za wananchi na muda.

(c) Ili kurekebisha hali hiyo, mambo yafuatayo ambayo ni baadhi tu ni vyema yakafanyiwa kazi kwa kila mmoja wetu:-

(i) Tuongeze ukubwa wa eneo la kilimo, matumizi ya zana bora za kilimo, na kuongeza eneo la umwagiliaji na matumizi ya mbolea.

(ii) Tukuze viwanda na hasa vidogo vidogo ili tuweze kuuza bidhaa zaidi badala ya malighafi za kilimo.

(iii) Wajasiriamali wapatiwe mikopo yenze riba nafuu na elimu ya biashara.

(iv) Wananchi wahamasishwe kuwa na hisa katika makampuni mbalimbali yaliyopo nchini.

(v) Tuwekeze zaidi kwenye elimu.

(vi) Wananchi wasiuze maeneo yao ya biashara, badala yake waingie ubia na wawekezaji.

(vii) Kwa kuwa mitaji ya Watanzania walio wengi ni midogo, ni vyema tukawekeza kwa vikundi (ushirika).

Mheshimiwa Spika, ingawa mchakato mzima wa kuondokana na umaskini utachukua muda, lakini inawezekana kama kila mmoja wetu atatimiza wajibu wake. (*Makofi*)

MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA: Mheshimiwa Spika, asante. Nashukuru pia kwa majibu mauri ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa. Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, kwa kuwa wananchi wengi Tanzania tunayo ardhi ambayo ndiyo rasilimali yetu kubwa; na kwa kuwa tuna madini, wanyamaporu na rasilimali nyingine. Kwa nini Serikali haianzishi mchakato ili tuweze kutunga sheria ambayo itahusu kila mwekezaji awe na ubia na Mtanzania halisi kwa aaslimia isiyopungua 40%. Swali la pili; kwa kuwa, kitengo ambcho kinasaidia huduma za fedha ndogo ndogo kwa maana ya kitengo cha *Micro-Finance* kipo katika BoT, maana ya Benki ya Taifa na hakijatoa ufanisi mkubwa;

Kwa nini Serikali haianzishi chombo ambacho kitaratibu, kitaanzisha na kitasimamia taasisi ndogo za fedha ili kuleta haki na usawa kwa wananchi wote wapate mikopo hadi vijiji? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. YUSSUF OMAR MZEE): Mheshimiwa Spika, la kwanza, suala la Serikali kuititia Bunge lako Tukufu kutunga sheria kwa Watanzania kuwa na ubia katika mashirika mbali mbali. Mimi nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge na ushauri huu naupokea na nitawashauri wenzangu ili tuweze kuliangalia jinsi litakavyoweza kutekelezeka. (*Mkofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili; suala la *Micro-Finance*, nataka nisema tu kwamba hii ni fursa ambayo imetolewa kwa Watanzania. Watanzania wanaweza wakaanzisha *Micro-Finance* na hakuna tatizo lolote.

Kwa mfano, *SACCOS* ni *Micro-Finance*, Benki za wananchi vile vile ni *Micro-Finance Institutions*. Kwa hiyo, wananchi wanayo fursa ya kuanzisha na wana fursa vile vile ya kutoa mikopo kwa wananchi katika maeneo yao. Nataka nitoe wito kwa Halmashauri ambazo ahazijaanzisha Benki za Wananchi zifanye hivyo na nataka nitoe wito kwa Vijiji ambavyo havijaanzisha *SACCOS* vifanye hivyo ili waweze kutoa mikopo kwa wananchi wetu. (*Makofi*)

SPIKA: Ngoja nichague wawili, mmoja kutoka Upinzani, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Mlata.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nimwulize Naibu Waziri swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, hatuwezi kuendelea bila kuwa na uchumi mzuri na kwa hivyo, Baba wa Taifa aliwahi kusema: “Maendeleo ya Watanzania ni Maendeleo ya watu, si Maendeleo ya vitu”.

Je, unaposema kuwa uchumi umekua wakati watu ni maskini, huoni kwamba unakwenda kinyume na fikra na sera sahihi za Baba wa Taifa ambaye pia alikuwa Mwenyekiti wenu wa CCM? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Spika, siendi kinyume na usemi uliosemwa na Baba wa Taifa, isipokuwa, ninachokisema na Serikali inachokisema ni *ku-complement* usemi wa Baba wa Taifa, kwa maana hiyo ni kwamba uchumi wetu unakua lakini kama nilivyosema ni kwamba kunahitajika mchakato wa muda mrefu ili wananchi wetu na wao waweze kuondokana na umaskini wa kipato.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda tu nataka niseme kwamba, Watanzania tulikuwa na umaskini wa aina nyingi, kuna umaskini wa kipato, kuna umaskini wa elimu, kuna umaskini wa afya. Lakini leo Mwenyezi Mungu ametujalia na sera nzuri za Chama cha Mapinduzi hatuzungumzii umaskini wa Afya na umaskini wa Kipato, kuna *indicators* nyingi zinaonyesha kwamba umaskini wa afya na umaskini wa elimu tumeondoka huko na huu umaskini wa kipato tutaondoka.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba nimwuuilize swalii dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri mwenyewe amekiri kwamba umaskini wa Watanzania walio wengi ni hasa wale walioko katika sekta ya kilimo. Je, Waziri atakubaliana nami kwamba Serikali bado haijaweka mikakati mizuri ya kurudi kwa wakulima na kuwekeza kule ili umaskini wa Watanzania hawa uweze kutoka na kuinua uchumi wa kipato chao.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Spika, hivi asubuhi tu Mheshimiwa Waziri Mkuu alielezea jinsi Serikali inavyotaka kuwakaribia zaidi wakulima, na ninataka niongeze tu kwamba nia ya Serikali hii katika kuongeza tija kwa wakulima. Lakini nataka niongezee zaidi kwamba eneo ambalo kama nilivyosema tuna hekta milioni 44 za kilimo Watanzania tunatumia milioni 4.5 tukiongeza ukubwa huu, tukiongeza matumizi ya matreka kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu, tukiongeza matumizi ya mbolea.

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani tutafikia hatua nzuri zaidi na tutaondokana na umaskini na nia hiyo kwa Serikali ipo na ninadhani Mheshimiwa Spika wewe ni shahidi tumeeleza wakati wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo lengo la Serikali ni kuongeza Bajeti katika sekta ya kilimo na nia hiyo ipo na tutaifanya ili kuongeza tija kwa wakulima.

SPIKA: Sisi wa umri huu tunaelewa kwamba uchumi unakua, kwa sababu mimi nilipokuwa nakwenda shule nilikuwa natembea peku, bila kuvalaa viatu, mpaka chooni. Sasa hivi hakuna mtoto anayekwenda shule bila kuvalaa viatu. Kwa hiyo, vigezo ni hivyo, wengine wanafikiria Maendeleo yanakuja kwa mara moja tu. (*Makofî*)

Na. 101

TBS Kusimamia Usalama na Ubora wa Chakula

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH aliuliza:-

Kwa kuwa, Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) lina wajibu pia wa kudhibiti ubora na usalama wa chakula nchini, na kwa kuwa yapo maeneo ya Miji na Vijiji ambapo kunauzwa biashara kama vile Mamalishe, migahawa, masoko, machinjio, wauza chipsi, mishkaki, juusi na kadhalika, na wananchi wengi hutumia maeneo hayo kujipatia mahitaji yao ya chakula:-

(a)Je, Serikali inajisimamia vipi shirika hilo ili kuhakikisha maeneo kama hayo yanakuwa salama kwa afya za wananchi?

(b)Je, ni vigezo gani vinavyowekwa na *TBS* ili vifuatwe na wafanyabiashara wa aina hizo?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Maida Hamadi Abdallah , Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shirika la Viwango Tanzania *TBS* limepewa jukumu la kutayarisha na kusimamia utekelezaji wa viwango vya Taifa. Katika kulitekeleza jukumu hili *TBS* hushirikiana na taasisi nyingine za Serikali, kama vile Mamlaka ya Chakula na Dawa (*TFDA*) Mkemia Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Maji na Nishati (*EWURA*), Polisi wa Usalama Barabarani, Afisa Afya wa Wilaya, Miji , Manispaa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha maeneo kama vile ya Mama lishe, migahawa, masoko, machinjio ya wauza chips, mshikaki, juisi na kadhalika yanakuwa salama kwa afya ya wananchi, shirika la viwango Tanzania limetayarisha jumla ya viwango vya vyakula na maji vipatavyo 18 katika eneo hili. Usimamizi wa utekelezaji wa viwango hivi hufanywa na Mamlaka ya Chakula na Dawa (*TFDA*), hata hivyo, kwa kuwa mamlaka ya chakula na dawa haina mtandao katika ngazi za chini, mamlaka imekasimu usimamizi wa majukumu ikiwa ni pamoja na Maafisa Afya, Maafisa Mifugo, Ukaguzi wa nyama na Wataalam wengine. Eneo la uzalishaji wa chakula ambalo limekidhi matakwa ya kiwango husika hupewa cheti na *TFDA*.

Mheshimiwa Spika, vigezo muhimu ambavyo vimekuwa na *TBS* na kukaguliwa na *TFDA* kwenye usalama wa chakula ni pamoja na mazingira ya uandaaji wa chakula ikihusisha jengo, vyombo vinavyotumika na mahitaji mengine muhimu katika kuandaa chakula. Aidha, waandaaji wa chakula hutakiwa kukidhi viwango vya usafi na kupimwa afya zao. Lengo ni kuhakikisha kuwa chakula hakichafuliwi na vimelea vya magonjwa au kemikali zenyne madhara.

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swalii moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi sasa kumejitokeza wafanyabiashara mbalimbali wanaouza dawa za kienyeji, kama vile dawa za pumu, homa nakadhalika. Je, Serikali inasema nini kuhusu *TBS* kuchungunza dawa hizi za kienyeji ambazo nafikiria nyingi hazina usalama kwa wananchi.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba madawa ambayo yanatolewa katika jamii yetu yapo yale yanayotoka viwandani, na yapo yale ya kienyeji, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hata haya madawa ya kienyenji, vilevile inabidi yakaguliwe na *TBS* pamoja na *TFDA*.

Mheshimiwa Spika, hawa wanaouza madawa ya kienyeji huwa wanapitiwa na utaratibu huu huu wa kukaguliwa na endapo itaonekana kwamba madawa hayo yanaweza yakaleta athari kwa wanadamu basi hatua sitahiki huchukuliwa.

MHE. MUSSA Z. AZZAN: Mheshimiwa Spika, nashukuru, pamoja na mambo mema wanayofanya *TBS* lakini bado yapo matatizo ya baadhi ya bidhaa katika maduka. Mfano kama dawa za mswaki, unapoibonyeza, badala ya kutoa dawa inatoa povu, ujazo za chupa a gesi za kupikia hazifiki kiwango kinachotakiwa, lakini haya kabisa ni dhahabu zinazouzwa katika maduka ya masonara, kiwango cha dhahabu ni ndogo, thamani kubwa kina mama wanunua, na wakienda kurudisha au kutaka kuibadilisha wanapewa pesa kidogo sana.

Je, Serikali inasema nini kuhusu kuisaidia *TBS* au kuhakikisha inaondokana na tabu hii.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, ni kweli haya anayosema Mheshimiwa Zungu kwamba wapo baadhi ya wafanya biashara amba wanakosa uaminifu katika kutimiza vile viwango ambavyo vimewekwa katika baadhi ya bidhaa kama hizi zinazosemwa. Kwa mfano dawa za Miswaki na vile vile kama alivyosema dhahabu na niongezee hata kwenye vyombo vyta *electronics*. Kuna wengine amba wanauza vyombo feki na Wizara yangu siyo tu kwamba inatumia *TBS* lakini tunatumia pia hata Tume ya ushindani kuhakikisha kwamba huyu mtu ambaye analeta bidhaa feki au bidhaa ambazo hazifikii kiwango, anachukuliwahatua ili asipate faida badala ya yule mtu ambaye analeta bidhaa ambazo ni bidhaa sahihi kwa ajili ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, hatua zinachukuliwa ikiwa ni pamoja na kupelekwa mahakamani, kuwaharibia bidhaa pamoja na faini. Ninachokisema hapa ni kwamba tatizo hili limeenea maeneo mengi karibu Tanzania nzima, mtu anaweza kuamua kuchukua bidhaa feki pale inakuwa ni ngumu lakini msimamo wa Serikali ni kwamba watu hao wanavunja sheria. Ninachowaomba Watanzania ni kutoa ushirikiano kadri inavyowezekana kwa kuitaarifu Wizara yetu, *TBS*, Tume ya Ushindani na hata Polisi inapoonekana kwamba kuna bidhaa ambazo ni feki na kuhatarisha usalama wa wananchi ni vizuri kutoa taarifa halafu tuchukue hatua.

Tukichukua hatua kama kutoa adhabu, au faini kubwa, au pengine kifungo basi tutakuwa tunazuia wale wengine amba wanaweza wakaiga utaratibu huu na kwa maana hiyo basi tutakuwa tunapunguza tatizo kama si kulizuia kabisa katika nchi yetu. (*Makofit*)

Na. 102

Malipo ya Leseni za Bunduki kufanyikia Sikonge

MHE. SAID J. NKUMBA aliuliza:-

Kwa kuwa walipaji wa leseni za bunduki wilayani Sikonge wamekuwa wakilipia malipo yao Tabora Mjini; na kwa kuwa Sikonge sasa ina *OCD* wake:-

Je, ni lini utaratibu wa huduma hiyo utaanza kutolewa Sikonge Mjini, ili kuwaondolea usumbufu wamiliki wa silaha Wilayani Sikonge.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Sikonge ni mojawapo ya Wilaya mpya hapa nchini. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba jitihada zetu ziwe kuwaondolea usumbufu wananchi. Ni kweli Wilaya hii ina *OCD* lakini ofisi hiyo ya *OCD* bado haijapewa *Pay Station* ili kuweza kufanya malipo au kupokea maduhuli ya Serikali ikiwemo malipo ya leseni za Bunduki.

Mheshimiwa Spika, tayari Wizara yangu imekwisha ifahamisha Hazina ili Ofisi mpya za Makamanda wa Polisi wa Wilaya *OCD*'s hapa nchini ikiwemo Sikonge ziweze kuwa na idhini ya kupokea maduhuli ya Serikali na hata kufanya malipo mbalimbali kwa askari Polisi walio chini ya himaya zao kupitia ofisi hizo.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kutamka kwamba wananchi wa Sikonge kwa sasa wataendelea kulipia leseni zao Tabora Mjini mpaka hapo Ofisi ya *OCD* Sikonge itakapopata idhini ya kupokea maduhuli ya Serikali.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kwa kuwa matatizo yanayoikumba Sikonge yanafanana sana na yale yanayoikumba Tunduru katika upatikanaji wa leseni za uendeshaji wa magari, na vilevile Tunduru tuna *OCD* ambaye anapokea maduhuli ya Serikali.

Je, Serikali itakuwa tayari kuiruhusu Wilaya ya Tunduru *OCD* atoe leseni za kuendesha pikipiki na leseni ndogo za kuendeshea magari madogo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, suala la vibali vya leseni si suala ambalo linashughulikiwa na Wizara ya mambo ya ndani ya Nchi, isipokuwa ni suala ambalo linashughulikiwa na Wizara ya Fedha, nimelipokea na nitazungumza na ndugu zetu wa Wizara ya Fedha na tutaweza kumpatia jibu Mheshimiwa Mtutura.

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa ni haki ya wananchi wa Tanzania kuomba na kumiliki silaha kwa utaratibu uliowekwa na wananchi, lakini kuna tatizo la vikao vya ngazi ya Wilaya na Mkoa ambavyo vinahusika katika kuchambua maombi hayo ya wananchi, vikao hivyo havikai hadi miaka miwili mpaka mitatu.

Je, kuna tatizo gani hasa la kufanya hivyo vikao visikae kwa wakati muafaka?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa kweli nasikitika kama ni kweli kwamba vikao ambavyo ni lazima vifanyike katika Wilaya na katika ngazi ya Mkoa kuhusu utoaji wa leseni ama kutazama maombi ya leseni havifanyiki.

Lakini kwa kuwa nimelipokea nasema kwa masikitiko makubwa tutalifanya kazi kwa sababu ni wajibu kwamba hivi vikao na lazima majibu yatoke kama wale walioomba wanapewa ama hawapewi, ni wajibu kwamba vikao vikae na majibu lazima yatoke.

Mheshimiwa Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba hilo tumelipokea na tutalifanya kazi.

Na. 103

Vituo vya Polisi Kutofanya Kazi

MHE. LUCY F. OWENYA aliuliza:-

Kwa kuwa, Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema alipokuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kulijengwa vituo vingi sana vya Polisi; kwa mfano katika barabara ya *Rose Garden* kwenye magorofa ya *TPDC Mikocheni* kuna kituo cha polisi lakini kinatumiwa na *Private Security*:-

Je, kwa nini vituo hivyo havifanyi kazi kama ilivyotarajiwa.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Eneo la *Rose Garden* katika maghorofa ya *TPDC* kulikuwa na kibanda cha walinzi kilichojengwa na *TPDC*. Kabla ya kujengwa kituo hicho cha polisi katika eneo la Mikocheni B Jeshi la Polisi lilikuwa linatumia kibanda hicho *sentry box* kwa shughuli za Kipolisi kwa lengo la kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao katika eneo hilo na yale ya karibu. Baada ya kujenga kituo cha polisi katika eneo la Mikocheni kwa kushirikisha nguvu za wananchi wa Mikocheni B Jeshi la Polisi lilihamishia shughuli zake katika kituo hicho.

Uamuzi wa kituo hicho kutumika na kampuni binafsi ya Ulinzi ni jukumu la *TPDC* na sio la Jeshi la Polisi kwani kibanda hicho cha walinzi ni mali ya *TPDC* na siyo mali ya Jeshi la Polisi.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo sijaridhika nayo, katika majibu yake amesema kituo kile si cha Polisi. Lakini kituo kile kimeandikwa Kituo kidogo cha Polisi *TPDC* na katika majibu yake amesema Polisi walikuwa pale kuimarisha ulinzi na usalama wa Raia na mali zao, kwa sasa hivi tuna mchakato wa kusogea huduma za ulinzi karibu na wananchi kwa mantiki ya Polisi Jamii na tayari pale kuna kituo kidogo cha Polisi. (*Makofi*)

Je, Serikali haioni sasa kwamba ni wakati muafaka wa kufufua kituo kile ili kiweze kutumika kwa wananchi wa eneo lile?

NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kile kituo ni kweli Polisi walikuwa wanakitumia, lakini si kituo chao kile kituo kilijengwa na *TPDC* ni mali yao na Polisi ilikuwa inakitumia kwa sababu ilikuwa haina kituo katika maeneo yale. Lakini baada ya wananchi wa Mikocheni B kujenga kituo chao kwa nguvu zao Polisi ilihamia katika kituo hicho. Kwa nyongeza ambayo iliifanyia kwa kukikamilisha na ndicho kituo ambacho kinatazama hali ya ulinzi na usalama katika eneo lote la mikocheni pamoja pia na eneo analolizungumzia la *TPDC*.

MHE. ANNA MAULIDA KOMU: Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina swali dogo. Je, anawaambiaje wananchi kuhusu kusaidia kujenga vituo hivi kila Kata ili viweze kuwasaidia hawa Polisi Jamii wanaojitolea kufanya kazi wakati wa usiku kulinda kwenye maeneo yao?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, katika mwelekeo mpya ambayo tumekuwa nao katika Wizara na katika Jeshi la Polisi tumekuwa tunakuja na hii falsafa ya Ulinzi Shirikishi na Polisi Jamii na ni kweli tunajaribu kuwahusisha wananchi na tunawaomba waweke nguvu zao katika kujenga vituo vya Polisi kwa sababu uwezo kidogo wa Serikali unakuwa haba kutokana na uhaba wa Bajeti.

Lakini kama wananchi watajitolea waweke jitihada za kujenga hivi vituo itatusaidia sote kama Taifa katika masuala ya ulinzi na katika suala la kuhakikisha kwamba kuna usalama katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba nikubaliane naye Mheshimiwa Maulida Komu kwamba Serikali inaunga mkono suala la wananchi kujenga vituo na kujitolea na Serikali itakuwa tayari kuijunga nao kuhakikisha kwamba ulinzi shirikishi unakuwa na maana katika Taifa letu. (*Makofi*)

Na. 104

Ubovu wa Barabara ya Kigoma – Nyakanazi na Kigoma – Tabora

MHE. MHONGA SAIDI RUHWANYA aliuliza:-

Kwa kuwa, tatizo la Barabara za Kigoma – Nyakanazi na Kigoma – Tabora bado linaendelea na majibu ya Serikali siku zote ni kwamba, Serikali haijapata fedha wananchi wavute subira:-

(a) Je, ni kweli kwamba, tangu Uhuru – 1961 Serikali haijapata fedha za ujenzi wa barabara hizo ambazo hazijawahi kutengenezwa kwa kiwango cha lami miaka 46 ya uhuru?

(b) Je, ni vigezo gani vinavyotumika kutoa fedha na kujenga Barabara za Mikoa mingine kwa kiwango cha lami?

(c) Je, ni lini sasa barabara ya kiwango cha lami itakayoiunganisha Kigoma na Mikoa ya jirani itajengwa ili wanachi wapate fursa ya kiuchumi na usafiri wa uhakika kama ilivyo kwa Mikoa mingine?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) ba (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tatizo la kutojengwa kwa kiwango cha lami barabara za Kigoma – Nyakanazi na Kigoma – Tabora pamoja na barabara nyingine nchini ni uwezo mdogo wa Serikali kifedha kuweza kuhudumia sekta zote za kiuchumi na kijamii. Hata hivyo, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele kwa ujenzi wa miundombinu ya barabara nchini. Na ndiyo maana hivi sasa Serikali imeanza kujenga barabara za Kigoma – Nyakanazi na Kigoma – Tabora kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali haina vigezo vyovoyote vinavyotumika kubagua baadhi ya Mikoa wakati wa kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Barabara. Hiyo ndiyo sababu kuna miradi mingi ya ujenzi wa barabara inayoendelea kutekelezwa kote nchini kwa viwango mbalimbali ikiwemo ile ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

(c) Mheshimiwa Spika, mipango ya ujenzi wa barabara za kiwango cha lami zitakazounganisha Mkoa wa Kigoma na Mikoa jirani iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo:-

(i) Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kigoma – Kitakwe (km.35.7) Mkataba wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kigoma – Kidakwe ulisainiwa tarehe 12/6/2008 na Mkandarasi yuko katika hatua za mwisho za maandalizi ya kuanza kazi.

(ii) Mradi wa Barabara ya Ilunde – Malagarasi – Kaliua (km.156):-

(a) Mkataba wa kufanya usanifu wa kina na kuandaa nyaraka za zabuni kwa barabara ya Ilunde – Malagarasi – Kaliua (km.156) ulisainiwa Julai 2007 kati ya *TANROADS* na Kampuni ya *Crown Tech.* ya Tanzania na kazi hiyo ya usanifu imekamilika.

(b) Serikali ya Korea Kusini imekubali kufadhili ujenzi wa daraja la Malagarasi na “*approach roads*” zenye urefu wa kilometra 48.

(c) Sehemu ya barabara ya Kidahwe – Uvinza – Ulunde – Malaragasi (km.130), mazungumzo kati ya Serikali ya Tanzania, Abu Dhabi *Fund* na *SAUD Fund* yanaendelea kwa ajili ya kupata fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami.

(d) Mradi wa barabara ya Kaliua – Urambo – Tabora (km126), usanifu wa kina ulikamilika mwaka 2006.

Pamoja na juhudhi hizo zinazoendelea, barabara ya Kigoma – Tabora nayo ipo kwenye orodha ya barabara ambazo zimeanishwa na Serikali kujengwa kwa utaratibu wa *Sovereign Bonds*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara inayounganisha Mkoa wa Kigoma (Kidahwe) – Nyakanazi, usanifu wa kina wa barabara hii unatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2008. Barabara hii nayo iko katika orodha ya barabara zilizoainishwa na Serikali kujengwa kwa utaratibu wa *Sovereign Bonds*.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Spika ahsante sana. Naomba niseme ukweli kwamba sijaridhika na majibu ya Serikali kwani ni majibu ambayo yamekuwa yakijirudia rudia mara kwa mara yanatoa matumaini lakini hayatekelezeki.

Mheshimiwa Spika, maneno ni yale yale, vuta subira, tukipata pesa tutajenga na tupo kwenye upembuzi yakinifu, nilichohitaji mimi ni ahadi ya Serikali ni lini itajengwa.

Mheshimiwa Spika, swal la pili vilevile sikubaliani na Serikali inaposema haina pesa kwa sababu tuna rasilimali nyingi na makampuni mengi makubwa ya wawekezaji hayalipi kodi, na vilevile tunasamehe kodi sana kwa wawekezaji. Vilevile nchi yetu imekuwa ikisamehewa madeni mengi. Vilevile *TRA* tumekuwa tunawapongeza kwa kukusanya mapato kwa kuvuka malengo.

Mheshimiwa Spika, Kigoma ikiwa Mkoa mmojawapo unaolipa kodi ninaomba nirejee kwenye majibu yake, amesema Korea Kusini imekubali kutujengea barabara ya Malagarasi kwa kilometra 48 na daraja. Vilevile amesema Kidahwe-Uvinza mazungumzo ya Serikali yanaendelea kati ya Serikali ya Tanzania na *Abu Dhabi Fund* na *SAUD Fund* hivi vyote havionyeshi *time frame* ni lini hizo pesa zitapatikana kwa upande wa Korea Kusini. Kwa hiyo, ni maneno yale yale na upande wa suala la *Abu Dhabi Fund* na *Saud Fund* vilevile hamna *time frame* haijulikani yatakwisha lini.

Mheshimiwa Spika, Kigoma ni sehemu mojawapo ya wananchi na wanalipa kodi. Naomba kujua kwa kiwango kikubwa kinachokusanywa na *TRA* haioneckani kwamba kuna umuhimu wa kuchukua angalau kwa awamu kiasi kile ambacho kinazidi ili kujenga angalau robo robo barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mhonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaupa kipaumbele sana Mkoa wa Kigoma kuhakikisha kwamba wananchi wa Kigoma wanaunganishwa na Mikoa mingine yote haraka iwezekanavyo na kwa njia mbalimbali kwa kutumia fedha zetu wenyewe nchini na fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kazi imeanza sasa hivi na mkandarasi yupo pale Kigoma akiwa ameanza kazi kwa kuunganisha Kigoma na nchi jirani ya Burundi kuanzia Mwandiga mpaka Manyovu. Kazi imeshaanza na ulipaji wa fidia umefanywa kwa baadhi ya watu na tunamalizia sasa hivi kulipa fidia kwa wale ambaa walikosewa hawakuingizwa katika kulipa fidia.

Mheshimiwa Spika, mkandarasi ameshapatikana ameanza kazi, Kigoma mpaka Kidahwa, tayari *process* ya *procurement* imefanywa kwa fedha zetu za Serikali, ni hivi sasa siyo mwakani au mwaka wa kesho kutwa.(*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia daraja la Malagarasi pesa zimeshapatikana na taratibu hizi za kumpata Mkandarasi zipo katika hatua mbalimbali za kumpata Mkandarasi wa kuanza kazi hiyo na hii inajumuisha *approach roads* kilomita 48. Ni kwa ajili ya mwaka huu wa fedha, kazi ianze katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ndogo itakayobaki ambayo mpaka sasa hajawenza kufikiwa hatua ya kupata fedha ni ile ya kutoka Nguruka mpaka mpakani mwa Tabora ambayo ndiyo Serikali inaifanyia kazi. Serikali inaifahamu na tupo mbioni kufanya kazi hiyo na tuna nia ya kufanya kazi hiyo. Wakandarasi katika baadhi ya maeneo tayari wako kazini wakifanya kazi ndani ya Mkoa wa Kigoma.(*Makofi*)

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kunipa nafasi, kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kazi ambayo kwa kweli inaendelea sasa katika Mkoa wetu. Mimi nilikuwa na swali dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia barabara hiyo ya kutoka Kigoma mpaka Manyoni ni kilomita nyingi sana, na baadhi ya maeneo kama kutoka Tabora hadi Kaliua tumeshamaliza usanifu wa kina, mimi nilitaka kuiomba Serikali, kwa maeneo yale ambayo tumemaliza usanifu wa kina hata kwa nchi yote *process* ya *procurement* ianze kwa sababu mchakato huu wa kupata Mkandarasi unatumia muda mrefu sana. Lakini bado unaweza ukaanza kutangaza leo ukitegemea kupata mwaka kesho, ule tu mchakato wenyewe unapofika wakati wa kutoa tenda tayari tutakuwa tumeingia kwenye Bajeti nyingine. Tumepata pesa, lakini tunaposubiri tunakuwa tunakuwa tunajichelewesha sisi wenyewe katika miradi yetu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Serikali iniambie mpango huo utaanza kuutekeleza lini?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafsi yakujibu swali moja la Mheshimiwa Serukamba, moja ni kwamba Utaratibu huo pamoja na kwamba Serikali sasa hivi tumejiwekea mpango wa kutoa fedha mwezi hadi mwezi. Lakini kwa mazingira maalum ya ujenzi wa miundombinu na kwamba *process* ya kumpata mkandarasi inachukua muda. Tumetumia njia hiyo kwa miaka kadhaa hivi sasa tayari *procurement* inaanza kabla hata fedha hazijatoka kwa kujua kwamba tunachukua kipindi kisichopungua miezi mitatu kumaliza *process* nzima. Ndivyo hivyo tunafanya kila siku na tutaendelea kufanya namna hivyo ili kuhakikisha kwamba kazi za miundombinu zinakamilika. Tabora, Manyoni tumeshaingiza katika mpango wa mwaka huu wa fedha tunakamilisha taratibu za usanifu ili kazi hiyo ianze mapema iwezekanavyo na pengine kwa sababu ya uhitaji mkubwa wa Mkoa wa Tabora.

Tunaweza tukaisogeza kidogo iende upande wa Kaliua ili tusianzie Tabora kwenda Manyoni, bali ianze nyuma zaidi kwa upande wa kwenda Kigoma. Lakini hii itategemea mazungumzo na uongozi wa Mkoa wenyewe. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea kidogo kwa sababu muda tuliooutumia kwa mambo mengine. Mimi nilikuwa na *observation* kidogo tu hapa ukurasa wa pili haya majibu ya Mheshimiwa Waziri haya ile (i) barabara ya Kigoma, Kidakwe na Ilunde Malagarasi zote ni *bold* lakini Kaliua, Urambo Tabora siyo *bold*. Sasa sijui maana yake ni nini. Halafu kwingine inatamka na fedha zitapatikana. Hii ni sentensi moja mradi wa barabara ya ya Kaliua, Urambo, Tabora km 126 usanifu ulikamilika mwaka 2006 basi. Basi, nadhani siku nyingine mtakapojobu mtajitahidi. (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naona umenigusa ndiyo maana nikaona nisimame nikutoe wasiwasi. Mheshimiwa Rais alipokuwa kwenye ziara Mkoani Tabora alinipigia simu kuniagiza nifanye kila juhud tuhakikishe tunapata fedha kwa ajili ya kuanza matengenezo ya barabara kutoka Tabora, Kaliua, Urambo na kuendelea kwenda kuungana na Kigoma. Kwa hiyo, nimetekeleza agizo hilo kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, sitaki sasa niende kwenye maelezo ya kina. Lakini nataka nikuhakikishie kwamba barabara hiyo, inashughulikiwa hivi sasa. (*Makofi*)

SPIKA: Haya ni mambo mazuri kweli haya. (*Kicheko*)

Na. 105

Uingizaji wa Ndege Nchini

MHE. MKIWA A. KIMWANGA aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilipojobu swali Na. 168 la Mheshimiwa Lucy Owenya, kwenye Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge kuhusu ndege aina ya *Airbus* iliyoingizwa na *ATCL* ilisema kuwa, ndege hiyo ni nzima na ilifanyiwa *C Check* kabla ya kuingizwa nchini:-

Je, Serikali inatuambia nini juu ya ndege zilizoingizwa na kampuni ya *Community Air* ambazo zilifanya kazi kwa muda mufupi na baadaye kugundulika kuwa ni mbovu?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kampuni ya *Community Airlines* iliingiza nchini ndege moja tu aina ya *Boeing 737-800* ambayo iliingia nchini tarehe 7 Disemba 2007. Ndege hii ni

mojawapo ya ndege za muundo mpya zinazotengenezwa na kampuni ya *Boeing* ya Marekani na kama kanuni za usalama wa ndege nchini (*Tanzania Civil Aviations Regulations* zinavyoolekeza, ndege hii ya aina ya B 737-800 ilifanyiwa matengenezo ya C-Check.

Aidha wenyne ndege hiyo walikaguliwa na wataalam wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania, kabla ya kuingizwa hapa nchini. Baada ya ya kuingia nchini ndege hiyo ilifanya kazi bila matatizo yoyote kuanzia tarehe 10 Disemba, 2007.

Mheshimiwa Spika, tarehe 15 Januari 2008, hitilafu ya kiufundi ambayo haikutarajiwa wakati ndege hiyo inaruhusiwa kuingia nchini ilijitokeza na ikalazimu kuhitajika kwa vipuri. Kwa kuwa vipuri vilivyohitajika havikuwa katika orodha ya vipuri anzilishi, vipuri vyaa ndege hiyo ilibidi viagizwe kutoka kwenye karakana ya wenye ndege iliyopo nchini Uturuki.

Baada ya vipuri hivyo kuletwa nchini na kufungwa ndege ilitengemaa na kuanza tena safari zake tarehe 17 Januari, 2008.

Mheshimiwa Spika, ndege ya *Community Airlines* ilikodishwa kwa mkataba wa *wet lease* ambao mwenye ndege *Pegasus* ndiye aliyekuwa na jukumu la kuhakikisha ndege inaruka kwa kutumia marubani wake na kutengenezwa na mafundi wake. Jukumu la mwenye biashara *Community Airlines* lilikuwa ni kuhakikisha tu kwamba anayo biashara ya kutosha ya kutumia ndege hiyo kwa faida. Kwa kawaida mfumo wa *wet lease* hutumika duniani kote kwa makampuni yanayoanza biashara ya usafiri wa anga wakati yakijenga uwezo wao kitaaluma katika marubani na mafundi.

Mheshimiwa Spika, sababu iliyofanya ndege ya B737-800 kusimamishwa kutoa huduma haikutokana na ubovu wa ndege, bali ilitokana na ndege hiyo kugonga kitu kingine (*foreign object damage FOD*) Tarehe 25 Januari 2008 na ndege kupata madhara ambayo yalihitaji matengenezo maalum na hivyo ndege hiyo ililazimika kurudishwa kwa wenyewe. Kampuni ya *Community Airline* iliruhusiwa kuleta ndege mbadala aina ya B737-500 tarehe 29 Januari 2008, kampuni ya *Community Airlines* ilisitisha huduma za ndege hiyo baada ya kuamua kuvunja mkataba wake wa ukodishaji na kampuni ya *Pegasus*.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ndege hiyo iliingia nchini baada ya kufanyiwa matengenezo ya *C Check* na kwa kuwa ndege hiyo ilifanya kazi kwa siku 35 kabla ya hitilafu za kiufundi.

(a)Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba matengenezo yaliyofanyiwa ndege hii hayakuwa makini na ingeweza kuleta madhara kwa wasafari wa ndege hiyo?

(b)Mheshimiwa Waziri amesema kwamba kampuni ilivunja mkataba ningependa kujua kwamba katika kuvunja mkataba huo Serikali yetu ilipata hasara gani au ilipata faida gani, kama ni hasara ni kiasi gani na kama ni faida ni kiasi gani? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba matengenezo ya *C- Check* yalikuwa ni matengenezo makini na kama nilivyokuwa nimesema katika jibu la msingi hapa kwamba hitilafu iliyojitokeza baadaye ilikuwa ni hitilafu tofauti na hitilafu ambayo ingeweza kutokea kuhusiana na suala la *C- Checking*. Kwa hiyo, hii ni hitilafu ambayo ingeweza kujitokeza kwa ndege nyine aina yoyote tu na ndiyo maana matengenezo yake yalikuwa yamekwenda katika kutengenezwa katika nchi ile ambayo ndege ile ilitoka.

Lakini kuhusu kuvunja mkataba nimesema hapa kwamba mkataba huu ulikuwa ni kati ya *Community Airlines* na hawa watu waliokuwa wameingia nao mkataba. Kwa hiyo, kueleza kwamba Serikali imepata hasara au faida kiasi gani nadhani kama ni suala la kuainisha hasara au faida ni kati ya Kampuni ya *Airlines* na lile shirika ambalo walikuwa wameingia nalo mkataba.

SPIKA: Kwa kuzingatia muda tumalize swal la mwisho.

Na. 106

Kupeleka Umeme Katika Mgodi wa Nickel – Kabanga

MHE. ELIZABETH N. BATENGA (K.n.y. MHE. PROF. FEETHAM FILIPO BANYIKWA) aliuliza:-

Kwa kuwa mgodi wa kuchimba madini ya *Nickel* uliopo Kabanga (*Kabanga Nickel*) Wilayani Ngara unahitaji umeme wa *MW 40* na kwamba umeme huo hauwezi kupatikana kutoka kwenye mitambo ya kufua umeme wa *TANESCO* iliyopo Ngara kwa sasa.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka umeme wa *MW 40* ili mgodi wa Kabanga *Nickel* uweze kuanza kufanyakazi mapema mwaka 2009?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Profesa Feetham Filipo Banyikwa, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mgodi wa *Kabanga Nickel* utahitaji *MW 40* za umeme kwa ajili ya shughuli za mgodi. Kwa kutambua mahitaji hayo makubwa, *TANESCO* kwa kushirikiana na Serikali wamefanya mawasiliano ya karibu na mwekezaji kubainisha njia bora ya kupeleka umeme wa kutosha kwenye mgodi wakati uzalishaji utakapoanza.

Aidha, wawekezaji ambao ni kampuni za *Barrick* na *Xstrata Nickel* wamemwajiri mtalaam mshauri kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu ili kubaini njia bora ya

kufikisha umeme stahiki kwenye mgodi huo. Mtalaamu mshauri ni kampuni ya *SNC – Lavalin* ya Canada kwa kushirikiana na kampuni ya *BEC* kutoka Australia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kazi hiyo kukamilika *TANESCO* na mwekezaji watakaa pamoja ili kuainisha mpango na mkakati wa kupeleka umeme kwenye mgodi huo.

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nilikuwa naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

(a)Kwa kuwa ameeleza kwamba watalaan sasa wanaangalia namna watakavyopeleka umeme kule maeneo ya *Kabanga Nikel*. Je, Serikali itahakikisha na kushauri kwamba njia ya umeme huo ipite maeneo ya Lulenge, Bukililo, Bugalama maeneo ambayo hayajapata umeme ili wananchi wa maeneo hayo waweze na kupata umeme huo?

(b)Kwa kuwa hizi machine za kufua umeme zilizowekwa Ngara ni miaka takribani mitano lakini mpaka sasa maeneo mengi hayajapata umeme. Je, ni lini Serikali itahakikisha kwamba mashine hizo zinapewa uwezo wa kufua umeme ili maeneo ya Mgoma, Kilusha, Rusumo, Kata nzima ya Nyamiaga, Mabawe na Kabanga kwamba yanapatiwa umeme?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza kama nilivyosema mtalaam akishakamilisha kutoa ushauri wake kwa jinsi ambavyo ataona inafaa na akawashauri Shirika letu la *TANESCO* pamoja na mwekezaji tutakuwa tumeshabaini kwamba mtalaam atakuwa ameshauri hiyo njia ya umeme ipitie maeneo gani. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge kwa sababu ni suala ambalo ni endelevu asubiri wakati tutakapokuwa tumeshakamilisha kupata taarifa tutatoa taarifa kwa kuititia ufuutiliaji wake ama Mheshimiwa Profesa Banyikwa ama kwa njia ya kuuliza swali kwa kuititia Bunge lako Tukufu. Kwa hiyo, tutatoa taarifa sahihi kadri ambavyo muda unakwenda. Kuhusu umeme Ngara tunamwahidi Mheshimiwa Mbunge na nilishawahi kusema, Wizara yetu imeshasema mara kadhaa, tunaendelea na juhudhi kwa kweli kuhakikisha wananchi wa maeneo ya Wilaya ya Ngara wengi wanapata umeme hasa kwa maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge anayasema. Lakini pia tuna mpango wa kufufua umeme kutokana na mradi wa kuzalisha kwa kutumia maji pale Rusumo ni juhudhi za nchi tatu bado tunaendelea lakini naamini kwamba kufikia mwaka kesho Mheshimiwa Mbunge atakuwa na taarifa nzuri zaidi kwa sababu tutampa taarifa nzuri zaidi kwa sababu kuna juhudhi ambazo sasa hivi zinaendelea na tunaamini zinaleta matunda mazuri. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote, Naibu Waziri kwa majibu yao na Waheshimiwa Wabunge kwa maswali yao. Kabla sijasoma matangazo kuna mwenzetu mmoja mtalaam wa Kiswahili amekumbusha hivi kwamba baadhi yetu tunasema dawa za mswaki, hizi ni dawa za meno. Ule mswaki ni kwamba ni nyenzo, yenyewe ndiyo inapakwa ile dawa lakini lengo

ni kwamba ukishapata kwenye mswaki upeleke kwenye meno. Kwa hiyo, kinachohudumiwa ni meno siyo mswaki. Naomba tukumbuke hilo. (*Makofi/Kicheko*)

Nilisema hapa kuhusu Maendeleo na kwamba sisi wa zamani tunaona mambo mengi yametendeka. Nimeandikiwa na baadhi ya watu nadhani wa rika langu. Mmoja anasema hivi: "Alianza kuva viatu alipofika darasa la 10 na alikuwa anaviweka sandukuni na alikuwa haendi navyo chooni akitaka kwenda chooni anavua na mvua ikinyesha havai. Kwa hiyo, ninyi vijana mnaopiga kelele hakuna maendeleo mimi siwaelewii kabisa. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo, wageni wa leo. Wageni wa Mheshimiwa wa John Malecela ambaa wanatoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania wako 16. Wageni wale wa Chuo Kikuu Huria, tafadhali wasimame wale pale. Karibuni sana. Tunawatachia mema katika mafunzo yenu. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa Lawrence Masha, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ambaa kwanza ni Katibu Mkuu wa Wizara na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi Bwana Mohamed S. Muya, watakuwa pale *Speakers Gallery* karibu sana Katibu Mkuu.

Huyo ndiyo Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya ndani ya Nchi. Amefuatana na Bwana Dominiki Rutta ambaye ni Mwenyekiti wa Tughe Wizara ya Mambo ya ndani Bwana Dominiki Rutta, yule pale. Makamu wa Tughe bwana Alcado Nchinga yule pale, Bwana Simon Isaac Mjelu Katibu wa Tughe Wizara, Bwana Donald Lonungu Katibu Msaidizi wa Tughe Wizara, Bwana Felitio Kibangali, Katibu wa Baraza Bibi Agaka Ng'ingo, Katibu Msadizi wa Baraza hayupo kwa udhuru. Bwana Khamis Simba Kamishna wa Polisi, huyu labda mpelelezi naona hana sare. Hakuvaare sare leo. Ndugu Mtweve Kamishna wa Polisi na Ndugu Michael Shija, Kamishna Msaidizi Zimamoto na Uokoaji.

Karibuni sana na inaelekea mna kikao cha Baraza la Wafanyakazi. Nawatachia mukutano mwema. (*Makofi*)

Wageni 20 wa Mheshimiwa John Lwanji ni viongozi kutoka matawi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Serikali za Vijiji na Kata ya Itigi wakiongozwa na Mheshimiwa Ali Ninja, Diwani wale wa Itigi. Ahsante sana majirani zangu mnasikia tunavyohangaika kupata barabara huko ndiyo hali yenye hiyo.

Wageni wa Mheshimiwa Said Amour Arfi ambaa ni wanachama wa Chadema, Chuo Kikuu cha Dodoma Wanachama wa Chadema ni mmoja loo! Basi karibu sana Ndugu yetu. (*Makofi*)

Halafu wageni wa Mheshimiwa Raphael Mwalyosi wanaotoka Wilaya ya Ludewa ni Mheshimiwa Justin Mwakila, Diwani wa Kata ya Lumbila mwambao mwa Ziwa Nyasa. Ahsante karibu sana. Loo! Safari ndegu kweli kutoka mwambao wa Ziwa na

Mheshimiwa Capt. Charles Mgimba, Diwani Kata ya Ludende, yule pale. Ahsante sana, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Mtutura, ni Mke wa Mheshimiwa Mbunge ambaye anaitwa Sofia Mtutura, yule pale ahsante sana. Pia msaidizi wake anaitwa Hussein Kaisi, Msaidizi wa Mheshimiwa Mbunge. (*Makofi*)

Halafu wageni wa Mheshimiwa Godfrey Zambi na Mheshimiwa Luka Siyame wa Majimbo mawili haya ya Mbozi ni Aden Mwakyonde, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi huyu Mheshimiwa yule pale. Ahsante sana. Mwingine Mheshimiwa George Nzunda, Diwani wa Kata ya Vwawa na Idan Mwashinga Afisa wa Mji Mdogo Tunduma yule pale na Donald Mshane Afisa wa Mji Mdogo wa Vwawa. Ahsante sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Alhaji Dr. Juma Ngasongwa na Mheshimiwa Vita Kawawa ni wajumbe wa Kamati ya Barabara ya Ulanga hadi Namtumbo. Loo! Kuna kuna Kamati ya barabara ya Ulanga hadi Namtumbo. Dr. Rajab Rutengwe, Mkuu wa Wilaya ya Ulanga pale *Speakers Gallery* karibuni sana. Ndugu Kimolo Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo. Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya ya Ulanga na Namtumbo naomba wasimame popote walipo. Ahsanteni sana. Wenyeviti wa Halmashauri Ulanga na Namtumbo.

Yupo mmoja ahsante sana karibu. Wahandisi, mameneja wa *TANROADS* Morogoro na Ruvuma yule pale karibu sana na Mhandisi Kilowoko kutoka Wizara ya Miundombinu. Ahsante sana. Karibuni nyote. (*Makofi*)

Sasa wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya ambaye ameandamana na watumishi waandamizi 10 karibuni sana. Wageni wa Mheshimiwa George Simbachawene ni Mariana Simbachawene ambaye ni mkewe Mheshimiwa Mbunge, naomba asimame pamoja na binti yao Caritas Chawene. Huyu anaitwa Chawene siyo Simba tena. Simba imewekwa sijui kwa nini. Karibuni sana. (*Kicheko*)

Wapo wanachuo 30 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara Dodoma wakiongozwa na Bwana Filipo Bundala, Naibu Waziri wa Elimu Bunge la wanachuo *CBE* Dodoma. Hawa wana mfumo nao wa Serikali zao. Ndiyo nilistuka mwanzo nilipoona Naibu Waziri halafu jina Bundala nikaona mm! Karibuni sana. Wananchi watatu kutoka Mkoa wa Dodoma ambao ni Grace Kaugila. Leo wamekuja sijui, niliwatamka jana hawa, wapo upande ule, Mahambanyungu na Rose Theodos Mgomba. Karibuni sana. Matangazo ya kazi zetu. Mheshimiwa Mohamed Missanga Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu ameniomba nitangaze kwamba leo saa tano asubuhi kutafanyika Kikao cha Kamati ya Miundombinu katika Ukumbi wa Msekwa. Nadhani kuna wageni ambao wanahitaji kuzungumza nao saa tano asubuhi Kamati ya Miundombinu Ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa Gideon Cheyo Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji anahitaji wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji mkutane leo tarehe 6 Novemba, 2008 saa 11.00 Ukumbi Namba 219. Mheshimiwa George Simbachawene Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo anaomba wajumbe wote wa Kamati hiyo ya Sheria Ndogo mkutane katika Ukumbi Namba 219 saa 5 yaani baada ya dakika hivi. Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya Ukimwi, anaomba wajumbe wote wa Kamati hiyo, mkutane saa tano Ukumbi Namba 227. Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa Naibu Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, anaomba leo saa 10.00 Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani, wakutane katika Ukumbi Namba 219. Waheshimiwa Wabunge, kuhusu mauzo ya Viwanja hapa Dodoma Katibu wa Bunge ameniomba kwamba kutakuwa na wawakilishi kutoka Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu - Dodoma (*CDA*) katika Chumba Namba 133 ghorofa ya kwanza jengo la utawala kuzingatia maombi ya Waheshimiwa Wabunge kupata viwanja katika eneo lile la Itega.

Kwa hiyo, mnaweza kwenda kukutana watalaan wa *CDA* kupata maelezo ya ziada kuhusu shughuli hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, nakumbusha leo saa saba mchana katika Ukumbi wa *African Dreams, Area D* kutakuwa na semina iliyoandalowiwa na mradi wa *Deepening Democracy* kwa ajili ya Kamati tano (5) zifuatazo: Kamati ya Fedha na Uchumi, Kamati ya hesabu za Serikali, Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, Kamati ya Miundombinu na Kamati ya Huduma za Jamii.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani hayo ndiyo matangazo niliyoyapata kwa leo. Kwa hiyo, namwomba sasa Katibu atusogezze mbele kwenye hatua nyingine inayofuata. (*Makofi*)

MISWADA YA SHERIA ZA SERIKALI

(*Kusomwa Mara ya Kwanza*)

Muswada wa Sheria ya kufanya Marekebisho kwenye Sheria mbalimbali wa mwaka 2008 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendment) Bill, 2008*).

Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania wa Mwaka 2008 (*The Tanzania Trade Development Authority Bill, 2008*).

Muswada wa Sheria ya Viwango wa Mwaka 2008 (*The Standards Bill, 2008*).

(*Miswada yote mitatu iliyotajwa hapo juu
ilisomwa kwa mara ya Kwanza*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa Miswada hiyo imekwishesomwa kwa mara ya kwanza yaani (*The Tanzania Trade Development Authority Bill, 2008, Miscellaneous Amendment Bill, 2008 na Standards Bill, 2008*).

Nimesimama tu kueleza Umma unaotuangalia kwamba kutokana na matangazo Kamati nne (4) zinakutana wakati huu. Kwa hiyo, mtu angepiga picha sasa angesema Wabunge wanafanya utoro. Lakini kwa kweli Wabunge wamekwenda kufanya kazi za Kibunge ambayo ni kufanyakazi za Kamati za Bunge.

Kwa hiyo, napenda umma utuelewe kwamba Bunge siyo Ukumbi humu tu, kuna kazi za Kamati zinaendelea wakati wote kutengeneza mambo yatakayoletwa sasa ndani ya Ukumbi wa Bunge kwa maamuzi ya Bunge. Nilipenda kufafanua hilo. (*Makofi*)

Muswada wa Sheria ya Afya ya Akili wa Mwaka 2008

(*The Mental Health Bill, 2008*)

(*Kusomwa mara ya Pili*)

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Afya ya Akili, *The Mental Health Act. 2008*, kama ulivyopangwa katika shughuli za leo pamoja na jedwali la marekebisho kama lilivyoambatanishwa sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Charles Mwera Nyanguru, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mbunge wa Jimbo la Tarime. Namtakia utumishi mwema kwa wananchi wa jimbo la Tarime na taifa zima kwa ujumla. (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba niwashukuru wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Omar Shabani Kwaang', Mbunge wa Babati Mjini kwa kuuchambua muswada ulio mbele yenu na kutoa maelekezo na michango ambayo imeniwezesha kuwasilisha muswada huu siku ya leo.

Aidha, napenda kuishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hususan Idara ya Muandishi Mkuu wa Sheria kwa kuandaa muswada huu na jedwali la mabadiliko kwa wakati. Vilevile shukrani za kipekee ziwaendee wadau wote walioshiriki katika kujadili muswada huu kwa kina na kuleta mapendekezo ambayo kwa kiasi kikubwa yamezingatiwa kwa lengo la kuuboresha muswada huu. Naomba niwatambue wadau hao kama ifuatavyo; *Youth Action Volunteers, The National Organisation for Legal Assistance, The Muhimbili University College of Health Science and MUHAS* na *The Tanzania Public Health Association*.

Mheshimiwa Spika, sheria ya magonjwa ya akili sura namba 98, *The Mental Diseases Act. Cap 98*, ni sheria inayotumika sasa. Sheria hii ilitungwa mwaka 1937 wakati wa utawala wa Waingereza, sheria hii haizingatii masuala mengi ya kimsingi kuhusiana na masuala ya afya ya akili. Katika kipindi cha tangu 1937 hadi sasa, hapa Tanzania na nchi nyingine duniani tumeshuhudia mabadiliko mbalimbali ya kijamii,

kisayansi, kiuchumi na kisiasa na hivyo kuifanya sheria iliyokuwepo ishindwe kuendana na mabadiliko haya.

Mheshimiwa Spika, sheria ya sasa ya magonjwa ya akili ina upungufu kwasababu inaashiria kuwabagua na kuwatenga wagonjwa wa akili badala ya kuwaandalia mazingira huru ya tiba kama watu wengine wenye magonjwa kwa mfano ya kisukari, shinikizo la damu na kadhalika. Sheria ya sasa haigusi kabisaa suala la kinga dhidi ya madawa ya kulevyta, vyanzo vya magonjwa ya akili na tiba kwa waathirika wa dawa za kulevyta. Muswada huu wa sheria unalengo la kuboresha huduma kwa wagonjwa wa akili kwa kuzingatia haki za msingi, kujali utu na kuongeza ushirikishwaji wa jamii. Aidha mabadiliko ya sheria yana lengo la kutekeleza muongozo wa Shirika la Afya Duniani ambaao unalenga kuboresha huduma za afya ya akili kwa nchi wanachama, Tanzania ikiwa ni moja ya nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, chimbuko na madhumuni ya muswada. Madgumuni makubwa ya mapendekezo haya ni kuboresha utoaji wa huduma kwa wagonjwa wa akili kwa kuweka masharti yanayozingatia utekelezaji wa haki za binadamu kwa kuondoa ubaguzi, unyanyapaa na udhalilishaji kwa wagonjwa wa akili na waathirika wa dawa za kulevyta. Aidha muswada umezingatia sera ya afya pamoja na viwango vya kimataifa kuhusu huduma za afya ya akili kama vilivyobainishwa katika muongozo wa Shirika la Afya Duniani. Nia ya muongozo huo ni kuboresha huduma za afya ya akili, vilevile muswada huu unakusudia kufuta sheria ya magonjwa ya akili sura ya 98. Mambo muhimu yaliyozingatiwa kватика muswada. Muswada ulio mbele yenu unaendana na sera ya afya ambayo inalenga kutoa huduma bora ambazo zinawafikia wananchi wengi na zenye viwango ambavyo vinakubalika kitaifa na kimataifa. Masuala mengine muhimu yaliyobainishwa ni pamona na haya yafutayo:-

1. Mheshimiwa Spika, dhana na haki za binadamu katika sheria. Kwa muda mrefu wagonjwa wa akili na waathirika wa dawa za kulevyta wamekuwa wakipata huduma bila kuzingatia haki za binadamu. Sheria mpya itaweka taratibu na masharti ambayo yatahakikisha kwamba haki za binadamu zinazingatiwa.

2. Mheshimiwa Spika, hiyari ya mtu binafsi kushiriki katika kupata tiba. Suala la tiba kwa wagonjwa wa akili mara nyingi limechukuliwa kuwa ni suala la lazima, sheria mpya itaweka taratibu za kisheria za kufuata endapo kutakuwa na ulazima wa kutoa tiba bila ridhaa hasa kama kuna uwezekano wa mgonjwa kujidhuru, kudhuru watu au mali.

3. Mheshimiwa Spika, kuimarisha viwango vya huduma. Sheria itasisitiza umuhimu wa kutoa huduma za afya ya akili kwa kufuata viwango vinavyokubalika. Aidha sheria itatoa nafasi kubwa ya ushirikishwaji wa jamii na sekta mbalimbali katika utoaji wa huduma za afya, kwani kwa muda mrefu jamii na wananchi kwa ujumla wamekuwa wakijitoa katika jukumu la kuwashudumia wagonjwa wa akili na kuviachia vituo vya kutolea huduma za afya pekee. Muswada huu umeainisha nafasi ya jamii katika kuwashughulikia wagonjwa wa akili hapa nchini.

4. Mheshimiwa Spika, tiba na ushauri kwa waathirika wa dawa za kulevya. Katika miaka ya hivi karibuni tatizo la dawa za kulevya limekuwa likiongezeka siku hadi siku, sheria itatoa tafsiri ya nani muathirika wa dawa za kulevya na kuanzisha vituo vya ushauri na tiba kwa waathirika hao.

5. Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Baraza la Taifa la Afya ya Akili. Sheria itaananzisha Baraza la Taifa la Afya ya Akili, ambalo litakuwa na jukumu la kumshauri Waziri mwenye dhamana ya Afya kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu Afya ya Akili hapa nchini.

6. Mheshimiwa Spika, huduma za kinga. Wizara yenyе dhamana ya afya kwa kushirikiana na sekta nyingine itaweka mipango mahsusni na kutoa miongozo ili kuboresha elimu ya kinga dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya na vilevi vingine vinavyochangia ongezeko la magonjwa ya akili hapa nchini.

7. Mheshimiwa Spika, kuhusisha jamii katika kuimarisha huduma za afya ya akili. Kulingana na malengo ya sera ya afya, jamii itaelimishwa na kushirikishwa katika kupanga na kusimamia huduma za afya ya akili vijijini na mijini kwa kushirikisha viongozi wa Serikali za Mitaa. Waganga wa tiba za asili pia watashirikishwa ili kuzingatia suala la usalama wa tiba zao wakati wanapowahudumia wagonjwa wa akili.

8. Mheshimiwa Spika, kuimarisha huduma za wagonjwa wa akili wahalifu. Sheria mpya italenga kuwalinda wagonjwa wa akili pale wanapotuhumiwa kufanya uhalifu kwa kuwapa haki ya kufanyiwa uchunguzi na kutibiwa kama raiya wengine. Sheria itaainisha masuala ya usalama ya usalama wa wagonjwa wahalifu, wafanyakazi wanaowahudumia pamoja na raiya wengine.

Masuala ya kuwarudisha wagonjwa wahalifu uraiyani yataendelea kutumia taratibu za sasa za kimahakama pamoja na kuhusisha Wizara za Katiba na Sheria, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia Bodi ya Afya ya Akili.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya sheria ya afya ya akili inayopendekezwa kutungwa. Sheria hii pindi itakapopitishwa inatarajiwa kuleta matokeo yafuatayo:-

1.Kuboresha na kupanua huduma za wagonjwa wa akili na waathirika wa dawa za kulevya.

2.Kupunguza idadi ya wagonjwa wa akili mitaani kwa kuwapeleka kwenye vituo vya afya kwa matibabu.

3.Kuwalinda wagonjwa mbalimbali wa akili nawaathirika wa dawa za kulevya, kuondokana na kudhalilishwa kiuchumi, kisaikolojia, kijinsia, kimwili, kubaguliwa na kadhalika.

4.Kuimarisha mazingira ya utoaji wa huduma ya afya ya akili kwa kuzingatia viwango bora.

5.Kuongeza usimamizi wa haki za msingi za wagonjwa wa akili na kupunguza uwezekano wa kudhalilishwa, kubaguliwa au kutengwa na jamii.

6.Kutoa nafasi kubwa ya ushirikishwaji wa jamii na sekta mbalimbali katika kuboresha huduma za afya ya akili.

7.Kuanzishwa Baraza la Taifa la Akili na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Mpangilio wa Muswada. Muswada ulio mbele yenu umegawanyika katika sehemu sita zifuatazo.

Sehemu ya kwanza inahusu jina la sheria, tarehe ya kuanza kutumika na tafsiri ya maneno yatakayotumika katika sheria.

Sehemu ya pili inahusu kulazwa kwa hiyari kwa wagonjwa wa akili na muda watakaolazwa katika sehemu ya kutolea huduma za wagonjwa wa akili. Sehemu ya tatu ya muswada inatoa utaratibu wa jinsi ya kusimamia watu wenye ugonjwa wa akili pamoja na haki na usimamizi wa mali zao.

Mamlaka za Mahakama ya Kazi, Hakimu Mkazi na Mahakama ya Wilaya, katika kusimamia masuala yanayohusu wagonjwa wa akili na masuala yanayohusiana zimeainishwa katika sehemu hii.

Sehemu ya nne inahusu kuanzishwa kwa Bodi ya Afya ya Akili na shughuli zake ambazo ni pamoja na kuititia taarifa za wagonjwa wa akili waliofanya makosa ya jinai, kuwasikiliza wagonjwa na ndugu zao kuhusu masuala yanayowahusu wagonjwa hao nakadhalika.

Sehemu ya tanoo inahusu utaratibu wa jinsi ya kusimamia mali ya mtu mwenye ugonjwa wa akili, ridhaa ya Mahakama katika kutoa uamuzi kuhusiana na mali ya mtu mwenye ugonjwa wa akili pamoja na uwezo wa Mahakama kumsimamia mtu aliyeteuliwa kusimamia mali hizo.

Sehemu ya sita inahusu masharti ya jumla ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa vituo vya kutolea huduma za afya ya akili, Bodi ya haki za Wagonjwa, Baraza la Ushauri la Afya ya Akili, makosa na adhabu, matumizi ya sheria ya makosa ya jinai sura namba 20 katika masuala, ushahidi na kuitwa shaurini chini ya sheria hii. Vilevile sehemu hii inatoa uwezo kwa Waziri mwenye dhamana ya Afya kutengeneza kanuni chini ya sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho kuna majedwali mawili ambapo jedwali la kwanza linahusu Bodi ya Haki za wagonjwa na muundo wake na taratibu za vikao. Jedwali la pili lina fomu mbalimbali ambazo zitatumika katika utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha mwisho baada ya kutoa maelezo hayo, kwa heshima naomba Waheshimiwa Wabunge, wajadili mapendekezo yaliyomo katika muswada huu na hatimaye kuupitisha na kuwa Sheria ya Afya ya Akili, yaani *The Mental Health Act. 2008*.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

MHESHIMIWA DR. HAJI MWITA HAJI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Bunge toleo la 2007, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii yanayohusu Muswada wa Afya ya Akili, *The Mental Heath Bill, 2008*, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya hii, Mheshimiwa Omar Shabani Kwaang'.

Kabla ya kuwasilisha maoni ya Kamati, kwa niaba ya familia yangu naomba uniruhusu nitoe shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, Katibu wa Bunge, Hospitali ya Mkoa wa Dodoma na Hospitali ya Muhimbili Kitengo cha Moi pamoja na Waheshimiwa Wabunge na watu wote, bila kuwasahau wapiga kura wangu wa Jimbo la Muyuni kwa misaada yenu mikubwa ya hali na mali kwangu na mke wangu wakati nilipopata ajali ya gari hapo tarehe 17 mwezi wa nane mwaka huu. Kwa kweli tunawashukuru nyote na hatuna cha kuwapa ila Mwenyezi Mungu, awarudishieni yote kwa kipimo chake na ninasema asanteni sana. Baada ya shukrani hizo sasa naomba kuwasilisha maoni ya Kamati yangu yanayohusu muswada huu.

Kamati ilipata muda wakutosha wa kufikiria na kujadili Muswada wa Sheria ya Afya ya Akili ya Mwaka 2008 katika vikao viwili ambapo kimoja kilifanyika Ofisi ya Bunge Dar es Salaam na kingine kilichofanyika Dodoma. Katika kikao kilichofanyika Dar es salaam, Kamati ilipata maelezo ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kuhusu madhumuni ya Muswada.

Aidha, Kikao hicho kilishirikisha wadau mbalimbali wa Muswada kutoka sekta ya afya hususan vyuo vikuu vya utabibu, Chama cha Wanasheria Tanzania, *Tanzania Law Society, National Organisation for Legal Aid – NOLA, Youth Action Volunteers,*

Kituo cha Haki za Binadamu, Mashirika yasiyo ya Kiserikali yanayohusiana na Ushauri wa Kisheria na Waandishi wa Habari. Kwa niaba ya Kamati ninawashukuru wadau wote walioshiriki na kutoa maoni yao ambayo yalileta changamoto wakati Kamati ikifikiria vifungu vya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Madhumuni ya muswada huu ni Sheria ya magonjwa ya Akili Sura Na. 98 toleo la 2002, *The Mental Diseases Act.Cap 98 R.E 2002*. Inayotumika hivi sasa ni ya mwaka 1937 ambayo ilitungwa wakati wa utawala wa Waingereza, Sheria hii imepitwa na wakati na haizingatii mabadiliko mbali mbali ya kijamii na mahitaji ya msingi kuhusiana na masuala ya Afya ya Akili kama alivyozungumza Mheshimiwa Waziri. Kutungwa kwa Sheria hii kuna lengo la kuboresha huduma kwa wagonjwa wa Afya ya Akili kwa kuzingatia haki za msingi za afya, kujali utu na kuongeza ushirikishwaji wa jamii katika kuwahudumia wagonjwa wa akili. Aidha mabadiliko ya Sheria ya Afya ya Akili yana lengo la kutekeleza Mwongozo wa Shirika la Afya Duniani, mwongozo ambao unalenga katika kuboresha huduma za afya ya akili kwa nchi wanachama, Tanzania ikiwa ni mmoja wa wanachama hao.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu utaboresha utoaji wa huduma kwa wagonjwa wa akili ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri kwa waathirika wa dawa za kulevyu kulingana na Sera ya Afya. Vile vile Muswada unaweka masharti yatakayozingatia utekelezaji wa haki za binadamu kwa kuondoa vitendo vya ubaguzi na udhalilishaji kwa wagonjwa wa akili na waathirika wa dawa za kulevyu. Muswada huu unazingatia viwango vya Kimataifa kuhusu huduma za msingi kwa wagonjwa wa afya ya akili kama zinavyobainishwa katika Mwongozo wa Shirika la Afya Duniani kuhusu kuboresha huduma za afya ya akili.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa Muswada huu unaendana na Sera ya Afya ambayo inalenga katika kutoa huduma bora za Afya kwa kuwafikia wananchi wengi na kwa viwango vinakubalika kimataifa ,masuala mengine ya muhimu yaliyobainishwa katika Muswada huu ni pamoja na:-

- Dhana ya Haki za Binadamu katika Sheria;
- Hiari ya mtu binafsi kushiriki kupata tiba;
- Kuimarisha viwango vya huduma;
- Tiba na ushauri kwa waathirika wa dawa za kulevyu;
- Kuanzishwa kwa Baraza la Taifa la Afya ya Akili;
- Huduma za Kinga;
- Kuhusisha jamii katika kuimarisha huduma za Afya ya Akili; na
- Kuimarisha huduma za wagonjwa wa akili wahalifu.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati. Kamati ina maoni kuwa kutungwa kwa sheria hii kutawakomboa Watanzania wengi wanaohitaji huduma za tiba za wagonjwa wa akili. Aidha Sheria hii itawalinda wagonjwa mbalimbali wa akili ikiwa ni pamoja na waathirika wa madawa ya kulevyta, na hivyo kuondokana na kudhalilishwa kiuchumi, kisaikolojia, kimwili pamoja na kubaguliwa. Vile vile Sheria hii itaongeza usimamizi wa haki za msingi kwa wagonjwa wa akili na kupunguza uwezekano wa kudhalilishwa, kubaguliwa au kutengwa na jamii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kwamba Serikali iboreshe huduma zinazohusiana na afya ya akili kama vile:-

- Serikali iongeze idadi ya watumishi katika hospitali za wagonjwa wa akili hususan hospitali ya Mirembe na taasisi Isanga.
- Serikali izingatie kutoa motisha kwa wafanyakazi wanaohudumia wagonjwa wa akili wakiwemo Madaktari na Wauguzi.
- Serikali izingatie kutenganisha wagonjwa wa akili na waathirika wa madawa ya kulevyta katika taasisi ya Isanga kwa kuharakisha ujenzi unaoendelea wa kituo cha kuwashudumia waathirika wa madawa ya kulevyta katika hospitali ya Mirembe.
- Serikali iwapatie nyumba za kuishi wafanyakazi na wanafunzi madaktari na wauguzi wanaosomea magonjwa ya akili katika Chuo cha afya ya akili Mirembe.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefarijika kuona kuwa Serikali imeafiki pendekazo la muundo wa bodi ya Haki ya Wagonjwa katika Jedwali Namba Moja na kujumuisha wajumbe wengine wawili amba moja atawakilisha Sekta binafsi, *private sector*, na mwingine atawakilisha asasi zisizo za kiserikali, *NGO*. Kamati inatoa angalizo kuwa Sheria iweke mazingira yatakayowawezesha watumishi wanaohudumia wagonjwa wa akili kupata haki ya kinga dhidi ya madhara yanayoweza kutokea kutokeana na wagonwa wa akili wanaowahudumia. Kwa kuwa tafsiri ya neno, *Medical Officer*, limejikita zaidi katika maana ya daktari anayefanya kazi katika utumishi wa umma, na haimuhusu daktari katika sekta binafsi, Kamati inashauri kuwa madaktari wanaofanya kazi katika Sekta binafsi wahuishwe katika Sheria hii kwani mchango wao ni mkubwa katika kuwashudumia wagonjwa wa akili.

Katika jedwali la kwanza, kifungu cha kwanza, kinachohusu wajumbe wa Bodi ya haki ya Wagonjwa, kipengele (f) kimejumuisha kiongozi wa dini kuwa mjumbe, Kamati inashauri kuwa katika kipengele hicho maneno, *local religious leader*, yaondolewe ili kuepukana na utata unaoweza kujitekeza wakati wa kutekeleza sheria.

Aidha kamati inapendekeza kuwa majina yaliotajwa katika kifungu hiki yatenganishwe na yaorodheshwe tofauti. Katika kifungu 9(1) cha Muswada, Kamati inashauri kwamba Askari Polisi ye yote aliye kotokeza kwenye kituo cha Polisi ahusike katika kuchukua hatua muafaka za haraka za kukabiliana na mgonjwa wa akili, za kumfikisha kwenye kituo

cha huduma badala ya kumsubiri Askari mwenye dhamana ya Kituo cha polisi kuchukua hatua hizo. Kuhusu gharama zinazotokana na uharibufu wa mali au madhara yanayotokana na mgonjwa wa akili, Kamati inashauri kuwa gharama hizo zilipwe na Serikali kwa minajili ya kulinda mali za wagonjwa hao. Vinginevyo mali za wagonjwa wa akili zitaishia katika kulipa fidia na gharama za mawakili. Baada ya Sheria mpya kupitishwa na Kanuni zake kutayarishwa, hatua za haraka zichukuliwe kutafsiri Sheria na Kanuni hizo kwa lugha ya Kiswahili ili ziweze kuelewka kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, napenda kumaliza kwa shukrani. Kamati yangu inamshukuru Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii Mheshimiwa *Professor David H.Mwakyusa*, na Naibu Waziri Mheshimiwa *Doctor Aisha O. Kigoda* pamoja na wataalam wao wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Wilson Mukama kwa ushirikiamo waliota kwa Kamati wakati Kamati hii inafikiria Muswada wa Sheria ya Afya ya Akili ya Mwaka 2008. Pia Kamati inawashukuru watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ufanuzi waliota wakati Kamati inafikiria Muswada huu. Aidha Kamati inawapongeza Wadau wote walioitikia wito wa kushiriki katika vikao vya mashauriano na kutoa maoni yao juu ya Muswada huu. Kamati inathamini sana mchango wao.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii ambao kwa kutekeleza wajibu wao katika kuboresha Muswada huu. Naomba kuwatambua wajumbe wa Kamati waliochambua Muswada kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Omar Shabani Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji ambaye ni Makamu Mwenyekiti.

Wajumbe wa Kamati ni Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mheshimiwa Pro. Feetham F. Banyikwa, Mheshimiwa Merce Emmanuel, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Hemed M. Hemed, Mheshimiwa Janeth B. Kahama, Mheshimiwa Dr. Christine G. Ishengoma, Mheshimiwa Susan A. Lyimo, Mheshimiwa Haroon Ali Suleiman na Mheshimiwa Martha M. Mlata,

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Dr. Samson F. Mpanda, Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwiomba, Mheshimiwa Dr. Lukas Jelas Siyame, Mheshimiwa Fatma Abdullah Tamim na mimi mwenyewe Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalize kwa kumshukuru Kaimu Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kashililah na Ofisi yake kwa kuihudumia vizuri Kamati yangu katika kutekeleza majukumu yake.

Aidha napenda kumshukuru Katibu wa Kamati hii Ndugu Hosiana John kwa kuratibu vikao vya Kamati hadi maoni ya haya kutoka katika muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono Muswada huu na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Dr. Mwita Haji Mwita, kwa kuwasilisha vizuri taarifa ya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, nina udhuru kidogo namwomba sasa Mheshimiwa Naibu Spika, aendeleze shughuli ambazo zinafuata hivi sasa.

Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa nitamwita Msemaji kutoka Kambi ya Upinzani, anayeshughulikia Muswada huu. Mheshimiwa Dr. Tarab Ali Tarab. (*Makofi*).

MHE. DR. TARAB ALI TARAB - MSEMADI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu Muumba wa vyote kwa kunijalia uzima, Pili nikushukuru wewe kunipa wasaa huu kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu muswada wa Sheria ya Afya ya Akili ya mwaka 2008, *The Mental Health Act. 2008*. Kwa mujibu wa kanuni za Bunge, kanuni ya 86(6) toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kutoa pole kwa Kiongozi wetu wa Upinzani Bungeni Mheshimiwa Hamad Rashid ambaye amerejea kutoka nchini India kwa matibabu. Mwenyenzi Mungu amponye haraka kutohakana na upasuaji mkubwa aliyofanyiwa hivi karibuni na aweze kurejea kwenye majukumu yake ya kawaida mapema.

Sambamba na hilo natoa pongezi kwa uongozi mzima wa Kambi ya Upinzani kwa mshikamano iliouonyesha katika kipindi hiki cha Bunge ambacho kimekuwa na mambo mengi yaliyohitaji ushirikiano wa pamoja ili kutimiza yale ambayo watanzania wanategemea toka kwetu. Aidha nakupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuliongoza Bunge hili kwa mujibu wa kanuni na taratibu tulizojiwekea sisi wenywewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho wa Pongezi lakini kwa umuhimu ni kwa Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Prof. Mwakyusa pamoja na Naibu wake pamoja na timu ya wataalam wa wizara hii kwa kuleta Muswada huu na jinsi walivyokubaliana na hoja mbalimbali za wadau pamoja na wajumbe wa kamati katika kuhakikisha muswada huu unakidhi matakwa kama vile ulivyokuwa

umekusudiwa. Kwa ujumla Kambi ya Upinzani haina pingamizi na kupitishwa kwa muswada huu na Bunge na kuwa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uhalisi uliyopo, je ni kweli mgonjwa wa akili anaweza kujielewa naye akajipeleka hospitali ili atibiwe? Kambi ya Upinzani inaomba kweli tuliangalie suala hili kwa uhalisia wake na sio kama mswada unavyosema katika kifungu cha 4(1) nanukuu: “*Any person who has attained the apparent age of eighteen years and voluntarily submit himself for the mental disorder treatment, shall be accepted to such mental health care facility*”, mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu 9(1) cha Muswada huu kinachotoa majukumu kwa viongozi wa dini askari polisi watendaji wa mitaa na kata na pale wanapoamini kuwa mtu ana ugonjwa wa akili kumpeleka kwenye kituo cha matibabu. Kambi ya upinzani inauliza je watu hao wanaopewa majukumu na sheria hii tayari wamepewa taarifa ya majukumu hayo? Na je wamepewa mafunzo ya jinsi ya kuwashughulikia au kuwa-handle wagonjwa hao hadi kituo cha matibabu? (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Waziri akito mapendekezo ya Muswada kwenye Kamati ya Bunge alisema kuwa Wizara kwa kushirikiana na sekta nyingine itaweka mipango mahususi ya kutoa miongozo ili kuboresha elimu ya kinga dhidi ya matumizi ya madawa ya kulevyta na vilevi vyengine vinavyochangia ongezeko la magonjwa ya akili nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kambi ya upinzani inauliza kwa kuwa matumizi ya madawa ya kulevyta ni kosa la jinai, na Wizara ya Mambo ya Ndani kisheria ndiyo inayoshughulika na masuala yote ya makosa ya jinai na isitoshe kuna kitengo katika ofisi ya Waziri Mkuu kinachoshughulikia madawa ya kulevyta, Je, kwa Wizara ya Afya kuweka kitengo cha kushughulikia suala hilo si kugawanya nguvu zetu chache tulizonazo kama Taifa? (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani nawashukuru Waheshimiwa wote kwa kunisikiliza na naomba kuwasilisha, ahsante. (*Makofit*)

NAIBU SPIKA: Huu Muswada una wachangiaji wachache tu. Kwa hiyo, tunafikiri waliofikiri wenzao wamejiandikisha wengi, hawajajiandikisha wengi. Kwa hiyo, mnakaribishwa Waheshimiwa Wabunge. Kwa kuanzia tu huyu ninayetaka kumwita simwoni humu ndani ya ukumbi. Sasa badala yake nitamwita Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo. Huyu ni wa pili na Mheshimiwa Prof. Dr. Mtulia yupo na Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, ndiyo waliojiandikisha.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niwe wa kwanza kuchangia Muswada uliopo mbele yetu. Kwa kweli sina mambo mengi nitasema kwa ufupi tu. Kimsingi ni kwamba mimi naunga mkono kwa asilimia moja kuletwa kwa Muswada huu hapa Bungeni. Kwa sababu natambua kuwa afya ya

akili ni moja ya afya ya msingi, lakini sekta hii ina matatizo ya kukosekana kwa dawa endelevu na kwa ujumla suala zima za afya ya akili ina matatizo. (*Makofi*)

Ikumbukwe kwamba afya ya akili ni *cross cutting issues*. Ni suala mtambuka kwani maisha yetu ya kila siku uwe katika kutafuta umaskini au utajiri na mambo mengine yote huzaa tatizo ya magonjwa ya akili. Hivyo ningependa kushauri.

Kwanza, Serikali kwa maana Wizara hii iweke mkakati na msukumo mkubwa wa Bajeti ya kutosha kwenye eneo hili. Lakini pia kama nilivyotangulia kusema eneo hili lina matatizo ya kutokuwa na wataalam wa kutosha. Nashauri Wizara ya Afya ianzishe mtaala utakao walazimisha kila kunakoendeshwa kozi ya *Medical Officers* basi kuwe na mtaala unaohusu afya ya akili. Hii itatusaidia kuwafikia Watanzania wengi vijijini kule na katika hali hiyo kwenye zahanati zetu kule vijijini na kwenye vituo vyetu nya afya kuwe na wataalam katika hali iliyoko sasa ambayo kwenye zahanati unamkuta mtu yuko yuko tu ana fani nytingine anasaidia saidia pale. Lakini kwenye suala la afya ya akili hajui kitu ina tulazimisha kwenda mbali ama uende wilayani au mkoani au Mirembe. Jambo hili kwa kweli linapunguza nia nzuri ya kuhudumia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko jambo lingine ningependa nishauri kwanza bahati nzuri mimi nilifanya Wizara ya Afya pale kazi *Section* ya afya ya akili pale katika hali ilivyo haiwezi kusaidia sana. (*Makofi*)

Mimi nashauri, Serikali ianzishe kwa makusudi mazima *Directorate* ya afya ya akili, jambo hili litatusaidia sana kufika kwa sababu *Directorate* ipo watagawana kazi watafika vijijini kwa urahisi watafika katika wilaya kwa urahisi. Lakini katika hali iliyoko sasa ambayo Dr. Mbatia pale yuko chini ya mtu hawezi kujitanua ipasavyo au hata mkuu wa *section* nytingine akiwepo pale mpaka upate ruhusa ya Dr. Barege ambaye sasa ndiye *Director* wa *Hospital Services* pale mimi naiona ipo ngumu kidogo. Tuwaanzishie *Directorate* ya kwao wafanye kazi vizuri na tuweze kuwahudumia wananchi kwa urahisi.

Lakini pia liko jambo la sera iliyopo, nadhani tunafuata sera ya *World Health Organization (WHO)* ya kwamba kuna baadhi ya madawa au *Group A or Category A*, dawa au *Category B*. Kuna dawa ambazo hazitakiwi kwenda vijijini kule kwa maana ya zahanati au kwenye Wilaya. Mimi nafikiri katika eneo hili tuweke *exception* kidogo tutengeneze *exception rule* kwamba zile dawa zinazohusu wagonjwa wa akili ziende moja kwa moja mpaka kwenye ngazi ya vijijini. Hii itaturahisishia sana suala zima la kutoa huduma kwa wagonjwa wa akili.

Lakini lingine ambalo ningependa kushauri, kwenye Muswada ukiangalia nimepitia haraka haraka lakini kuna mahali wanataka *religions leaders* kuwepo pale. Mimi naona katika utekelezaji wa jambo hili lisije likatuletea matatizo mbele ya safari. Kwa sababu inatamka tu *religions leaders* haisemi labda muislam au mkristo, na huko mbele tunaweza hata kuanza kubaguana ameweka muislam tu au ameweka mkristo tu. Kwa hiyo, basi katika kutengeneza jambo nzuri tu-specify kabisa kwamba *religions leaders* wa kwenye bodi hii watakaohusika basi mmoja awe muislam mwingine awe

kiongozi wa dini ya kikristo itaondoa *segregation* huko mbele au malalamiko yasiyo na sababu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwisho nichukue nafasi hii kuipongeza *non-governmental organization* iliyoko Mtwara inaitwa *Basic Needs* wamejihuisha sana na suala hili la *Mental Health Care*. Na wamewahi kufika jimboni kwangu kuna mzee alikuwa yaani mgonjwa kabisa ni wa kumfunga kamba wakati wote lakini wamekaa naye wamemsaidia sana sasa hivi ana afya yake amerudishwa kwa ndugu zake anaitwa Mzee Adam. Niliona nitumie nafasi hii kwa sababu tunaongelea suala la afya ya akili na mchango wao kule Mtwara *Basic Needs* ni mkubwa niliona nisiachie hapa angalau nigosie utendaji wao mzuri ambao umesaidia wagonjwa wengi kupata afuanu na hasa Mzee Adam ambaye alikuwa hajiwezi kabisa sasa ni mwenye afya nzuri anajitambua, anakula na anafanya shughuli zake za kila siku. Kwa kweli mchango wao ni mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana nilisema leo nina machache tu ni hayo ahsante. (*Makofi*)

MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Hakika ni nafasi adimu utaona hata Bunge lako linapwaya sana hii shida wanadhani iko kwa yule.

Mheshimiwa Naibu Spika,....

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, ngoja tukusahihishe hapo tumeshaelezwa kwamba wajumbe wengi wamekwenda kwenye Kamati mbalimbali. Karibu Kamati sita hivi zinakutana kwa ajili ya kazi muhimu. Kwa hiyo, sio kuwa wameudharau Muswada huu.

MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA: Ahsante kwa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Wizara, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, watendaji wa wakuu pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kwa kutueltea Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Huduma ya Jamii na tumetoa mawazo yetu katika Muswada kwa hiyo sitakuwa msemaji sana, ila nimesimama hasa kuongeza uelewa wa tatizo lenyewe la afya ya akili. Kwa kweli tafiti nyingi zilizofanywa dunia nzima, zimeonyesha kuwa wanadamu wote wanaYo asili ndogo ya matatizo ya afya ya akili.

Tatizo linalotupata sisi ni kile kiwango tu, pengine kama mtu wa kawaida ukimweka katika hali fulani anaweza kabisa kabisa aka *break down* na akapata matatizo ya afya ya akili. Kuna wale wenzetu waliozaliwa na matatizo ya afya ya akili ya aina ya wasiwasi, wale wako wengi sana na takriban na sidhani kama yuko mtu anaweza kukosa kuwa na wasiwasi. Kwa hiyo, Ninasema tu kwamba hii shida iko kwa wingi na tuanze sasa kukubali tufanye nini ili tuweze kuidhibiti.

Lingine ni kwamba kuna shida ya magonjwa ya akili inakuja *acutely* yaani kwa dharura. Nimeshashuhudia wagonjwa na magonjwa kama homa za malaria, *typhoid* au homa ya aina yoyote ile. Hao wagonjwa wanaweza kubadilika kabisa na wakuvua nguo, kutukana watu hata kuweza kuua.

Lakini baada ya shida ile kutibiwa mgonjwa yule anarudi anakuwa salama. Kuna wagonjwa wengine wa magonjwa ya akili ya kudumu ya muda mrefu, hawa kwa bahati mbaya wanatokana na asili wazazi wao wana asili ya ugonjwa wa akili hasa ya *schizophrenia* au ya *Mania*. Kwa hiyo, mtoto akizaliwa katika familia ile anaweza baadaye akaumwa ugonjwa huo. Na kwa bahati nzuri kwamba magonjwa haya yote sasa yanatibika. Lakini tatizo lenyewe kubwa na hatujui ukubwa wa shida hii. Hivi ukiuliza kuna wagonjwa wangapi wenye matatizo ya afya ya akili, ni tabu kujibu.

Kwanza ni wengi wanajificha na wale wachache wanaokuja hospitali tu labda ndiyo tutapata takwimu zao na hili jambo nilikuwa nataka nilisisitize kwamba Wizara itafute namna fulani ya kuweza kufanya tafiti itakayotuambia sisi Watanzania wacha wale wanaokuja hospitali, wale walio majumbani hivi wako wangapi wagonjwa wenye kuumwa matatizo ya akili. Jambo hili ni gumu sana, lakini lazima tulifanye.

Kwa vile ugonjwa huu watu wengi wanao tatizo linalonikuta mimi ni ule unyanyapaa tulionao kama wana jamii. Tuna majina mabaya mengi tu ana wazimu huyo, kichaa, basi mambo zimeshafyatuka, mimi naona majina kama haya tungejizuia kwa sababu kwa kweli ile ilijifyatuka kwa yule bwana, kesho inaweza ikafyatuka kwako.

Tutafute namna bora ya kuwasaidia hawa kwa kuondoa unyanyapaa na mimi katika suala hili ambalo liko katika Muswada, tutauondoa unyanyapaa tu kama tukiweza kuwaelimisha wana jamii wetu kwamba hii shida ya afya ya akili iko miongoni mwetu kwanza haimbukizi. Wale wanaopata magonjwa mengine ya kuumia ubongo, au kupata kansa ya ubongo au jibu katika ubongo hao wanatibiwa.

Lakini haiwezekani leo mgonjwa aliyepata *acute brain syndrom* yaani anakuwa kama mwendawazimu kabisa kabisa, hashikiki, leo huyu tunamuona sio mwenzetu tena leo yaani tunamdhara. Mimi nilikuwa nadhani njia bora ni kuelimisha jamii juu ya magonjwa haya. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani Wizara ikubali kuwa na kitengo kabisa cha afya ya akili ya jamii juu ya matatizo ya akili kitengo hicho kitumie pesa nyingi kuelimisha wananchi na hiyo itatupa sisi faraja kubwa, tunaweza kabisa kupunguza tatizo la watu wengi wanaoumwa ugonjwa huo hawatibiwi na wale wanaotibiwa wananyanyapaliwa na hata mali zao kuharibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni dhumuni kuu la kutibu ugonjwa wa aina yoyote ile. Nayo ni kumsaidia mgonjwa arudi katika afya yake ya kawaida na aweze kuendelea na shughuli zake, *rehabilitation*. Ninaomba sana Serikali itumie nafasi kubwa kuweza kuwafanya hawa wagonjwa wa afya ya akili waweze kurudi katika *community* ili ufanye hivyo itakuwa lazima upate kundi kubwa la wafanyakazi wa afya ya akili ya

jamii. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba kitengo hiki kiongezewe nguvu na watu waende katika vijiji wakaongee na watu.

Watatuambia tu *level* za magonjwa ziko vipi lakini muhimu ni kwamba mgonjwa ambaye alikuwa na hali mbaya ametibiwa akili zake zimerudi, huyu asipewe jina tu anawazimu anawazimu, hapana. Tunaomba aanze kupata nafasi ya kurudi katika hali yake ya maisha na watu waweko wa kupita na wanaweza kuwapa dawa mara moja kwa wiki, labda na dawa zake ziko kiasi gani na anaendelea kula. Tunaweza kabisa tukapata faida kubwa ya kuwatibu watu hao.

Ili ufanikiwe sana Mheshimiwa Waziri lazima tukupigie debe upande wa bajeti. Kwa kufuata Azimio la Abuja, *The Abuja Declaration*, wakuu wetu wa Afrika wamekaa Abuja na kutamka kwamba ili tuweze kusaidia kutibu magonjwa yaliyoko katika nchi zetu, lazima Wizara hizi za afya zipewe hata kwa uchache asilimia 15 ya bajeti ya taifa. Sasa mwaka huu tumepewaa nadhani takribani asilimia 10.5 au 11, lakini bado tunaiomba Serikali iongeze bajeti ili bajeti hiyo uitumie sana pamoja na mambo mengine kusomesha kada ya *community mental health workers* ambaa watapita sehemu nyingi na kuweza kuwasaidia watu wetu. Sasa nilikuwa nataka niseme kwa msisitizo, ninaomba sana sana wakati ufile sasa watu wailewe afya ya akili ni ugonjwa wa watu wengi na yeye anaweza akawemo, siku moja tuache unyanyapa kabisa na kwamba kada hii ya *community workers* watakwenda vijijini kusaidia wagonjwa wenye matatizo ya akili. Kama alivyosema mse maji aliye pita kwamba sasa iwe *mandatory* kwamba shule zote za *medical assistant* na uuguzi kuwepo na mafunzo ya afya ya akili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante Profesa Mtulia, kwa kutusaidia kujua kwamba sisi wote tuna matatizo hayo ila ni kiwango tu wewe unamkuta mtu anakuwakia hasira usishangae ujue tayari zimechemka. Kwa hiyo, nadhani hilo la muhimu sana. (*Makofii*)

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia Muswada huu wa Afya ya Akili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru sana kwa Muswada huu kwa sababu mara nyingi tunapotunga sheria zetu tunawahi hasa kujifikiria sisi ambaa tunaamini ni wazima na tunakuta tumejisahau kutoa kipaumbele kwa makundi maalum kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawajibika kusema kwamba kundi hili ni kundi ambalo linatakiwa liangaliwe kwa jicho la huruma sana, kwanza kundi hili ni kundi ambalo limekosa hata haki ya msingi ya kuweza kupiga kura kwa mujibu wetu wa katiba. Kwa mujibu wa kifungu (5)(2)(b) kinasema kwamba mtu asiyeha na akili timamu hataruhusiwa kupiga kura.

Lakini wakati huo huo pia kifungu (9) kinazungumzia umuhimu wa kila binadamu au kila mwananchi kuweza kuheshimiwa na kuthaminiwa kadri inavyostahili katika nchi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nimeanzia na nafasi kwanza kabisa wote tunakiri kwamba mtu akishakuwa na ugonjwa wa akili hasa yule aliyefikia kiwango kikubwa ni kwamba hajitambui inavyostahili. Lakini kwa mujibu wa makosa ambayo yanajitokeza baada ya mgonjwa huyo kwa mfano amefanya mauaji anapelekwa mahakamani kama kawaida na akifika kule kesi mwishoni wakishamthibitisha waseme kwamba huyu ameua bila kukusudia kutokana na h ali yake. Sasa mimi hayo yote nayachukulia kwamba ni kumwongozea mateso huyu ambaye tayari imeshajulikana ni mgonjwa hasa mara ya mwisho nilivyoona kwamba yale yaliyojitekeza pale Muhimbili ikibidi tufanye hivyo na wakati tayari kwenye hospitali. Nilikuwa nafikiri ikiwezekana hata kabla ya kupelekwa Mahakamani basi uanze kufanyika uchunguzi kabisa ili ikithibitika kwamba huyo mtu ana ugonjwa kweli wa akili basi hana haja ya kupelekwa mahakamani wakati tunafahamu hana akili timamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hilo pia katika kuthamini utu wa mwanadamu nimeangalia hasa katika maeneo mbalimbali tunayotoka kwenye vijiji jinsi ambavyo mgonjwa wa akili anaachwa wakati mwingine anachapua tu taka taka unakula wakati mwingine hata nguo alizovaa hazistahili hata kama hana akili timamu ni kwamba utu wake uko pale pale. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria yawezekana ni kwa ajili ya hofu yetu ya kumkaribia mtu asiye na akili timamu. Je hatuwezi kufanya bidii ya kuongeza watu ambao watakuwa na utaalam wa kumchukua mtu kama huyo na kumhifadhi. Wakati mwingine ukishaonekana tu akili zako zimekuwa za aina hiyo basi ni kamba zile nzito au kamba zinazokata ndiyo anafungwa mgonjwa kama huyo kwa ajili ya kupelekwa hospitalini. Na wanaofunga wanashahau kwamba pia wanampa majeraha na maumivu mengine. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kwa kweli utumike utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba mgonjwa kama huyo anashughulikiwa bila kuongezewa maumivu yanayozidi. Jambo jingine nililokuwa nalifuatilia ni kutokana vilevile na uzoefu tuliuopata mara ya mwisho pale Muhimbili kwamba wagonjwa walikuwa pamoja kukatokea kukawa na ile hali iliyojitekeza mpaka ikafikia kwenye mauaji. Sasa nilikuwa najaribu kufikiria kwamba kwa kuwa inaeleweka mgonjwa asiye na akili timamu anaweza akatumia kifaa ambacho kina hatari kuweza hata kuhatarisha maisha ya mwenzake. Je, hizo wodi ambazo tunazijenga kwa ajili ya wagonjwa kama hao, si zingekuwa pengine na utaratibu mzuri wa kuweka hata wakawa kwenye chumba peke yao ili kila chumba angalau tunakuwa tumepunguza ile *risk* ya yeye kuweza kuleta madhara kwa mgonjwa mwingine. Lakini ile hali ya kuwaweka pamoja wakati huo labda mwingine anahitaji kutundikiwa dawa, kwa kweli hata yule *nurse* kukaa mle ndani peke yake na hali kama ile inakuwa pia ni hatarishi kwake.

Kwa hiyo, nilikuwa naona kama imezingatiwa kwenye Muswada bahati mbaya sijaupitia wote basi hilo suala ni la msingi kuzingatia kwamba wodi zinazotayarishwa kwa ajili ya wagonjwa wa aina hiyo ziwe ni wodi *special* ambazo zitasaidia kupunguza hatari ya kuweza kuumiza wao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine ambalo nilikuwa napenda nilizungumzie ni kiwango cha hali ya afya zisizo na akili katika jamii, visababishi ni nini, Mheshimiwa Naibu Waziri wakina mama tunafahamu, mtoto anapokuwa amechelewa kuzaliwa, akafikia wakati mwingine akanywa hata maji kwa vyovoyote vile ubongo wake wanasema unakuwa na hitilafu. Kwa msingi huo nilikuwa nazungumzia kwamba matatizo hayo mara nyingi yanawapata hasa akina mama wenye umri mdogo, tumeshasema mara nyingi kuhusu sheria ile ambayo itamwezesha mtoto wa kike angalau aweza kuolewa akiwa na umri wa zaidi ya miaka 18. Lakini sheria hiyo mpaka leo haijaletwa, matokeo yake tunashindwa hata pa kusimamia ili kuweza kudhibiti afya za mabinti ambao wanajifungua kabla ya umri wakati mifupa yao haijakomaa na hivi kuwa ni hatarishi kwa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sambamba na Muswada huu ili kuweza kupunguza kiwango cha ongezeko la watu wenye akili isiyofaa basi ni vyema Muswada huo ukaletwa mapema ikibidi hata kwa dharura ili tuweze kuupitisha na kuweza kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nilikuwa nafuatilia mambo mengine ambayo yanababisha ongezeko hilo, si mara moja tunasikia wakati mwingine unakuta watoto wamefikia hata kujinyonga kwa ajili tu ya mazungumzo yaliyojitekeza kwenye familia au pengine hata mifarakano ya kwenye familia. Lakini ilikuwa mara ya mwisho niliwahi kuulizia kuhusu vituo vya kuweza ku-*council* yaani kutoa ushauri nasaha kwenye familia ili kuweza kupunguza tatizo kama hili. Lakini mpaka leo sijasikia kamili mpango mkakati ni upi na si hivyo tu vilevile wakinamama angalau huyu ambaye anakua asiye na akili timamu ameshaonekana mtaani inakuwa ni rahisi watu kumwonyesha kwamba yule pale ana tatizo akasaidiwa.

Lakini akina mama kuna wakati tunakuwa na ukatili, mtoto amezaliwa akili zake labda pengine hazijawa nzuri nikisema mama namaanisha pia hata baba kwa sababu mtoto sio wa mmoja. Unakuta mtoto yule kuhakikisha kwamba wale wanaoweza kutibiwa na kuweza kupona angalau kupunguza yale matatizo basi waweze kutibiwa na wale ambao haiwezekani basi tuwajali na kujuu kwamba wao hawakujitakia na kama alivyoongea Prof. Mtulia ni kwamba hali kama hiyo inaweza ikampata mtu mwingine yoyote yule na wakati wowote ule.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana akina mama tujitokeze tunapokuwa na watoto wa namna hiyo ili kuhakikisha kwamba wale wanaoweza kutibiwa na kuweza kupona angalau kupunguza yale matatizo basi waweze kutibiwa na wale ambao haiwezekani basi tuwajali na kujuu kwamba wao hawakujitakia na kama alivyoongea Prof. Mtulia ni kwamba hali kama hiyo inaweza ikampata mtu mwingine yoyote yule na wakati wowote ule.

Kwa hiyo, ninaloomba sana kwa jamii tuchukuliea kwamba tatizo ambalo kweli linaweza likampata mtu yoyote yule na tunaomba sasa katika semina nyingi zinazoendeshwa mara nyingi zinakuwa katika maeneo ya mijini kule vijijini haziendi. Wakiitwa wataitwa tu wale viongozi wale wenye ambao wanahusika moja kwa moja hawapati zile semina. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nashauri sasa hivi tutoke katika ngazi ile ya mikoa au wilaya peke yake tuanze kupita hata kwenye vijiji au kwenye Kata ili wale wananchi waweze kusikia moja kwa moja ni jambo gani linahusiana na sheria ili

kuweza kusaidiwa kwa sababu kimsingi wote tunatambua kwamba kutokujua sheria hakumaanishi unapunguziwa kosa.

Kama ndivyo hao watu tunavyowasema kwamba hawajatekeleza, wakati sheria hizo wanakuwa hawajaelimishwa. Kwa hiyo, misingi hiyo mimi naona haki inakuwa haijatendeka kwa sababu tumemtegemea mtu afanye lile ambalo hajaweza kulifahamu. Sasa wakati umefika kwa Serikali yetu kuweza kupanga mkakati kwenye Bajeti zetu ili sheria hizi ambazo tunazitunga zisiishie tu kwa ajili ya tukio moja ambalo limejitokeza bali kweli ziwafikie wananchi ili ziweze kutimiza yale matakwa ambayo yako kwenye sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo niseme kwamba naunga mkono hoja na nashukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, umesahau kusema kwamba, saa nyingine mtoto akizaliwa wa aina hiyo, baba anamkimbia mama na mtoto wake anamwacha hapo hapo, ipo nayo hiyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Pindi Chana na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, wajiandae na msemajji wetu wa mwisho nafikiri ni Mheshimiwa Beatrice Shellukindo.

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia na niseme tu kwamba, nimewajibika kuchangia kwa sababu jana Bunge lako Tukufu, lilinichagua kuwa Mjumbe wa Baraza wa Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya Muhimbili. Kwa hiyo, kwa mara nyingine tena, nashukuru sana na niliahidi kwamba, nitakukwa kiungo barabara kati ya pande hizi mbili. Kwa hiyo, nalishukuru sana Bunge lako Tukufu, lakini vilevile nawashukuru sana wale walioniwezesha kuingia katika nyumba hii, yaani Wananchi wote wa Iringa hususan Wanyalukolo wote nawashukuruni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili la afya ya akili, kwa maoni yangu ni jambo nyeti sana, kwa sababu ndio eneo ambapo hatma ya mtu inaposimamia. Mwananchi anahitaji maisha na wakati mwingine maisha bora na ili awe na maisha bora, anahitaji uwezo (*capacity*). Sasa akishakuwa hana uwezo wa kufanya maamuzi, afya nzuri inakuwa ni tatizo na tumeshirikishwa hapa kwamba, wakati mwingine jambo hili linakuwa katika viwango; kuna mwingine ameathirika sana, mwingine ameathirika kidogo. Kwa hiyo, mimi binafsi naona hili jambo ni nyeti sana katika nchi yetu, kwa hiyo, ninaunga mkono hoja ya kuleta Muswada huu, wakati huu ni barabara na maboresho yaliyokuwemo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili linahitaji mashirikiano ya wadau, linahitaji mashirikiano ya vyombo vyote husika. Katika kutatua na kuboresha jambo hili, tunahitaji ushiriki wa vyombo vya dola, kwa mfano, Polisi wakati mwingine ndio wanaotakiwa kuandika taarifa mbalimbali, vyombo vya afya, tunahitaji Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Sasa hivi utakuta Mashirika mengi yasiyo ya Kiserikali ni kama Mashirika ya Dini, ambayo yanajitolea kuhudumia watu kama hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukulia nchi zilizoendelea, tatizo hili wameliangalia kwa mtazamo tofauti; wanavyo vyombo kwa mfano, hutamkuta mtu mwenye tatizo la akili anatembea barabarani kwa sababu akitembea barabarani tu anaweza akagongwa. Kwa wanawake anaweza akabakwa au kupata matatizo mengi ya hatari zaidi. Kwa hiyo, ni muhimu sana Wizara tukatafakari ni vyombo gani vinapaswa vishirikishwe na ni nani mwenye uwezo na mamlaka, kwa mfano, wale wenyewe matatizo ya akili wanaotembea barabarani kuweza kuwachukua na kuwapeleka katika huduma hizi za afya wakapata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ipo haja ya kulitazama sana. Sasa kuna suala la mafungu, yaani fedha, tunahitaji mafungu ya kutosha kwa sababu huduma hii nyeti inahitaji wito, inahitaji wataalam wa kutosha na wakati mwingine kusipokuwa na vitendea kazi, wodi za kutosha katika hospitali zetu nalo ni tatizo. Inaweza ikatokea kabisa, mgonjwa huyu anachanganywa na mgonjwa mwingine ana *degree* kubwa ya *psychiatry*, mwingine *degree* ndogo, yule mwenye tatizo kubwa anachukua chombo anamgonga mwingine, yule mwingine hawezu kuinuka kujiokoa mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunahitaji vyumba vya kutosha, tunahitaji wahudumu wale wa afya za akili wa kutosha, wenyewe wito, wenyewe kujitolea na wakati mwingine matatizo haya ya afya ya akili, unahitaji hata wataalam wa masuala ya kiroho, wanaotoa huduma za kiroho, yanasakiwa wakati mwingine kutoa ushauri. Kwa hiyo, nilidhani ipo haja ya kuangalia maeneo haya, wale wadau washirikishwe na Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali, watazame sasa ni jinsi gani wanaweza wakahudumia eneo hili kwa ufasaha zaidi, Serikali itoe wito kupitia vyombo vyake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia huduma hii muhimu katika nchi yetu ni muhimu sana ikawepo hata katika ngazi ya Serikali za Mitaa. Msemaji aliyepita amezungumza na mimi niseme kwamba, hospitali zetu zote za Wilaya, kwa sababu huko ndiko wananchi wapo, kwa mfano, Hospitali ya Njombe unayotoka wewe Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo na wodi na huduma. Wananchi wakifika Wilaya ya Njombe wakihitaji huduma ya afya ya akili, wasiambiwe waende Hospitali ya Mkoa wa Iringa au Muimbili Dar es Salaam. Huduma hizi ziwepo katika kila Wilaya iwe ni Makete, iwe ni Rudewa, kote katika ngazi za Wilaya na wataalam wale wawepo kama ni wa kutoa ushauri na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sasa hapo kuna suala la mafungu, katika bajeti za Hospitali za Wilaya iwe ni *Basket Fund* katika Wilaya zetu, watazame ni jinsi gani wanaweza wakali-*accommodate* hilo na wakati mwingine hata kufanya sensa za watu wenyewe matatizo ya akili, itasakiwa zaidi tunavyozidi kwenda kiliboresha jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu pia kuangalia sababu zinazopelekea matatizo haya ya ugonjwa wa akili, wakati mwingine tukiangalia sababu itasakiwa kiliboresha jambo lenyewe, kwa sababu mtu anapokuwa na mgonjwa wa akili anapotibwa, wale wataalam wanakuwa na kitu kinachoitwa *goal*. Lengo lao ni kumtoa

huyu mtu mwenye tatizo hilo kumfikisha wapi; apone, aweje, aboreshwe vipi akili yake. Wakati mwengine unakuta mtoto amezaliwa vizuri, lakini kutokana na dawa za kulevy (drugs) au uvutaji wa sigara, ambapo ameanza mapema sana tofauti na umri wake, anapata hayo matatizo.

Kwa hiyo, zile sababu zinazopelekea matatizo ya akili ni muhimu sana Wizara ikatafakari na kushirikiana na vitengo husika, kuona jinsi ya kuboresha. Kwa mfano, wakati mwengine masuala ya ajali, mtu anaweza akapata ajali matatizo ya akili yakaongezeka. Kwa hiyo, vitu kama hivi ni jinsi gani tunaweza tukapunguza ajali, ipo haja wadau mbalimbali waweze kushirikishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia suala la wazazi, maeneo Muswada umeeleza kwamba, endapo mtoto atakuwa chini ya umri wa miaka 18, basi anaweza akapokelewa kupidia mlezi au mzazi wake katika kile kituo. Kwa hiyo, ni vizuri sana wale wataalam wetu wanapopokea wagonjwa kama hawa, wakachukua historia ya kutosha kwamba ilianza lini na kwa sababu gain, ili kupunguza matatizo kama haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa mara nyingine tena, niseme ninaunga mkono hoja hii na ni jambo jema sana lakini suala la kuwawezesha kimapato vitengo hivi na Wizara hii ni jambo la msingi sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba kuchukua nafasi hii kwanza, kukushukuru kwa kunipatia nafasi muhimu, niweze kuchangia Muswada uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na wataalam wake wote, kwa kuleta Muswada huu muhimu kwa ajili ya kuangalia kundi hili la Watanzania. Mengi sana niliyotaka kuzungumza yamezungumzwa na wenzangu, kikubwa nitasisitiza baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naijiliza maswali mengi kila nikipita maeneo mbalimbali ya mikoa tofauti; kwa nini tatizo la ugonjwa wa akili linaongezeka? Ukiangalia miaka ya nyuma, kwa mfano, miaka miwili au mitatu iliyopita, nimekuwa natembelea mkoa mmojawapo ambao nimekuwa ninau-target na kuangalia suala hili kwa makini ni Mkoa wa Morogoro ...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa usisogee sana kwenye *microphone*.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Kwa hiyo, kila ukikaa miezi miwili, mitatu, ukienda unakuta ameongezeka mtu. Kwa hiyo, kama walikuwepo watatu utaona tena wamekuwa wanne, utaona tena wamekuwa watano. Swali langu kubwa ninauliza; kwa nini tatizo hili la ugonjwa wa akili linaongezeka? Zaidi kabisa unakuta kwamba, siyo wale wanaoanza utotonii wengi ni vijana. Kwa hiyo, mimi ninaweza nikahusisha tatizo hili la ugonjwa wa akili moja kwa moja na dawa za kulevy kwamba, pengine

uvutaji wa dawa unaongezeka, ndio sababu hasa tatizo la ugonjwa wa akili linaongezeka na kwa sehemu kubwa kwa upande wa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipita mijini na mitaani, kila mahali ni tatizo; badala ya kupungua linaongezeka. Ningependa kujuu Serikali imefanya utafiti gani kwa mikoa tofauti kuona ni kwa nini tatizo hili linaongezeka?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni la wagonjwa hawa wengi kuwa wanazunguka mitaani, kitu ambacho ni hatari sana; kwanza, wenyewe kwa usalama wao, kwa sababu mara nyingi tu wanakoswa koswa na magari barabarani. Hata mimi mwenyewe nikiwa naendesha gari, mara nyingi ninawakosa barabarani. Hii ni hatari sana kwa usalama wao. Pili, ni hatari pia kwa watu wengine, mara nyingine unaweza ukawa unapita mahali unaona watu wanakurupuka wanakimbia, kwa hiyo, ile ni hatari sana. Hata mimi mwenyewe mara nyingi tu ninakutana na mtu amechukua fimbo anakimbiza tu watu, kwa hiyo, inabidi ukimbie hujui hata ukimbilie wapi. Mimi naona ni hatari sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningeomba Serikali iandae utaratibu maalum na uwepo kuanzia kwenye ngazi za mitaa. Mabaraza ya afya yale yaanze kufanyakazi kuhakikisha kwamba, kila anapoonekana mtu mwenyeye tatizo hili na bahati mbaya hatambui anachofanya, basi aweze kuwekwa mahali maalum ili aweze kuwa na uangalizi wa karibu. Tofauti na wanavyoachwa wanazunguka ni hatari sana. Ninaomba Mheshimiwa Waziri, achukue *specific example*, kwa mfano, Mkoa wa Morogoro ni tatizo ambalo linaongezeka siku baada ya siku, maana mimi nimekuwa Mkoani Morogoro kwa muda mrefu, kwa hiyo, ninafahamu tatizo hili linavyoongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la watumishi hawa wanaowahudumia wagonjwa wa akili. Kama walivyotangulia kusema wenzangu, nadhani kwa kundi hili ambalo bahati mbaya mambo mengi wanayofanya wanakuwa hawayatambui ni muhimu sana tukahakikisha kunakuwepo na watumishi wa kutosha. Hili limekuwa linasababisha matatizo ya wagonjwa hawa kuumiza wengine, kama tukio ambalo limetokea hivi karibuni huko Muhimbili, ambalo lilisikitisha watu wengi. Ilionekana kabisa kwamba, mtumishi aliyekuwa anahudumia ile wodi aliondoka, akaacha wagonjwa peke yao.

Matukio yaliyotokea yamesikitisha na yameleta picha mbaya kwa Taifa. Kwa hiyo, tunaomba Wizara iwe na mkakati wa kuhakikisha kwamba, watumishi wanakuwa wa kutosha, pale ambapo nesi ametoka kwa ajili ya shughuli maalum, basi kabla ya kuondoka awepo mwengine ambaye anaweza kuangalia wagonjwa hawa ili kuhakikisha kwamba tatizo hilo halitokei tena kwa wagonjwa hawa ambao ni kundi muhimu katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kulisemea hapa ni kuhusiana na bajeti inayotolewa Serikalini, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, kundi hili linapata huduma. Pamoja na kuwa wana matatizo ya akili, lakini pia wanahitaji huduma zote muhimu. Mara nyingi unakuta wanatembea uchi, kwa kweli inatia uchungu sana.

Wanajiokotea tu vyakula nya kuokota huko mitaani, kwenye madampo, inakuwa haileti picha nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningependa kwa kutambua kundi hili, basi Wizara ihakikishe kwamba, inaweka fungu maalum kwamba, pale wanapokuwa kwenye familia zao au kwenye mitaa wapatiwe huduma zilizo muhimu. Litengwe fungu maalum, kwa sababu hawawezi kufanya kazi wakajitafutia kutokana na matatizo yao. Kwa hiyo, Serikali ichukue jukumu hili kuhakikisha kwamba, watu hawa wanapata huduma zinazostahili kwa ajili ya maisha yao, kwani wao ni binadamu na tunastahili kuwaangalia kwa jicho la karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa na fursa niweze kuchangia hoja hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, niseme tu ninaipongeza sana Wizara ya Afya, kwa kuja na Muswada huu. Kama waliotangulia walivyosema, tatizo hili unaweza usione kama ni la muhimu sana, lakini pale ambapo linakukuta katika jamii yako, utaelewa umuhimu wake na kwa hapa kwetu Tanzania, kama wenzangu wengine walivyosema, linajitokeza kwa kasi sana. Lilikuwepo pengine tulikuwa hatujui maana sehemu nyingi ambazo mimi pengine ninatoka, watu wengine wanaamini mtu kalogwa, kafanywa nini, lakini nadhani bado linahitaji *research* kama mwenzangu alivyosema kwamba, kwa nini matatizo kama haya yanaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile niseme tu ninashukuru sana kwamba, Muswada huu umeletwa na Wizara. Kwa wengine sisi ambao tunatoka vijijini sana, siyo pembezoni lakini maeneo ya ndani sana, unakuta huduma hii unashindwa ufanye vipi, wengine hatuna hata hizo Hospitali za Wilaya, tuna Vituo nya Afya na Zahanati, sasa mtu anapotokewa na matatizo kama haya, Mbunge unakuwa unafadhaika kwa sababu suala hili kama upo maeneo yale hujui hata usaidie vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi nitoe mfano wangu, nimewahi kuleta wagonjwa wasiopungua 12 katika Hospitali ya Mirembe kutoka Wilaya ya Kilindi na hii inabidi ifanyike kwa sababu huduma ya aina hii kwa pale karibu hakuna. Ukitsema umpeleke hospitali ya karibu zaidi, ambayo huwa tunaenda Hospitali ya Wilaya ya Handeni, bado ni mwendo wa kilometra karibu tisini na kitu, pia ile huduma yenye wataalam wale husika kwa kweli inakuwa ni tabu kuipata. Hata hivyo, ninashukuru kuwa wale niliowaleta waliweza kuhudumiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda kabla sijaenda kwenye Muswada wenyewe, nilikuwa niseme tu kwanza kabisa, tuangalie Muswada huu umekuja kwa wakati lakini huduma yenye ikoje? Kwa wengine ambao tumebahatika kupitia hospitali za watu wenye matatizo ya akili, husasan Mirembe ambapo mimi hupenda sana kwenda kuona wagonjwa tu hata kama sina mgonjwa wangu, kwa kweli unaangalia pale hali yenye inawezesha sheria hii hata ikipita kutoteklezeka? Wale watumishi kwanza, licha ya

kwamba ni wachache, ninadhani utaalam wao pia ni wa siku nyingi, hauendi na wakati, sidhani kama wanapewa zile *course* za mara kwa mara; wanafanya kazi kwa uzoefu. Katika yale mazingira wanayofanyia kazi, katika pita pita yangu katika maeneo hayo, niliwahi kukuta nesi ameumwa vibaya sana kwenye mkono na mgonjwa; je, wana bima? Anapewa dawa ya kutibiwa, anaenda anatibiwa kawaida anafungwa kidonda basi imeisha hiyo, hawa watu wanafanya kazi ya kujitolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Wabunge wenzangu, mtakubaliana nami kuwa, hata sisi wenyewe ukiwa na ndugu yako ambaye ana matatizo ya akili, penginepo kuna saa ambazo unamwogopa hata kulala naye chumba kimoja maana hujui atafanya lipi, sembuse huyu ambaye hana undugu naye, lakini amejitoa kwa sababu ya kazi yake na ni wito wake pengine kuweza kufanya kazi ya aina hiyo, lakini unakuta wanapata matatizo kama hayo. Sidhani kama wana bima, kipindi nilichopita waliniambia hawana bima sijui kama ilishapatikana kwa sababu niliongea na mamlaka husika sijui kama kuna lililofanyika? Hili ni suala pia la kuliangalia. Je, utaalam wao unaendana na wakati na aina ya wagonjwa wenyewe? Hilo ni jambo lingine pia la kuangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nadhani wapewe posho ya ziada ili kuwapa moyo kama motisha kwa kazi na mazingira magumu wanayofanyia kazi, ingesaidia. Wanajitolea siyo siri, ukiwaona utajua kweli hawa watu wana moyo; unakuta nesi mmoja kajifungia ndani ya wodi ya wagonjwa wenyewe matatizo aina hiyo, ambao hujui nani atafanya nini na kwa wakati gani. Mwingine anaamua tu kufanya kitu, kuna siku niliingia ndani nilitoka mbio, mgonjwa anaamua tu kunyanya kitanda, anataka kufanya vitu vya aina mbalimbali, sasa huyu anashinda mle ndani na hawa wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kuna haja pia ya kuangalia. Nimeona niyaseme haya, kabla sijazungumzia Muswada kamili ili tuone kama Muswada utatekelezeka. Tusipitishe tu sheria mradi tumepitisha, inabaki kwenye *record*, wakati haitekelezeki. Je, fedha za kuwahudumia wagonjwa zipo? Wagonjwa unakuta mara nyingine wanakula mlo mmoja, ukiangalia kile chakula kwa kweli yataka moyo, unaweza usitofautishe magereza na pale ingawa hata magereza hawastahili kupata chakula kibaya. Ninaweza kusema kwamba, tunahitaji kujuu kama fedha za kutekeleza haya ambayo yamo ndani ya sheria zipo? Je, huduma nyingine vitendea kazi visto kwa watu wa aina hii? Lazima tuangalie vitu vyote hivi, tusije na sheria lakini hali halisi inakuwa nini, tumepitisha sheria kwenye *records and then kinachoendelea* nini? Hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nilisema kwamba, nione angalau hayo mambo pia wanayaangalia vipi kwa wagonjwa wa aina hii, kwa sababu wagonjwa kama pale unakuta mara nyingine wanapata mlo mmoja kwa siku, ambao siyo mlo wa kutosheleza labda ni ugali na maharage, ugali na nyama au wali na nyama kitu kama hicho. Huyu mtu anatumia dawa za akili, ambazo ni kali mara nyingine inategemea na kiwango chenyewe cha tatizo. Dawa zenyewe zinatia usingizi, zinalegeza lakini akiwa na lishe nzuri inawezekana. Sasa kwa hali hiyo, ukiangalia nakuwa na wasiwasi sana kama vipengele vingine katika Muswada huu vitawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija sasa kwenye Muswada wenyewe, ukurasa ule wa nne, sehemu ya pili, kipengele cha 4(4), ukiangalia pale kipengele kinasema, *the Officer in charge of the mental*, hapa alikuwa anazungumzia kwamba, mtu ambaye anaonekana hana matatizo makubwa anaweza akaruhusiwa kurudi nyumbani. Sasa pale inaendelea “...*the Officer in charge of the mental health care facility shall insure the continuity of care on such person on out-patient basis,*” inawezekana? Tunao hao wataalam Sijawahi kuona hata mgonjwa mmoja wamemfutilia acha hao wa Kilindi amba ni mbali, hata hao wa mijini, hata wa hapa Dodoma Mjini, inawezekana tunao hawa wataalam maana yake vipengele vingine tusiweke kwa kuiga nchi nyingine amba pengine zina wataalam hao. Tuangalie hapa kwetu je, tuna uwezo huo; tunazo hizo fedha na utaratibu huo? Mungu anisamehe, lakini nasema hata kwenye magonjwa ambayo tunayo sasa hivi kama gonjwa la UKIMWI, bado kunatakiwa kufanywa huduma ya nyumba kwa nyumba ambayo hatuifanyi, pamoja na kwamba, fedha nyingi tunazo. Tumepewa misaada ya kila aina katika sekta hiyo, lakini haifanyiki kikamilifu; je, hapa sasa kwenye hii sekta ambayo wengi hawajaitilia maanani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nilitaka tu kutoa angalizo kwa baadhi ya vitu ambavyo lazima tuviangalie kwa karibu sana. Vilevile kuna aina mbalimbali ya matatizo ya akili; kuna mtu mwingine anaamua tu kunya maza ninyi mnakaa mnasema huyu mtu vipi? Amenyamaza tu lakini ni mgonjwa; je, tunao hao wataalam wa *ku-identify* aina hii ya wagonjwa; maana yake wengine unakuta wapo kwenye madaraka, wapo kwenye Mawizara na sehemu mbalimbali?

Wewe unafika unaongea na mtu kakasirika tu ana gubu, mwingine unashangaa haambili, ninyi mnasema huyu mkorofi kumbe mwenzenu ni mgonjwa; je, tunao hao watu wa aina hiyo? Sheria hii itakapopita tuna utaratibu gani amba tunafikiria kuufanya? Je, tutakuwa na wataalam wa aina hii kila Wizara, kila ofisi, labda kila taasisi wa kuchunguza kwa sababu mambo ni mengi sasa hivi, lazima tukubali maisha ya sasa na mazingira tuliyonayo, mara nyingine kichwa kinachanganyika. Mifano hii haipo mbali, hata humu sisi wenyewe mara nyingine mambo yanakuwa mengi tunachanganyikiwa; sasa je, katika hali hiyo tunasemaje kwa sheria hii? Mambo gani yanafanyika ili tuweze kuwa na wataalam wa kutosha wa kuweza kutambua wakati gani kuna nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia ukurasa ule wa kumi kwenye ile Bodi ya Afya ya Akili pale, mimi nilikuwa ninafikiria tatizo kubwa ambalo tunalipata tuna mambo mengi, tuna mikakati mizuri mingi, tuna mipango mizuri lakini tatizo mara nyingi linalojitokeza ni fedha. Siyo mara nyingine ni mara zote fedha hakuna; je, tunaonaje kama sasa hivi tukianza utaratibu tuanzie na hii *board* hapa tumuweke mtu mmoja mwakilishi kutoka Wizara ya Fedha, ambaye atakuwa kwenye hiyo *board*, atakuwa anajua kwamba hapa linapangwa hili na anaweza akasema jamani haya mnayoyapanga haiwezekaniki bajeti inatoka wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tangu pale mnaangalia sasa utaratibu mwingine kuliko inapangwa mipango mizuri, *board* zitakaa fedha zitatumika za vikao

vya *board* na utapoteza siku nzima, makaratasi halafu baada ya hapo hakuna fedha. Kwa hiyo, inabaki jamani tulikuwa na nia nzuri, lakini kulingana na bajeti na nini, mimi nilikuwa nadhani utaratibu mzuri sasa hivi tuwe na hawa wawakilishi kutoka Wizara ya Fedha. Natambua wazi katika Wizara ya Fedha, tunao watu ambao wanatuangusha, lakini hiyo siyo shida tunaweza tukairekebisha kule ili waweze kupatikana watu ambao watakuwa kwenye *board*. Hii *board* ningependekeza sana, kama iko *serious*, tumeamua kwamba sekta hii sasa itupiwe macho kwa umakini wake, basi mimi nilikuwa ninaomba sana na kipengele hicho kiweze kuongezewa mahali hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nilikuwa nasema suala la kuweka *records*, kwenye ukurasa wa 19 wamejaribu kuelezea *record keeping*. Sidhani kama *records* ziko sahihi. Nikimuuliza sasa hivi Mheshimiwa Waziri atupe takwimu ya wagonjwa wenye matatizo ya akili hapa nchini, sidhani kama atakuwa nayo kwa sababu wanatibiwa katika maeneo tofauti tofauti na inategemea nani ana uwezo wa kumfikisha mgonjwa wake wapi ili aweze kupata hiyo huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa ninadhani labda tungeimarisha kuanzia hapo, mwingine alisema Wizarani kuwe na idara au hata kama ni kile kitengo kiwe na *indent* tunajua kwamba, fulani na Fulani. Siyo Mama Shellukindo hapa anakuja anagombea siasa, mnaniweka baada ya miaka mitatu mnaona mwenzetu vipi mbona hatumuelewi, kumbe nina matatizo ya kichwa. Hakuna mahali penye *records* ambazo zinakuwa *confidential*, inatakiwa kuwe na kitengo, idara au sehemu ambayo Waziri ataona vyema kuwe na *record keeping* ya *people with mental problems*. Kwa hiyo, hata kama haijafahamika kwa kipindi kile, lakini wao wanakuwa nayo siri kama ilivyo kwenye baadhi ya magonjwa. Inapotokea jambo kama hilo, basi mnakuwa mnajua hilo au inatokea nafasi Mheshimiwa Rais anafanya uteuzi kwenye taasisi muhimu, halafu mnakuta tu mtu anawekwa lakini kwa sababu hakuna *record* na pengine kajitibia nje ya nchi alikuwa na hela, hakuna takwimu hapa nchini anaanza kufanya vitu vya ajabu ajabu kumbe mwenzetu ana matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani haya ya kwangu niliona niyachangie. Mwisho kabisa, kuna mahali hapa wamesema kwamba, watahusisha jamii; kuwe na mikakati ya kuihusisha jamii ili kuweza kusaidia na kushirikiana na kuondoa hili tatizo na kutoa huduma za aina gani kwa wagonjwa wa aina hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalam wa kazi hiyo katika jamii si Maafisa Maendeleo ya Jamii, mbona hamjawataja kwenye Muswada mzima? Hakuna mahali ambapo wanashirikishwa, mmeandika *social welfare* lakini kuna tofauti kati ya hawa *social welfare* wa ustawi wa jamii na maendeleo ya jamii, ambaye anaweza akakaa na mwananchi akampa zile mbinu. Anayejua amuingieje mpaka akubali na aelewé ni Afisa Maendeleo ya Jamii. Nilikuwa naomba pia na wao waangaliwe mahali ambapo wanawenza wakahuishwa, waweze kufanya hiyo kazi ili angalau hayo yanayokusudiwa yaweze kutekelezeka. Kwa kuwa nimeshiriki sana kwenye masuala ya matatizo ya akili, ninasema ninashukuru huu Muswada umekuja na Mungu awabariki, naomba utekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makofit*)

NAIBU SPIKA: Haku-*declare* kwamba na yeye ni Afisa Maendeleo ya Jamii, kwa hiyo, anapokwenda kule kuangalia, anatimiza wajibu huo. Ninakushukuru sana kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, tungeweza kumwita Waziri aanze kutoa majumuisho ya mjadala huu, lakini tukifanya hivyo tutakwama kwenye kipindi cha kupitia sheria kifungu na kifungu. Ili mtiririko uwe mzuri, nashauri tuahirishe halafu mchana Waziri akija tutaanza kutoa majumuisho halafu tutaingia kwenye Kamati ya Bunge Zima. Kwa hiyo, ninasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. DR. LUCY S. NKYA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kwa kuboresha Sheria ya Afya ya Akili. Ningependa kushauri yafuatayo kwa nia ya kuboresha:-

1. Ziwepo dawa za *maintenance therapy*; *Depo preps* mfano, *medicate* na *fluanxol Decarnoate*, ambazo zinasaidia sana kupunguza *relapse* ya *schizophrenics*.
2. *Establishment of Community Based Mental Health Services* kama inavyofanyika katika huduma za waathirika wa UKIMWI katika jamii (Hbc).
3. Tunahitaji kuongeza *Mental Health Rehabilitation Centres* kwa kila mkoa. Hii itapunguza sana uwepo wa *destitutes* kwenye mitaa yetu.
4. Ninaomba dawa za wagonjwa wa kifafa zipatikane kwa mtindo endelevu ili kuzuia athari za kuchanganyikiwa na kuwa *chronic psychotics*.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tunahitaji kutoa elimu ya afya ya akili kwa jamii, kwani bado wengi hawana uelewa sahihi kuhusu afya ya akili. Pia wanafunzi wa udaktari, bado hawapati mafunzo ya afya ya akili kwa uzito unaotakiwa.

Baada ya haya machache, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

(*Saa 06.37 Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)
(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wakati tunasitisha shughuli za Bunge asubuhi, wachangiaji waliokuwa wameomba orodha yao ilikuwa imekwisha na ikabakia mtoa hoja afanye ufanuzi wakati huu. Kwa hiyo, namwita sasa mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Karibu.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii tena ili niweze kuhitimisha hoja yangu.

Naomba nitoe shukrani zangu za dhati, kwa Waheshimiwa Wabunge wote, ambao walipata nafasi ya kuchangia kwa kuzungumza ndani ya Bunge hili na Mbunge mmoja ambaye alichangia kwa maandishi. Wote nawashukuru na kuahidi kwamba, ushauri walio tupu tutauzingatia na ni mategemeo yetu kwamba, itatusaidia katika utekelezaji wa Muswada huu muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwatambue Wabunge waliochangia ndani ya Bunge kwa kuzungumza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mbunge wa Muyuni na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mbunge wa Konde na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mbunge wa Rufiji, Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo, Mbunge wa Kilindi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimshukuru Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya, Mbunge wa Viti Maalum na Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, ambaye alichangia kwa maandishi. Napenda pia niwashukuru Wabunge wote, kwa michango yao ambayo wameitoa.

Michango waliyoitoa naomba niitolee ufanuzi kama ifuatavyo:-

Nitaanza na Msemaji wa Kamati ya Huduma za Jamii, ambaye hoja ilikuwa kwamba, ili kuboresha huduma za afya ya akili nchini, Kamati inashauri Serikali iongeze idadi ya watumishi wanaotoa huduma hizo. Vilevile kuwaongezea watumishi motisha na kuharakisha ujenzi wa kituo cha tiba na utengemeo wa waathirika wa dawa za kulevyia ili tiba yao iweze kutenganishwa na wagonjwa wengine wa akili. (*Makofii*)

Vilevile walishauri kwamba, hali ya usalamu ya wagonjwa iimarishwe, hii ni pamoa na wagonjwa wa akili na wafanyakazi. Aidha, Serikali ifikirie kutoa fidia ya gharama zinazotokana na uharibifu wa mali au madhara yanayosababishwa na mgonjwa wa akili.

Majibu ya Wizara ni kama ifuatavyo: Serikali kupitia Wizara yangu, imeandaa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), utakaotekeliza kwa awamu mbili za miaka mitano mitano. Katika awamu ya kwanza, kipaumbele kimewekwa katika upatikanaji wa watumishi watakaotoa huduma katika vituo vya huduma za afya. Wataalamu hao ni pamoa na wale wa afya ya akili.

Aidha, Wizara imeandaa Mpango Maalum wa kuibadilisha Hospitali ya Mirembe ijikite zaidi katika kutoa mafunzo ya utalaamu wa kuhudumia wagonjwa wa akili na waathirika wa dawa za kulevyta ngazi ya msingi.

Katika kuboresha mambo ya utegemeo, vilevile Kamati ilishauri kwamba, nyumba za wafanyakazi ziangaliwe kwa jicho la huruma. Ningependa kutoa *report* kwamba, pale Itega ambako tunajenga Wodi za Utengamao, yaani *Rehabilitation*, mwaka huu Serikali imetenga shilingi 610 milioni wakati nyumba za watumishi zimetengewa shilingi milioni 100. (*Makofi*)

Serikali inapokea ushauri wa Kamati kuhusu motisha kwa wafanyakazi wanaohudumia wagonjwa wa akili. Tutaendelea kujadiliana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kuhusu pendekezo hili na utekelezaji wake.

Kuhusu usalama wa wafanyakazi hususan pale wanapoumizwa na wagonjwa katika mazingira ya kazi, Wizara inaendelea kupokea ushauri huu na itaendelea kutekeleza kwa kuzingatia masuala ya usalama kwa watoa huduma, pamoja na wagonjwa kwa jumla.

Wakati suala la fidia kwa mfanyakazi aliyeumia katika mazingira ya kazi linasimamiwa na Sheria mpya, ambayo tumeipitisha mwaka huu ya *Workers Compensation Act*, kuhusu fidia za uharibifu wa mali; taratibu za kawaida za Mahakama zitaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ilikuwa Madaktari wanaofanya kazi katika Sekta Binafsi, wahanishwe katika utekelezaji wa Sheria hii kwani mchango wao ni mkubwa katika kuwahudumia wagonjwa wa akili. Tunakubaliana na pendekezo hilo na tayari kwenye jedwali la marekebisho hiyo imo, inataja Madaktari wanaofanya kazi katika Serikali na pia wale walio katika Sekta Binafsi. (*Makofi*)

Kuhusu suala la Wajumbe wa Bodi ya Haki za Wagonjwa, Kamati ilishauri kwamba, kipengele “F” kilichokuwa na Viongozi wa Dini kiondolewe ili kuondoa utata ambao unaweza kujitokeza wakati wa kutekeleza Sheria hii. Aidha, majina yalijotajwa katika kifungu hiki yatenganishwe na yaorodheshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kusema mabadiliko yote hayo yamezingatiwa. Sheria kabla hajajadiliwa, ilikuwa inazungumza Viongozi wa Dini, lakini kwenye Kamati ikaonekana hapa Dini zipo nyingi; siyo Wakristo na Waislam peke yao bali kuna Bahai na watu wengine. Hata kwa Waislam kuna Shia, Sunni na Wakristo Wakatoliki na ilionekana kwamba hii italeta matatizo kwa hiyo kipengele hicho kimefutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya nne ilitueleza kwenye ibara namba 9 kifungu (1) kwamba, Kamati imeshauri Askari Polisi ye yeyote aliye katika Kituo cha Polisi, ahusike katika kuchukua hatua muafaka za haraka za kukabiliana na mahitaji ya mgonjwa wa

akili na kuchukua jukumu la kumfikisha sehemu ya kutolea huduma badala ya kumsubiri mwenye dhamana ya kituo hicho. Tunakubaliana na hilo wazo na katika jedwali letu la marekebisho, hiyo imezingatiwa. Muswada umesema *Police Officer in Charge* na hapa tunakubaliana na wazo kwamba awe Polisi yeyote yule. (*Makofit*)

Kamati inashauri kuwa, baada ya Sheria mpya kupitishwa na Kanuni zake kutayarishwa, hatua za haraka zichukuliwe kutafsiri Sheria na Kanuni hizo kwa Lughya ya Kiswahili ili ziweze kueleweka kwa urahisi. Tunakubaliana na tunapokea ushauri huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye hoja za Kambi ya Upinzani. Suala la kwanza lilikuwa ni la mgonjwa wa akili kujipeleka mwenyewe hospitali, kama ilivyobainishwa katika ibara ya 4(1); je, hii inawezekana?

Mheshimiwa Naibu Spika, jibu ni kwamba, wagonjwa wengi wa akili wanaweza kujitambua kwamba wanahitaji matibabu na hasa pale wanapoju sehemu za kupata huduma hizo. Wagonjwa wanaweza kwenda kuomba huduma wenyewe au kuomba ndugu wawapeleke kutafuta matitabu. Kwa hiyo, hilo ni jambo la kawaida.

Ibara ya 9(1) imemainisha watu mbalimbali ambao wanaweza kuchukua jukumu la kumpeleka mtu yeyote anayehisiwa kwamba ana ugonjwa wa akili ili akapatiwe dawa. Je, watu hawa wana taarifa kuhusu majukumu yao; na je, watapatiwa mafunzo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara yangu, baada ya hii Sheria kupitishwa, utekelezaji wa wake, majukumu na vilevile kuhamasisha jamii iweze kuielewa Sheria hii, vitafanyika. Katika vipengele vingi tu vya Sheria, vinaonyesha jinsi elimu ilivyopewa kipaumbele. Vilevile ushirikishwaji wa wananchi wenyewe. (*Makofit*)

Swali lingine lililoibuliwa na Kambi ya Upinzani ni kwamba, matumizi ya dawa za kulevyta ni kosa la jinai na kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu ina kitengo, pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani, wanashughulikia masuala ya dawa za kulevyta. Je, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuwa na kitengo cha kushughulikia suala hili haitaleta mgongano na pia matumizi mabaya ya rasilimali?

Mheshimiwa Naibu Spika, jibu langu ni kwamba, tatizo hili la dawa za kulevyta ni mtambuka, Wizara yetu inajihuisha na masuala ya elimu ya kinga, tiba na utengemano. Vilevile katika Tume ambayo inaratibu masuala haya, inajumuisha Wajumbe kutoka Wizara nyingi tu ikiwemo Wizara ya Afya, lakini hata *TRA*. Tunalichukulia hili suala kwa ujumla wake, kwa hiyo, mahali sahihi kwa hii Tume kuweza kukaa na kuratibiwa ni Ofisi ya Waziri Mkuu, ambaye ndiye Mratibu Mkuu wa Shughuli za Serikali.

Kwa hiyo, hatuoni kama kutakuwa na migongano au mwingiliano wa majukumu na kwamba, kuna matumizi mabaya ya rasilimali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, alishauri kwamba, Wizara iweke bajeti ya kutosha ili kutoa huduma nzuri kwa wagonjwa wa akili. Vilevile iongezwe idadi ya wataalamu, ikiwa ni pamoja na kuanzisha mitaala ya fani ya afya ya akili katika vyuo vya mafunzo tabibu. Aidha, Wizara ianzishe Kurugenzi ya Afya ya Akili ili isimamie vizuri zaidi huduma za afya ya akili nchini, pia alishauri dawa zipatikane hadi ngazi ya msingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, kwa kutupigia debe kuhusu kuongeza bajeti na tutalifanyia kazi suala hilo.

Kuhusu kuundwa kwa Kurugenzi ya Afya ya Akili pale Wizarani pia tumepokea ushauri, lakini hili suala litategemea muundo mzima wa Wizara na uwezekano wa Serikali kuongeza Kurugenzi zaidi ya zile tulizonazo.

Suala la kuanzia Mtaala wa Mafunzo ya Afya ya Akili katika vyuo vya Tabibu tumelichukua na tayari nitoe *report* tu kwamba, Wizara ilishaandaa mikakati ya kuhakikisha vyuo hivyo vinatoa mafunzo kama hayo.

Kuhusu upatikanaji wa dawa za magonjwa ya akili ngazi ya msingi, hili Serikali kupitia Wizara yangu, inajitahidi kuhakikisha kwamba, dawa muhimu za wagonjwa wa akili zinafika hadi vituo vya huduma vya ngazi ya msingi.

Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, alitilia mkazo suala la kuchukua hatua za kupunguza unyanyapaa ndani ya jamii, pia aliishauri Serikali iongeze bajeti kufikia kiwango cha 15% kulingana na Azimio la Abuja. Vilevile alishauri Serikali itoe kipaumbele katika kuandaa takwimu sahihi za ukubwa wa tatizo la akili. Aidha, alishauri tutoe mafunzo ya watoa huduma za afya ya akili ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuielimisha jamii ili kupambana na tatizo la unyanyapaa. Msukumo mkubwa katika Muswada huu ni unyanyapaa, kuwatenga na kuwadhalilisha hawa wagonjwa.

Aidha, Serikali itaongeza Bajeti ya Serikali kulingana na uwezo wake na labda tuseme tu kwamba, sasa hivi Sekta ya Afya imepewa kipaumbele namba tatu katika Bajeti ya Serikali. Tunavyokwenda mwaka hadi mwaka, tunaona kuna ongezeko kidogo, mwaka jana tulikuwa 10.2% na mwaka huu tuko 11.1%. Kwa hiyo, tunakwenda *in the right direction*.

Tafiti mbalimbali zinaendelea kufanyika hapa nchini ili kubaini ukubwa wa matatizo ya wagonjwa na tutoe rai tu kwa wananchi kwamba, tunapowatafuta hawa wagonjwa wasifichwe, wanafichwa kwa kuona aibu kuwaleta mbele ili tuwatambue. Hata hivyo, Wizara inaendelea kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa takwimu mbalimbali za Sekta ya Afya. Kuhusu utoaji wa mafunzo ya watoa huduma ya afya ya akili katika jamii, Wizara inaendelea kuimarisha mafunzo mikoani kwa awamu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, alisema kwa uchungu kwamba, kundi la wagonjwa wa akili liangaliwe kwa jicho la huruma ili wapate haki zao za msingi, pamoja na kuthaminiwa utu wao. Vilevile alisema wodi za wagonjwa wa akili ziwe na nafasi ya vyumba kwa kila mmoja na suala la ushauri nasaha litiliwe mkazo ili kuondokana na mifarakano katika familia na jamii. Akashauri vilevile kwamba, Semina kuhusu Afya ya Akili zifikishwe hadi vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema Serikali imeyapokea mapendekezo mazuri ya Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya. Aidha, kwa kuwa suala la kuwa na chumba kwa kila mmoja, litazidi kuleta unyanyapaa, ipo hatari ya wagonjwa kuhudumiwa katika hali ya kutengwa na kuwa na usimamizi mdogo wa wataalamu hasa ukizingatia kwamba, watalamu tulionao kwa hivi sasa ni wachache. Ni vyema wagonjwa hawa waendelee kukaa katika wodi ya wazi chini ya uangalizi wa karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, alihoji suala la kuwafuutilia wagonjwa wa akili wanaozunguka mitaani. Pia Serikali ifanye utafiti kujua chanzo cha ongezeko la wagonjwa wa akili na watumishi waongezwe, kwa maana ya kuongeza Bajeti ya Serikali kwa kundi hili na kwamba kila hospitali ya Wilaya iwe na wodi za wagonjwa wa akili.

Kuhusu suala la uhaba wa wafanyakazi, tumeshaligusia hapo awali na ufuutiliaji wa wagonjwa wa akili wanaozunguka mitaani, utatekelezwa kwa mujibu wa Ibara ya 9 ya Muswada, yaani ni moja ya sababu ya kuletwa Muswada mbele ya Bunge hili Tukufu. Mapendekezo mengine yatafanyiwa kazi kama nilivyoeleza hapo awali na suala la wodi za wagonjwa wa akili Wilayani ni suala ambalo tayari lipo katika mwongozo wa Sera ya Afya kuhusu Huduma za Afya ya Akili. (*Makofifi*)

Kuhusu suala la kwamba, kijulikane chanzo cha matatizo haya akatoa mfano wa watoto wadogo ambao wanajifungua wakiwa bado hawajakomaa na kwamba, iletwe Sheria watoto hawa waruhusiwe lini kupata mimba. Nadhani hii itakuwa ngumu kidogo, Sheria tunaweza tukaiweka lakini nadhani kitu muhimu watu waelewe na wawe na maadili, kwa sababu Sheria inaweza ikawepo lakini mambo ya kupata mimba hayahitaji ridhaa ya mtu.

Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum alisema, utafiti ufanyike ili kujua vyanzo vya magonjwa ya akili, kwa nini yanaongezeka. Ametoa mfano wa Mkoa wa Morogoro, ambapo ametuambia amekaa kwa muda mrefu na kwamba, bajeti iongezwe na idadi ya watumishi wanaotoa huduma, pamoja na motisha pia viongezwe.

Tumepokea mapendekezo ya Mheshimiwa Sakaya kwamba, utafiti ufanyike na yeze kwa kauli yake ni kwamba, wengi ambao ameona wanahuksika ni vijana. Sisi tunajua kwamba, vijana wengi wameingia katika mchezo wa kutumia dawa za kulevyaa na hiyo inasababisha wingi wa vijana ambao akili zao sasa zinaharibiwa na hayo magonjwa. (*Makofifi*)

Tunazo takwimu za Hospitali zetu za Isanga na Mirembe, ambapo kwa miaka saba mfululizo utaona idadi ya wagonjwa waathirika wa dawa za kulevywa walivyolazwa. Kwa mfano, mwaka 2000 tulikuwa na wagonjwa 178, mwaka 2001 walikuwa wagonjwa 291, mwaka 2002 wagonjwa 334, mwaka 2003 wagonjwa 386, mwaka 2004 wagonjwa 527, mwaka 2005 wagonjwa 597 na mwaka 2006 wagonjwa 704. Utaona kwamba, idadi inaongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa hiyo ni tatizo ambalo ni lazima kuliwekea mikakati madhubuti.

Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo, alishauri kwamba, tuongeze vituo vya kutolea huduma za afya ya akili hapa nchini na watumishi waongezwe. Vilevile aliuliza kama wanawekewa Bima. Pia alizungumzia suala la motisha kwa wafanyakazi. Mambo mengi nimeyazungumza hapo awali, namshukuru Mama Shellukindo, kwanza, alituambia kuna wakati alileta wagonjwa idadi siikumbuki, kutoka Kilindi kuja kutibiwa hapa. Kwa jinsi alivyo kuwa akizungumza, alikuwa anauliza je, hii Sheria inatekelezeka; mbona tuna wafanyakazi wa kutosha, mbona kuna mtu mwingine anaweza akawa ameamua tu kutozungumza kumbe ni mganjwa; je, mna wataalamu wa namna hiyo?

Tunashukuru kwa mawazo yake na sisi katika Sekta ya Afya tunasema kwamba, ukifanya uzinduzi yaani *diagnosis*, basi ndiyo mwanzo wa kupona kwa mganjwa. Kwa yale aliyoyaorodhesha, sisi tunashukuru na tutayachukua kama changamoto ili tuyapatie majawabu wakati wa utekelezaji.

Mheshimiwa Dr. Lucy Nkyia, alitoa ushauri wa upatikanaji wa dawa na akazitaja kama *modicate*, uanzishaji wa huduma za afya ya akili katika jamii, kuongeza vituo vya utengamao wa afya ya akili kila mkoa na upatikanaji wa dawa za kifafa. Ushauri ni mzuri na sikushangaa kwa sababu yeye mwenyewe ni mtaalamu wa magonjwa ya akili, halafu ni mwanafunzi wangu. Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba, Wizara imepokea ushauri huo na itauzingatia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kuptitia hoja zilizotolewa na ndugu zangu Wabunge, waliopata nafasi ya kuchangia leo asubuhi. Kama nilivyo sema, nawashukuru halafu yote ambayo wametushauri tutayazingatia katika utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono. Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa kifungu cha 56(2) kinasema hivi: “Hoja au marekebisho au mabadiliko ya hoja yoyote yatahitaji kuungwa mkono na Wabunge wasiopungua kumi na endapo haijaungwa mkono, hoja au marekebisho au mabadiliko hayo yatatenguka na Katibu ataweka kumbukumbu kwenye Taarifa Rasmi kwamba, kwa kuwa hoja au marekebisho au mabadiliko haya hayakuungwa mkono, basi hayakujadiliwa.”

Sasa naona hapa kila wakati hoja ikitolewa na Serikali, tulikuwa tunawaangalia Mawaziri, lakini Kanuni haisemi Mawaziri inasema Wabunge. Kwa hiyo, mlichokifanya ni sahihi kabisa, si lazima Mawaziri isipokuwa Wabunge. Kwa hiyo, hoja imeungwa mkono. (*Makofi*)

Katibu kwa shughuli inayofuata.

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili*)

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Afya ya Akili wa Mwaka 2008
(*The Mental Health Bill, 2008*)

Ibara ya 1
Ibara ya 2

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 3
Ibara ya 4

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7
Ibara ya 8

(*Ibara zilizotajwa hapo zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 9
Ibara ya 10

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa, kwa Muswada mrefu, lakini nimeona hizi Wizara ambazo ni *highly technical*, zina vitu vidogo vidogo ambavyo itabidi tuwasaidie tu.

Katika Ibara hii ya 10(5) katika marekebisho imerekebishwa, lakini ya (6) kuna neno pale ambalo limeandikwa *rate of mental disordered* kule kwenye ibara ndogo ya (5)

imebadilishwa na imekuwa *mental disordered*. Kwa hiyo, ningeomba na hapa akubali ile ibara ndogo ya (6), ule mstari wa tatu nao usahihishwe uwe *mental disordered*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri tupo wote?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ibara ya 6 anayoizungumzia, inazungumza habari za *mental disorder*, pale tunamzungumzia mtu na tunam-*describe* kwamba, yupo *mentally disordered*. Kwa hiyo, hivyo ilivyo tunaona imekaa sawa.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni hivyo aondoe ile ‘ed’ iwe *mental disorder* kwa sababu imeandikwa *mental disordered*.

MWENYEKITI: Ni namba 5?

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Ni namba 6, mstari wa tatu; *a mental disordered* kama ulivyosema ni *have a mental disorder*, lakini ukiisoma haikai vizuri.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikubaliane naye.

MWENYEKITI: Kwa hiyo, tuna ile ya mwisho *paragraph* ndogo ya 6, pale chini tuondoe *disorder* tuseme *then*, huwezi kufanya *disordered* bila kuondoa *mentally*. Umeandika nini?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, tuPo mstari wa tatu; *a relative of a mentally disordered person* ndiyo sahihi.

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 11

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu tukubaliane katika ibara ya 11(6) pale inasema; *the court shall* badala ya *where is certified I think should be where it is certified*, ile *it* ikiingia pale itakaa vizuri tu.

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 12

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 13

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 14

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 15

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 16

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 17

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 17(1)(c), ile sentensi inayosema *deliberate and decide on issues of the patients brought in the Board attention, I think should be to the Boards attention* kuliko kuiacha iwe to Boards attention? Nadhani sasa hivi tutakubaliana?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 18

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Ibara ya 18, nilitaka tuone zile *marginal notes* ambazo zinasema; “*operating of the Board*” halafu zinasema “*at any meeting of the Board, half of the total should be Members, its total numbers of Members shall constitute a quorum.*” Nadhani *marginal notes* ingekuwa *quorum of the Board Meeting*, badala ya *operating of the Board*.

MWENYEKITI: Nafikiri ni sahihi.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho kipengele alichokisoma Mheshimiwa Shellukindo ni aya moja tu ya 18, labda ingekuwa *operations of the Board*.

MWENYEKITI: Inasemaje?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Nasema hiyo *marginal note* aliyoizungumzia, inahusu ibara nzima ya 18, ambayo inakuja mpaka ukurasa unaofuata. Kwa hiyo, kweli hiyo *operating of the Board* haileti maana, labda ingekuwa *operations of the Board*. Kusema *quorum* ni 18(1) peke yake.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Nakubaliana naye kwa hilo.

MWENYEKITI: Kwamba, tungenesema *quorum and operation of the Board*?

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Yaani sasa isiwe *operating of the Board* but *operation of the Board* na isiwe ile ya *quorum* ya kwangu.

MWENYEKITI: Halafu hata kifungu cha 17, ukurasa wa 11 tuna *Subsection (1)*; “*The Board shall* (a), (b), (c), (d), lakini hakuna (2). Kwa hiyo, *we could as well remove (1)*.

Je, Mheshimiwa Waziri tupo wote, tumerudi nyuma kidogo?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Samahani sikukupata Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Ukurasa wa 11, ibara ya 17, kuna ibara moja ndogo halafu *the Board shall be* (a), (b), (c), (d), mpaka (h). Sasa mtu angetegemea *there is a continuation of those subsections*, lakini hakuna nyingine.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Tunakubaliana na wewe.

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 19

Ibara ya 20

Ibara ya 21

Ibara ya 22

Ibara ya 23

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 24

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 25
Ibara ya 26

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 27

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebishi yake*)

Ibara ya 28

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 28(3), ile sentensi inayosema *every mental health care facility shall be put in place*, nadhani *shall put in place*. Ile be ingeondoka pale naomba Profesa akubali hii.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri una maelezo?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Nashangaa kwenye *amendment schedule* na sisi tuliiiondoa hiyo, bahati mbaya tu labda haikuwa *captured*. Ninakubaliana naye.

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebishi yake*)

Ibara ya 29

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 30

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebishi yake*)

Ibara ya 31

MHE WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 31(1)(a), ule msitari wa tatu wa hiyo ibara ndogo ya 1(a), kuna neno pale katika sentensi wanasema; “*prevention programmes for substance abuse and advice the Minister.*” Nadhani hii hapo wangeitumia *as advised by the Minister*.

MWENYEKITI: Tuweke *as instead of (c)*. Kama ilivyo ile ya 17(1) pale pia ingetoka. *Subsection (1)* pia ingetoka.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Ndio.

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 32
Ibara ya 33
Ibara ya 34
Ibara ya 35
Ibara ya 36

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 37
Ibara ya 38

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 39
Ibara ya 40
Ibara ya 41
Ibara ya 42

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 43

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Jedwali

(*Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake*)

(*Bunge lilirudia*)

Muswada wa Sheria ya Afya ya Akili wa Mwaka 2008
(*The Mental Health Bill, 2008*)

(*Kusomwa Mara ya Tatu*)

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima, imepitia Muswada wa Sheria uitwao *The Mental Health Act, 2008*, pamoja na mabadiliko yake, kifungu hadi kifungu na kuukubali. Hivyo basi, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada huo sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa*
Mara ya Tatu na Kupitishwa)

HOJA ZA SERIKALI

A Z I M I O

Azimio la Bunge la Kuridhia Upanuzi wa Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara, ilianzishwa mwaka 1960, ikiwa na eneo la kilomita za mraba 330. Hifadhi hii ilianzishwa kwa lengo la kuwezesha kukamilika mzunguko na mahitaji ya wanyamapori waishio katika Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Kulinda bionuwai kubwa ya eneo hilo na kuongeza vivutio kwa watalii wanaotembelea Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na eneo la Ngorongoro. Aidha, Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara ni Hifadhi pekee nchini inayohifadhi mifumo ya ardhi na mazingira ya bonde kuu la ufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kupanuka kwa shughuli za maendeleo ya binadamu hasa kilimo, makazi na utalii, Hifadhi hii imebanwa hadi kutishiwa wanyamapori wake kutoweka. Tishio la kutoweka kwa wanyamapori, linatokana na eneo linaloweza kutumiwa na wanyama kuwa dogo kutosheleza mahitaji yao. Aidha, shughuli hizo zitasababisha kutengwa kwa Hifadhi hii kutoka Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na eneo la Ngorongoro, maeneo ambayo yanategemeana sana kiikolojia. Matokeo ya tafiti zilizofanyika yanaonyesha kwamba, mwenendo huu umesababisha wanyama kama tohe, popfu, duma, kongoni, tandala, nsia na faru kutoweka. Mnyama aliyeanza kutoweka baada ya Hifadhi kuanzishwa ni duma akifuatiwa na kongoni, baadaye nsia na faru katika miaka ya 1980 na baadaye tohe na popfu walitoweka katika miaka ya 1990.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii, kupitia Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (*TANAPA*), mwaka 1971 ilichukua tahadhari ya kukabiliana na tatizo la kutoweka kwa wanyama katika Hifadhi kwa kuweka mikakati ya kutekelezwa kwa awamu. Mikakati hii ilikuwa ni pamoja na kununua mashamba yanayopakana na

Hifadhi; kudumisha mapito ya wanyama hadi Hifadhi ya Taifa ya Tarangire; kudumisha mapito ya Mwambao wa Ziwa Manyara kwa upande wa Mashariki na kudumisha maeneo ya mtawanyiko wa wanyama kwenye ukanda wa juu Magharibi mwa bonde kuu la ufa.

Juhudi za kukwamua Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara kutokana na athari ya udogo wake wa eneo lake ni pamoja na kupata ridhaa ya wananchi wanaozunguka msitu wa asili wa Hifadhi ya Marang ili kujumuisha msitu huo kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara. Pia kupata ridhaa ya wananchi wa vijiji vya Israleri, Losurwa, Kambi ya Simba, Aicho, Moyomayoka, Vilimavitatu na Minjingu ili washiriki katika kudumisha mapitio na maeneo ya mtawanyiko wa wanyama kutoka Hifadhi ya Taifa ya Manyara.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Babati, imewawezesha wananchi wa vijiji vya Sangaiwe, Maghala, Minjingu, Mwada na Vilimavitatu kuanzisha eneo la Yumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (*WMA*), inayoitwa Burunge ili kudumisha mapito ya wanyama yaliyopo kwenye vijiji vyao na kuwawezesha wananchi hao kufaidika moja kwa moja kutokana na matumizi ya wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii inalenga katika kutekeleza Sera ya Taifa ya Wanyamapori, kuhusu kuanzisha na kuboresha mfululizo wa mtandao wa maeneo yaliyohifadhiwa na ardhioevu muhimu ili kulinda bionowai ya Tanzania. Serikali imedhamiria kuboresha uhifadhi endelevu katika Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara, baada ya kudhihirika kuwa eneo la Hifadhi pekee ni dogo kuhakikisha uhifadhi endelevu na kuwa hali hiyo inatishia kutoweka bionuwai katika eneo hili ambalo ni muhimu sana katika utalii wa Kanda ya Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi itapanuliwa kwa kuongeza msitu wa asili wa Marang wenyе ukubwa wa kilomita za mraba 230.6, mashamba namba 1, 2, na 3, majimoto yenye ukubwa wa kilomita za mraba 38, sehemu ya Ziwa Manyara wenyе ukubwa wa kilomita za mraba 42.7 na ufukwe wa Ziwa Manyara wenyе ukubwa wa kilomita za mraba 7.4; hivyo, kupanua Hifadhi ya Ziwa Manyara kutoka kilomita za mraba 330 hadi kufikia kilomita 648.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali halisi ya maeneo yatakayo jumuishwa katika Azimio hili ni kama ifuatavyo:-

(a) Msitu wa Hifadhi wa Marang ultangazwa kuwa msitu wa Hifadhi ya Serikali Kuu kuititia tangazo la Serikali Na. 89 la mwaka 1938, hivyo msitu huu unapandishwa hadhi kuwa sehemu ya Hifadhi ya Ziwa Manyara

(b) Shamba Na. 1 Majimoto lilikuwa linamilikiwa na Bwana Baker ambaye baada ya kushindwa kuliendeleza alilirudisha Serikalini. Mwaka 1974 Serikali ilitoa miliki ya shamba hili kwa Shirika la Hifadhi za TANAPA kuititia Agenda Na. 2/74 ya tarehe 23 Julai, 1974 ya DDC ya Wilaya ya Hanang kwa wakati huo.

(c) Mashamba Namba 2 na 3 Majimoto yalikuwa yanamiliikiwa na Bwana Vasta Sisodya. Mashamba haya yalinunuliwa na Shirika la Hifadhi ya Taifa (*TANAPA*) mwaka 1990 na kupewa hatimiliki na 16426 na 354.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ilivyo hivi sasa ni kwamba, mashamba yote matatu baada ya kukabidhiwa kwa Shirika la Hifadhi za Taifa (*TANAPA*), yamerejea katika uoto wake wa asili wa msitu na hakuna shughuli za wananchi zinazofanyika katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii ilishawahi kuwasilishwa mbele ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1995 na kukataliwa kwa sababu zifuatazo:-

1. Wananchi wa Kijiji cha Moyomayoka walidai kutoshirikishwa katika zoezi la kubadili hadhi Msitu wa Hifadhi ya Marang ambao walidai kuwa sehemu ya msitu huo ni mali ya kijiji.

2. Kwamba mashamba Moja mpaka Tatu Majimoto yaliyonunuliwa na Shirika ni mali ya kijiji na Wanakijiji hawakushirikishwa katika kujadili matumizi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii iliyafanya kazi madai haya ambapo imedhihirika kwamba:-

1. Msitu wa Hifadhi ya Marang ambao kulingana na Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999 ni *reserved land* na haujawahi kubadilisha hadhi yake, hivyo haupo eneo la Kijiji cha Moyomayoka.

2. Ridhaa ya Kijiji cha Moyomayoka na Wilaya ya Babati ilipatikana wakati Shirika la Hifadhi za Taifa lilopatiwa Shamba Na. 1 kutoka Serikalini mwaka 1974 na iliponunua mashamba mawili Na. 2 na 3 kutoka wamiliki mwaka 1990. *TANAPA* ilipata hatimiliki ya mashamba husika mwaka 1990.

3. Kesi iliyofunguliwa na Wananchi wa Kijiji cha Moyomayoka mwaka 2002 ilifutwa na Mahakama tarehe 8 Juni, 2007. Kutokana na hayo, hoja hii inawasilishwa tena mbele ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuiridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara, inachangia ajira kwa wananchi wa vijiji vinavyozunguka Hifadhi. Hoja hii ikiungwa mkono, itapanua shughuli za utalii Kusini Magharibi mwa Hifadhi hivyo, kuwezesha Shirika la Hifadhi za Taifa kufungua lango kuu la kuititia watalii kwa upande wa Kusini mwa Hifadhi. Hatua hii itawezesha watalii kutoka Hifadhi ya Taifa ya Tarangire, kuingia Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara kwa urahisi kwa kuititia lango hilo. Wananchi wa Kusini na Mashariki mwa Hifadhi watafaidika zaidi na utalii hususan kwa kuzingatia kuwa wananchi hao wameanzisha eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori ambapo pia wanaendesha shughuli za utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii vilevile inalenga katika kuboresha huduma kwa watalii kwa kupunguza muda wanaotumia kutoka Hifadhi ya Taifa ya Tarangire

kwenda Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara, ambapo kwa sasa wanazunguka umbali mrefu kwa kupitia lango la hifadhi hii. Lango lingine likishafunguliwa Kusini mwa Hifadhi hii, litapunguza mzunguko huo. Aidha, msitu wa asili wa Hifadhi ya Marang utaboresha makazi na mazingira ya wanyamapor ikiwa ni pamoja na kukarabati ardhioevu na vyanzo vya maji vilivyoathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za Wizara yangu kuokoa Hifadhi ya Ziwa Manyara, kwa kuongeza maeneo niliyoyataja hapo awali, Wizara yangu ilikutana na wadau mbalimbali wakiwemo Kijiji cha Moyomayoka, ambapo suala la mahitaji ya ardhi kwa kijiji hicho yalijadiliwa. Suala la uhaba wa ardhi katika kijiji hicho lilijitokeza ambapo kijiji kiliomba kipatiwe Shamba Na. 3 Majimoto, ambalo linapakana na kijiji chao kwa upande wa Kaskazini kwa ajili ya matumizi ya wakazi wake. Mikutano shirikishi ilifanyika kati ya Wizara na wadau kwa lengo la kupata eneo la kukidhi hitaji la ombi lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri Shirika la Hifadhi la Taifa (*TANAPA*), lilipewa Shamba Namba 3 Maghala, kama urithi kwa ajili ya uhifadhi kutoka kwa mmiliki Marehemu Prince Bernard wa Uhlanzi. Shamba hili lipo Kusini mwa Kijiji cha Mayoka. Shamba hili halipo katika mpango huu wa upanuzi wa Hifadhi ya Manyara na limepakana na kijiji hicho kama nilivyosema kwa upande wa Kusini. Wizara yangu italishughulikia suala la upatikanaji wa eneo hili, kwa ajili ya matumizi ya kijiji yanayoendana na uhifadhi hususan kuwawezesha Kijiji cha Moyomayoka kujiunga na Jumuiya ya Hifadhi ya Burunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia kwa kusema kwamba, naomba Waheshimiwa Wabunge, muunge mkono hoja hii ili kuokoa Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara katika hatari ya kutoweka kabisa, jambo ambalo litaiweka doa nchi yetu katika sura ya Kimataifa. Hii ni kwa sababu ya sifa kubwa tuliyojijengea katika kulinda na kutunza bionuwai. Vilevile kutoweka kwa hifadhi hii kutaathiri mfumo wa ikolojia na utalii kwa mtandao wa Hifadhi za Taifa za Tarangire, Ziwa Manyara na Ngorongoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa kuwasilisha Azimio la Bunge la Kuridhia upanuzi wa Hifadhi ya Ziwa Manyara kama ifuatavyo:-

KWA KUWA Sera ya Wanyamapor inatamka kutenga na kupanua maeneo ya asili ili kukidhi haja mbalimbali za hifadhi na matumizi rasilimali ya wanyamapor;

NA KWA KUWA Hifadhi za Taifa ni maeneo yaliyohifadhiwa kwa hadhi za juu kabisa katika uhifadhi wa maliasili kwa ajili ya manufaa ya jamii ya sasa na urithi wa vizazi vijavyo;

NA KWA KUWA ili kuhakikisha urithi kwa ajili ya vizazi vijavyo uhifadhi endelevu ni muhimu;

NA KWA KUWA namna moja ya kuhakikisha uhifadhi endelevu ni kuwa na maeneo toshelezi kwa mahitaji na Hifadhi ya Wanyamapor;

NA KWA KUWA eneo la Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara limebainika kutokutosheleza haja ya uhifadhi endelevu katika hali ya sasa;

NA KWA KUWA kwa kupanua eneo la hifadhi hiyo kwa kuongeza Msitu Hifadhi wa Marang, mashamba matatu ya Majimoto na sehemu ya Ziwa Manyara kwa pamoja na maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori yanayozunguka Ziwa Manyara yatakidhi haja ya uhifadhi endelevu wa Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara;

NA KWA KUWA kwa mujibu wa kifungu cha 3 na cha 4 cha Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura 282, RE2002 ili maeneo ya msitu wa Hifadhi ya Marang, Mashamba ya Majimoto na sehemu ya Ziwa Manyara yaweze kuwa sehemu ya Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara; hakuna budi Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuridhia;

HIVYO BASI, Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kikao chake cha 13 kilichoketi Dodoma tarehe 6 Novemba, 2008 linaridhia Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara kupanuliwa kutoka kilomita za mraba 330 na kuwa na kilomita za mraba 648.7. Kama inavyoonesha katika ramani na jedwali la maelezo ya mipaka, kwa kuongeza Msitu wa Hifadhi wa Marang wenge ukubwa wa kilomita za mraba 230.6, Mashamba Namba 1, 2, 3 Majimoto yenye ukubwa wa kilomita za mraba 38, sehemu ya Ziwa Manyara yenye ukubwa wa kilomita za mraba 42.7 na ufukwe wa ziwa wenge ukubwa wa kilomita za mraba 7.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MHE. JAMES D. LEMBELI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la 2007 ili niweze kutoa maoni na ushauri kwa niaba ya Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kuhusu Azimio la Upanuzi wa Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi hii ya Ziwa Manyara ilianzishwa mwaka 1960 ikiwa na eneo la kilomita za mraba 330. Hifadhi hii ni pekee hapa nchini, inayohifadhi mifumo ya ardhi na mazingira ya bonde la ufa. Kutokana na kupanuka kwa shughuli za maendeleo hasa kilimo, makazi na utalii, Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara imebanwa hadi kutishiwa wanyama wake kutoweka. Baadhi ya tafiti mbalimbali zilizofanyika kwenye Hifadhi hii zinaonyesha kwamba, wanyama kwa mfano tohe, pofu, duma, kongoni, tandala, nsia na faru wameanza kutoweka. Pia miaka ya hivi karibuni, ndege waitwao erohe au kwa jina linginge *flamingo*, walikufa kwa wingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kupitia Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania, imechukua tahadhari mbalimbali za kukabiliana na tatizo la kutoweka kwa wanyama katika Hifadhi hii kwa kuweka mikakati ifuatayo:-

1. Imenunua mashamba yaliyokuwa yanamilikiwa na ma-settler Kusini mwa Hifadhi;
2. Imedumisha mapito ya wanyama hadi Hifadhi ya Taifa ya Tarangire;
3. Imedumisha mapito ya Mwambao wa Ziwa Manyara kwa upande wa Mashariki; na
4. Imedumisha maeneo ya mtawanyo wa wanyama kwenye ukanda wa juu wa Magharibi wa bonde la ufa kuunganisha Hifadhi ya Ziwa Manyara na Ngorongoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara, inapendekezwa ipanuliwe kwa kuongeza Msitu wa Asili wa Marang wenye ukubwa wa kilomita za mraba 230.6, Mashamba Namba 1, 2, na 3 Majimoto yenye ukubwa wa kilomita za mraba 38, sehemu ya Ziwa Manyara yenye ukubwa wa kilomita za mraba 42.7 na ufukwe wa Ziwa Manyara wenye ukubwa wa kilomita za mraba 7.4; hivyo, kupanua Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara kutoka kilomita za mraba 330 hadi 648.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo awali hoja hii ilishawahi kuwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu, lakini ilishauriwa kuwa, kwa kuwa wanakijiji walikuwa na kesi yao Mahakamani kuhusu maeneo ya Mashamba Namba 1, 2 na 3 Majimoto ni vyema iwepo subira mpaka kesi hiyo iishe. Taarifa tulizonazo ni kuwa, kesi hiyo imekwisha na mashamba husika yote matatu ni mali ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kipindi cha Kamati, Kamati yangu ilifanya ziara kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara na ilikutana na uongozi wa Hifadhi, pamoa na wafanyakazi. Hifadhi hii bado inakabiliwa na matatizo mbalimbali, ikiwemo uchache wa watumishi hasa wa jinsia ya kike. Uchache wa nyumba za kuishi watumishi, migogoro kati ya wananchi na wanyamapori, ujangili, kufungwa kwa mapito ya wanyama, uchomaji wa mkaa na ukosefu wa mipango madhubuti ya matumizi bora ya ardhi. Kamati ilipokea maombi mbalimbali ya wafanyakazi ikiwemo kuongezwa idadi ya watumishi wa kike. Mishahara na magari ya doria; hivyo Kamati inasisitiza Wizara kushughulikia maombi haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inaipongeza Wizara kwa kuweza kuwasilisha Azimio hili, lenye lengo la kuwalinda wanyama wanaotoweka kutohana na shughuli za maendeleo ya binadamu katika Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara. Azimio hili litasaidia kuhakikisha kwamba, jamii ya wanyama mbalimbali inaanza kuongezeka katika Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kutoa elimu kwa wananchi wa maeneo ambayo yanapakana na maeneo ya hifadhi ili kuhakikisha kwamba, wanahifadhi maeneo hayo vizuri kwa mujibu wa Sheria ili kulinda baionuwai zilizopo.

Kamati inasisitiza Wizara iendelea kushirikiana na Halmashauri za Mbulu, Babati Vijijini na Monduli ili kuwawezesha wananchi kuanzisha eneo la Jumiya ya Hifadhi za Wanyamapori (*WMA*), hasa kwenye maeneo ambayo ni mapito ya Wanyama ili kuhakikisha wanafaidika na matumizi endelevu ya Wanyamapori hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara bado inakabiliwa na tatizo la kupungua kwa kina cha maji hasa kutokana na shughuli za kilimo, kuongezeka kwa makazi ya watu na mabadiliko ya tabia nchi. Kuridhiwa kwa Azimio hili kutasaidia kwa kiasi kikubwa, kupunguza tatizo hili hasa kwa upande wa shughuli za kilimo zinazoendelea kwenye maeneo jirani na Hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kipindi cha mvua, maeneo mengi ya Hifadhi yanajaa maji hivyo upatikanaji wa majani ndani ya Hifadhi kwa wanyama unakuwa mgumu. Kuridhiwa kwa Azimio hili, kutasaidia kufungua mapito ya wanyama kwenda kutafuta malisho hasa kwenye maeneo ya msitu wa Marang na Hifadhi ya Tarangile. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwasilisha maoni na ushauri, sasa napenda kuwatambua kwa majina, Wajumbe wa Kamati hii walioshughulikia Maoni na Ushauri wa Azimio hili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Job Y. Ndugai - Mwenyekiti Hassan Rajab Khatib - Makamu Mwenyekiti na Wajumbe ni Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mheshimiwa William V. Lukuvi, Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mheshimiwa Dkt. Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Hadija Saleh Ngozi, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelili, Mheshimiwa Jacob Dalali Shibili, Mheshimiwa Dkt. Guido G. Sigonda, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Aziza S. Ally, Mheshimiwa Lucy T. Mayenga na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Kaimu Katibu wa Bunge, Ndugu Thomas Kashililah, kwa kuiwezesha Kamati kufanya kazi zake bila matatizo na Makatibu wa Kamati Ndugu Michael Kadebe na *marekebishi* Elieka Saanya, kwa kuihudumia kamati vizuri wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Naibu Waziri, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Blandina Nyoni na Watendaji wote wa Wizara, kwa kuandaa na kuboresha Azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio la Upanuzi wa Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara. (*Makofit*)

NAIBU SPIKA: Ahsante kwa kuwasilisha vizuri na kabla ya kuwa Mbunge alikuwa huko huko *TANAPA* kwa hiyo ni mtaalam. Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani. (*Makofi*)

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA – MSEMADI WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kutoa shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu, muumba wa vyote, kwa kunijalia uzima. Pili, nakushukuru wewe kwa kunipa wasaa huu, kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio la Kuridhia Upanuzi wa Hifadhi ya Ziwa Manyara, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kanuni ya 86(6), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii, kutoa pole kwa Kiongozi wetu wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, ambaye amerejea jana kutoka nchini India alipokuwa kwa matibabu. Mwenyezi Mungu, amponye haraka kutohana na *operation* kubwa aliyofanyiwa hivi karibuni, aweze kurejea kwenye majukumu yake ya kawaida mapema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Chama cha Wananchi (*CUF*), Mkoa wa Tabora, natoa salamu za pongezi kwa Viongozi wa *CUF*, Wilaya ya Kilwa, kwa ushindi mkubwa walioupata katika chaguzi ndogo za vitongoji na mitaa katika Wilaya hiyo. Pongezi pia kwa Uongozi wa *CUF* Wilaya ya Tanga Mjini kufuatia chaguzi ndogo za Udiwani zilizomalizika hivi karibuni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi, naomba kutoa pongezi kwa Watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii, wakiongozwa na dada yangu Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, kwa juhudhi wanazozifanya kuendeleza uhifadhi wa rasilimali zetu hapa nchini. Pia nilipongeze sana Shirika la Uhifadhi la Taifa (*TANAPA*), chini ya Mkurugenzi wake Mkuu, Ndugu Gerald Buruge, kwa kazi kubwa sana wanayoifanya ya kuhakikisha uhifadhi endelevu wa wanyamapori katika maeneo yote ya hifadhi za taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetambua maudhui makuu ya Azimio hili, ambayo ni kupanua wigo wa hifadhi ya Ziwa Manyara kwa kuongeza msitu wa hifadhi wa Marang na mashamba Namba Moja mpaka Namba Tatu, ambayo yanapakana na eneo la Hifadhi ili kutosheleza mahitaji ya wanyama ikiwepo kuongeza maeneo ya mazalia ya wanyama na shughuli nytingine za uhifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa Hifadhi ya Ziwa Manyara, ambayo ina baionuwai ya kipekee, isiyopatikana kwenye hifadhi nytingine yoyote na kwa kutambua umuhimu wa hifadhi hapa nchini na faida zake kwa taifa na Wananchi wa Tanzania kwa ujumla, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa ni muhimu sana jamii inayozunguka ishirikishwe kikamilifu kwa uhifadhi endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, rasilimali ya wanyamaporii tuliyojaliwa Watanzania ni utajili wa kujivunia; hivyo ni wajibu wa Serikali, mamlaka zote husika na wananchi kwa ujumla, kutunza hazina hiyo kwa manufaa ya taifa letu. Kutokana na maeneo mbalimbali ya wanyama yakiwemo mapito ya wanyama, maeneo ya wazi, maeneo ya mtawanyiko kuingiliwa na shughuli za kibinadamu ikiwemo kilimo makazi na kadhalika, imesababisha baadhi ya wanyama kupungua sana kutokana na mazalia yao kuharibiwa na wengine kutoweka kabisa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na upanuzi wa Hifadhi hii, Kambi ya Upinzani inataka kuelewa hatua zilizofikiwa na Serikali katika suala linalohusu Kijiji cha Vilima Vitatu, ambacho kilikuwa na familia zaidi ya 70, kuhamishwa kwa nguvu na eneo hilo la hekta zipatazo 4,084 za kijiji kuuzwa kwa mwekezaji wa Kifaransa, ambaye amejenga Hoteli katikati ya mapito ya wanyama, ambayo hupitisha wanyama kutoka na kurudi Tarangire na kwenda Ziwa Manyara. Hili lilifanyika pia bila kuwashirikisha wananchi wa eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi tuliyonayo ni kubwa na ina vivutio vingi karibu kila kona, hivyo hakuna sababu ya msingi ya Serikali kutoa vibali kwa wawekezaji kujenga kwenye mapito ya wanyama au katikati ya vituo vya utalii. Tunatoa rai kwa Serikali kuwa na mpango endelevu, kuhakikisha kuwa vivutio vyetu vinabaki katika hali ya uhalsia wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nawashukuru Wabunge wote kwa kunisikiliza, naomba kwa kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Awali ya yote, niseme tu kwamba, mimi sina tatizo na naunga sana jitihada za kuhifadhi wanyama wetu. Ninaipongeza vilevile Wizara, pamoja na TANAPA, kwa kazi nzuri wanayofanya pamoja na kwamba tuna matatizo makubwa pale ambapo wanyama wao wanapovuka na kuingia kwenye maeneo yetu. Mnyama akiingia kwenye shamba akamtafuna mwananchi huwa hawamjali, lakini mwananchi wetu akiingia kwenye msitu wao inakuwa mgogoro.

Sasa mimi nianzie tu kwa kusema, mapendelekezo yaliyopo mbele yetu sasa hivi ni kweli nimeongea na Mheshimiwa Waziri, nilikuwa na nia ya kuyakataa na iwapo Waziri hatanipa majibu ya kuridhisha, bado nasema kwamba, mimi sikubali kuunga mkono Azimio hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nakataa Azimio hili? Nalikataa kwa sababu katika vijiji vyangu vya Bugeri, Getamopu na Endara ambavyo vyote vinapakana na Msitu wa Marang, bado kuna utata mkubwa sana. Mwaka 1995 mimi nilikuwa mmojawapo wa waliokataa kupitisha Azimio hili, kwa sababu ya utata huo huo. Bahati mbaya tatizo hilo limejirudia, bado wananchi hawajashirikisha na mipaka inayozungumziwa haijakubalika kati ya Wananchi, Wizara na TANAPA.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1995 niliambiwa kuwa, kutakuwa na jitihada za kusaidia wananchi yale maeneo ambayo ni ya kwao watapandiwa miti ambayo itamea haraka ili angalau mahitaji yawe ya kawaida kama kuni, waweze kupata kazi; kazi hiyo haikufanyika. Unapozungumzia kuongezea eneo, maana yake unaingia kwa wananchi. Sasa wakati tunawahitaji wanyama hawa, tunahitaji utalii, lakini tuisahau kwamba haya yote yapo duniani kwa ajili ya kumhudumia binadamu. Hata siku moja, binadamu asije akahatarishwa kwa sababu kuna rasilimali wanyama. Wanyama ni wakumtumikia binadamu na si binadamu kuwatumikia wanyama. Ninatambua kwamba, binadamu ana akili na mnyama hana akili; ni lazima tumhudumie mnyama. Hilo ninalitambua lakini inapofika mahali kwamba, huyu mnyama sasa anakuwa tatizo kwa binadamu, mimi nadhani hapa sasa lazima tupate *balance* ya kutosha. Maeneo ambayo kwenye ramani yanaonekana nimekwishazungumza na Mheshimiwa Waziri, vijiji vyangu nilivyovitaja, kimsingi vinamegwa sehemu kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo linaanzia kwenye ramani ambayo Waziri ameisema na Kamati ameisema pia, ambayo imetolewa katika *GN* ya Mwaka 1938. Mwaka 1960/61 kulitokea mabadiliko ya ramani ambayo bado hatujaletewa na kwa taarifa tulizonazo, watu waliofanya mabadiliko haya kutoka kwenye Idara ya Misitu walifukuzwa kwa sababu walifanya mabadiliko ya ramani bila kuwashirikisha wananchi. Wananchi wanafahamu mabadiliko yaliyofanyika wakasukumwa na bado hadi leo wananchi wangu wanakamatwa kutokana na mabadiliko haya yaliyotokea mwaka wa 1960. Leo ni vigumu mimi kukubali kuidhinisha wananchi wangu waendelee kusukumwa, wakati bado utata uliokuwepo haujaondolewa. Kwa bahati mbaya, juzi wakati Azimio linaletwa, nilipita kwenye eneo hili kwa shughuli nyingine, wananchi karibu wanipige mawe kwamba mimi nimenyamaza wao wanaondolewa. Wananchi sasa wanaanza kuingia kwenye maeneo yao.

Mimi nadhani Mheshimiwa Waziri kama tulivyozungumza, ninaweza nikakubali tu kuongeza iwapo yale maeneo miliyoyasema, yataondolewa kwenye ramani hii, upimaji utafanyika upya, tukakubaliana maeneo ya wananchi hayataguswa na wananchi waendelee kuishi kama walivyoendelea kuishi kwa zaidi ya miaka 60 katika Vijiji vya Bugeri, Getamog na Endara. Ikiwa hivyo sivyo, basi mimi sitaunga mkono hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba, tunahitaji katika hali ya kawaida, kuongeza maeneo kwa ajili ya maeneo ya wanyama wetu. Tunahitaji kuhakikisha kwamba, mapito ya wanyama nayo yanalindwa, lakini kwa bahati mbaya Serikali nayo kwa miaka yote iliachia haya mapito. Miaka zaidi ya 60 wananchi wamejenga kwenye mapito na maeneo mengi katika Jimbo langu sehemu kubwa limeathirika. Kule Mbulumbulu, Lostitete, Kijiji cha Kambi ya Simba, Chemchemi; mapito haya yalijengwa zamani, wakati yanajengewa hakuna mtu aliyekuwa anauliza. Leo wananchi wameshakaa pale wamezaliana, wanawajukuu wapo hapo, leo ukiniambia haya yalikuwa mapito hakuna anayekuelewa tena kwa sababu jukumu la kwanza la kulinda na kuyahifadhi hayo mapito lilikuwa la Serikali.

Wale walioingia kwa sababu hawakujuua kama walinzi hawakuweza kuwaelekeza cha kufanya, leo huwezi kuwaambia wananchi ondokeni; wanakwenda wapi? Kwa hiyo, nadhani tunahitaji sasa kufanya utamaduni mpya na labda ni kazi ya *TANAPA* kuwafundisha wananchi; mbona kule Ngorongoro wananchi wanaishi na wale wanyama hawagombani, hawawaui, nina hakika hata makabila mengine yanaweza kufanya hivyo. Tatizo ni kwamba, wanyama sasa wakiingia kwenye maeneo yetu, sisi ni wafugaji lakini ni wakulima, wanakula mazao. Sasa tunafanya nini; hii ni kazi ambayo Wizara lazima iangalie ifanye nini. Tukiendelea kusema tunasogea tu kwa wananchi, tutamaliza maeneo. Wananchi wa Karatu hawana ardhi na unapogusa hata mita moja ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiingia kwenye Ofisi ya Mbunge wa Karatu, katika kesi kumi kila asubuhi, watu tisa wana matatizo ya ardhi. Unapowasogeza leo kwa sababu unawapa wanyama nafasi, maana yake unataka kuniongezea kesi zaidi na sijui nitazikibili namna gani. Unapotengeneza tatizo, unatengeneza *instability* katika eneo, unatengeneza wananchi wasiwe na amani, wananchi wasiwe na utulivu na wala wasijue wanafanya nini. Hii ina maana kwamba, wananchi wanakuwa siyo marafiki tena wa rasilimali za taifa na mimi nadhani nia yetu si kuwafanya wananchi kuwa maadui au wananchi wasiwe sehemu ya kuhujumu hata misitu, wasiwe sehemu ya kuhujumu wanyama; wananchi wawapende wanyama, wapende rasilimali zilizopo na iwapo tu kama wao wataona wananaufaika na rasilimali hizi za taifa. Sasa hii itawezekana kama kuna uhusiano mwema. Napenda Waziri achukue jitihada za ziada na anihakikishie hapa atafanya nini kujenga uhusiano kati ya *TANAPA* na wananchi wa vijiji vinavyohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano; miaka miwili tu iliyopita, watu wa *TANAPA* waliingia Kijiji cha Bugeri kuwafuata wananchi majumbani, kuangalia kama una stuli hata kama imetengenezwa miaka minne iliyopita, wanasema wewe ulipata wapi hii miti iliyotengenezea stuli umetoa kwenye msitu wetu. Wanakamata watu, wanapiga faini, hakuna utaratibu unaotumika, uadui unajengeka. Ningependa Waziri anisaidie hili litakomeshwa vipi?

Askari hawa wanaingia mpaka kwenye nyumba za watu na kufanya hata kazi ambazo si zao; wanaendelea kuangalia hata kama wamepika pombe za kienyeji, kama wamepika gongo na mimi nasema sikubaliani na gongo lakini sikubaliani na mtu ambaye si madaraka yake, kwenda kukamata gongo kwa sababu tu na yeche anatafuta namna ya kupata rushwa. Waziri utusaidie anafanyaaje? Usipofanya lolote, haya yote unayotaka kuyaleta, yataleta mgongano mkubwa.

Wapo wanyama ambao unataka wastawi, ustawi wao utakuwa na tatizo kubwa sana. Kwa kipindi cha zaidi ya miaka miwili, wananchi hao walikuwa na uadui mkubwa kiasi kwamba, gari la *TANAPA* halikutakiwa kwenye eneo hilo.

Sasa kama uhusiano huu haujarudishwa na kesi ya mtu wao aliyeuawa mpaka leo hatujui iko wapi, sina hakika kama Waziri ana habari na kesi ya mtu aliyeua. Sasa inapofika mwanadamu anauawa baadae akasahauliwa kama kuku na hakuna anayefuatilia na kesi ile haisukumwi na Serikali, nadhani kuna tatizo la msingi. Ujirani huu ambao

unatengenezwa na ramani hii ni lazima uimarishwe, panapotokea matatizo kuwa na mawasiliano ya karibu, kuwe na udugu unaojengeka kati ya wananchi wetu na hivi vyombo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kuongea zaidi, ninapenda Waziri anihakikishie kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Karatu haikushirikishwa, ni kweli kuna Azimio la Mwaka 1974 la iliyokuwa wakati ule Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, lakini Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu haikupita kwa wananchi. Mnakumbuka mwaka 1974, aina ya Halmashauri zilizokuwepo sio zile ambazo ziliwu zinaanzia kutoka chini. Kwa hiyo, hapakuwa na *process* ya *consultation*, ambazo zinaanzia kutoka vijiji, wananchi bado wanalamika na hata leo hawajashirikishwa. Wananchi wenyewe katika vijiji hawajashirikishwa. Napenda kujua ni kitu gani kitafanyika na namna gani imani ya wananchi itajengwa hata litakapopitishwa hili Azimio ni namna gani haki zao za msingi zitalindwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru ni imani yangu kwamba, Waziri atanipa majibu ya kuridhisha, vinginevyo sitakuwa tayari kuunga mkono Azimio.

NAIBU SPIKA: Isipokuwa na wewe mwenyewe usahihishe, unasema wanyama wa Waziri au wanyama wetu?

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, nasema wanyama wa Waziri kwa sababu wanapoingia kwetu, tukilalamika hatusikilizwi lakini sisi tukiingia kule kwao tunabanwa. Hii ni namna ya kuisema nashukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Wanyama wetu bwana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Mgana Msindai na yeye alikuwa Afisa Wanyamaporu kabla hajatoka huko.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Azimio hili. Kwa kweli hujakosea, wakati haya mambo hajaendelea, mimi nilikuwa Bwana Nyama wa Wilaya ya Mbulu wakati ule ilikuwa haijagawanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri na timu yake ya *TANAPA* na Idara ya Wanyamaporu, kuamka na kuanza kuyarudisha maeneo ambayo yalishapotea. Upande wa wanyamaporu, wameanzisha *Wildlife Management Area*, ambayo inaunganisha Tarangare na *Manyara National Parks*. *TANAPA* nao sasa hivi wameona umuhimu wa kuongeza hifadhi hii muhimu ambayo inajulikana duniani kote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze sana Wananchi wa Mbulu na Karatu, ambao wamekuwa kwa miaka yote wanafaidi Msitu wa Marang, kwa kupata chemchemi za maji na mambo mengine yanayowahusu; nawapongeza sana wao na Wabunge wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nianze kwa kusema kuna hoja ambayo imetolewa hapa na wenzangu walitangulia. Msemaji wa Kambi ya Upinzani,

amezungumzia juu ya Vilima Vitatu na Hotel iliyojengwa na wananchi waliohamishwa. Hiyo namwomba Waziri waende kuangalia, kwa sababu sasa hivi hali inavyokwenda pale ni nzuri sana; Msitu umerudi, wanyama wamerudi na mimi bahati nzuri nilikaa na wale wananchi vizuri. Nimesimama pale mara nyingi na kuongea nao, kwa kweli nao wanaridhika. Kama wapo wachache ambao hawaridhiki, basi Waziri aende yeye na timu yake wakaangalie. Kama kuna tatizo la Hoteli iliyojengwa pale, ile haisumbui wanyama, ila kama kuna tatizo la uhusiano kati ya wananchi na wenye Hoteli, waende kurekebisha ili waendelee kuishi nao vizuri.

Mheshimiwa Dr. Slaa, amezungumzia Guberi, mimi nakufahamu sana na wananchi wanaishi pale wamekuwa wanaishi na ule msitu kwa miaka mingi. Kuna tatizo la wanyama kupanda miti, waende mara moja na uanzishwe mradi pale. Wajenge uhusiano na wananchi ili wawasaidie nao waone matunda ya kuwalinda hao wanyamapor wa Manyara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mimi nikiwa huko, mashamba yote haya matatu yalikuwa yanamiliwi na wenye mashamba. Kwa makubaliano na mapatano, ikakubalika. Naipongeza Serikali kwa sababu mwanzo Azimio lililokuja hapa lilikataliwa na Serikali ikakubali kwenda kukaa na hawa watu wakakubaliana. Wale ambao hawakukubali, walikwenda Mahakamani na Mahakama ndiyo chombo pekee kinachopima uzito wa hoja za pande mbili; bahati nzuri Mahakama ilifuta kesi hiyo.

Kwa hiyo, eneo linalotakiwa kuongezwa halina mgogoro kabisa na mimi mwezi mmoja uliopita nilikuwa Manyara, kwa kuwa mimi Bwana Nyama, ninasikitika sana kwa sababu hiyo hifadhi inakwisha. Hifadhi ambayo kwa miaka mingi imekuwa inaliingizia taifa hili fedha za kigeni na ukienda hata kule Ulaya, wanajua kabisa kwamba, wanakwenda *Manyara National Park* kuangalia misitu iliyopo, wanyama na ndege waliopo wakiwemo Simba wanaopanda miti. Kwa hiyo, ninaomba sana, sisi kama wawakilishi wa wananchi, linapotokea jambo zuri kama hili tuliunge mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka yote mitano niliyokaa Mbulu, sikuwahi kugombana na watu wa Vijiji vya Daudi, Kilima Moja, Gihandu na vijiji vyote vya Karatu. Kwa kweli wameutunza huu msitu wa aina yake, una chemchemi maeneo mengi na toka nafikiri mwaka 1992, *TANAPA* imejenga kambi zake. Kwa hiyo, naomba sana, tunapitisha huu msitu kwa faida ya nchi yetu na sasa hivi, Tarangire na Manyara imeshaunganishwa, wameshirikiana na *TANAPA* na Idara ya Wanyamapor. Sasa Mheshimiwa Waziri, kazi uliyonayo ni kutoka Manyara kuitia Msitu wa Marang, ufungue *corridor* ambayo Mheshimiwa Dr. Slaa amesema, tulizembea kwa muda mrefu wananchi wakajenga ndani. *Corridor* ya kutoka *Marang Forest* kwenda Bonde la Yaida chini na hatimaye *corridor* ya kutoka Yaida chini kupita Mang'ora kwenda Ngororo zifunguliwe. Hapo tutakuwa tumeunganisha hifadhi zetu kubwa na zinazojulikana sana duniani, kwa kuwaruhusu wanyama waendelee kupita. Tunapofungua hizi *corridor*, tusitumie ubabe maana sisi ndiyo tulio kosea. Tukae na Serikali za Vijiji na Halmshauri za

Wilaya tuongee nao, kama ni kuwatafutia maeneo tuwatafutie, kama ni kuwalipa fidia tuwalipe fidia nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu wananchi wa maeneo yote hayo, ukienda kwenye *Open Area* kuna Wambugwe, Wabarbeig na makabila mengine ya wahamiaji. Sasa hivi wanafurahia sana. Pale mwanzo lile eneo lilishakuwa jangwa. Sasa hivi eneo la Mdori, msitu umerudi vizuri sana. Ukija Shamba Namba 1, 2 na 3, misitu imekuja mizuri sana na wanyama wanaopatikana mle wanajisikia wapo nyumbani na haya mashamba yapo karibu na maji moto ambayo wageni wengi hupenda kwenda kuangalia kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, kufungua njia ya Kusini, itawasaidia sana siyo watalii kutoka *Tarangire National Park* pekee, itawasaidia Wananchi wa Mkoa wa Manyara kutoka Babati, Mbulu na hata kutoka kwangu maana tunapakana nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ule usumbufu waliokuwa nao kutoka Tarangire au kutoka Babati mpaka wazunguke Mto wa Mbu utakwisha. Kwa hiyo, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tuiunge mkono hoja hii, kwa faida yetu sisi tulipo sasa na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. (*Makofi*)

MHE. DAMAS P. NAKEI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa fursa hii ya kuchangia Azimio la Bunge, ambalo lipo mbele yetu liliowasilishwa hivi punde na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Nipende tu kuanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri na vilevile nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati iliyochambua Azimio hili. Nawapongeza *TANAPA* kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Jimbo langu la Babati Vijijini. Hawa tunafanya nao kazi vizuri na pale Magara wanatujengea Hosteli ya Sekondari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mbele yetu kuna Azimio la Bunge, ambalo tunaambiwa na Waziri mwenyewe kwamba, liliwahi kukataliwa na Bunge hili miaka iliyopita, kutokana na sababu ambazo alizieleza katika ukurasa wa tatu kwamba, kubwa zaidi ni kutowashirikisha wananchi na wananchi ni wadau muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunaamini uhifadhi wa wanyamapor kwa sababu ni urithi wa Taifa letu. Kwa hiyo, nitashangaa tunapajaribu kuli-*modify* Azimio kama hili, labda hatuelewi umuhimu huo. Tunaelewa kabisa umuhimu wa wanyamapor katica nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, historia ya Azimio hili au eneo hili la Vijiji vya Moya Mayoka (wanaita Moya Mayoka), ni ndefu kidogo; tangu 1999 wakati wadau mbalimbali walipokaa pale *Arusha International Conference Centre (AICC)*, wakizozana juu ya maeneo ya mashamba ambayo sasa hivi yanazungmzwa. Kuna mashamba wanaita, Namba 1, Namba 2 na Namba 3, ambayo yalisababisha mvutano mkubwa kati ya

TANAPA na wanavijiji. Wanavijiji wakiamini Shamba Namba 1, walipewa na Serikali ya wakati ule. *RDD* wa Mkoa wa Arusha wakati ule aliwaambia wahamie katika eneo hilo, ikiwa ni pamoja na Shamba Namba 4. Mpaka sasa hivi wananchi wanaishi kwenye Shamba Namba 4, ikiwa ni kijiji hicho cha Mayoka. Shamba Namba 1 ilibidi watoke pale kwa sababu walikuwa wanapakana na wanyama na wanyama walikuwa wanasumbua kweli kweli, kwa hiyo ilibidi watoke wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho, *TANAPA* walinunua Shamba Namba 2 na Namba 3 na walipofanya hivyo, sasa mashamba yote hayo matatu yanakuwa ndani ya eneo la Kijiji cha Moya Mayoka, kijiji ambacho kilisajiliwa kwa mujibu wa taratibu zote za usajili na kuwa kijiji halali kabisa kisheria. Kwa hiyo, wanakijiji wale wanafahamu kabisa kwamba, maeneo yote hayo yanayotajwa yapo ndani ya mipaka. Kwa hiyo, wanakijiji wanashangaa wanapoona shughuli fulani zinafanyika ndani humo, bila kuwashirikisha wao, kwa sababu wao ni mionganoni mwa wadau. Kitendo cha kuwaweka pembeni kana kwamba hawatusiki, hicho ndicho kinachowaura na ndicho kilichofanya mwaka wa 1999 walipokaa pale Arusha, wakubaliane kabisa kwamba, mara baada ya mkutano huo, Uongozi wa *TANAPA* wakae na Halmashauri ya Wilaya ya Babati. Hawakukaa mpaka mwaka 2002 ndipo walipofungua kesi.

Kwa hiyo, kesi ile ikaendelea kukaa mahakamani mpaka ilipokosa nguvu, kwa sababu sheria zilikuja kubadilika kwamba matatizo yote ya ardhi yanatatuliwa kwenye Mabaraza ya Ardhi. Kwa hiyo, *automatically* kesi hiyo ilikuwa ifutwe, siyo kwamba haikuwa na hoja, kwa sababu haikuwa mahali pake tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia sababu zile ambazo kama alivyoeleza Waziri, zilifanya hoja hii ikwame mwaka 1995, ukurasa wa tatu pale chini, kuna *bullets* zile mbili na ukaangalia majibu yake ukurasa wa nne, huwezi kuona kwamba ni majibu yake. *Scientifically, just look at it.* Kwa hiyo, tunachosema sisi ni kwamba, yote haya ambayo yanaelezwa kwamba yalifanyiwa kazi wakati ule, yalitakiwa yarejeshwe kwenye meza ile ya mazungumzo, iliyokaa mwaka 1999 pale AICC. *Feedback* ilikuwa muhimu sana. Sasa ninyi au niseme Serikali; imefanya nini? Imefanya maamuzi yake yenyewe, bila kuihusisha ile sehemu ya pili ya mazungumzo. Hili ndio tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo hii mimi nazungumza na viongozi wa eneo husika, wanasisitiza kwamba, Shamba Namba 1 bado ni lao. Kwa hiyo, wanachoomba leo ni kwamba, kuliko kuchukua mashamba yote hayo matatu, basi wao ni *ku-swap* Shamba Namba 1 ambalo wanaamini bado wanalo, ingawa tunafahamu kwamba, *TANAPA* walichukua mashamba yote matatu na kupata Hati Miliki bila kukihusisha kijiji kinachohusika. Mimi nadhani Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999, inatutaka tuzishirikishe Serikali za Vijiji, lakini hatukufanya hivyo. Kwa hiyo, mimi nafikiri huo ndio upungufu, ambao Serikali lazima ikiri kwamba upo. Ningefurahi kama Mheshimiwa Waziri atajaribu kuliona hili na kulifanya kazi au kulirekebisha ili wananchi wale waweze kuona kwamba, wao pia ni *part and parcel* au ni sehemu pia ya uhifadhi wa rasilimali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo au hii *conflict* ambayo najaribu kuielezea ndiyo inayofanya wananchi wa Mayoka walalamike kwamba, wameachwa pembedi. *DC* wangu amenipigia simu, hafahamu jambo hili, Mkurugenzi Mtendaji, hafahamu jambo hili, wote hawa ni wadau katika utekelezaji wa zoezi zima la uhifadhi wa wanyama pale. Kwa hiyo, nilidhani ni vizuri Serikali ikaona kwamba, jambo hili lazima lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa mwisho, Waziri anazungumza kwamba, kuna shamba ambalo anafikiria kuwapatia wanakijiji, ambalo sasa hivi nadhani linamiliwi na mtu mwingine. Amesema anaweza akawapatia wanakijiji wa Kijiji cha Moya Mayoka ili liwasaidie katika matumizi yanayofanana au tuseme ya *WMA* kwa mfano. Kwa hiyo, namwomba Waziri athibitishe hilo ili kuonyesha kwamba, yupo pamoja na wananchi wale kwa kutambua kwamba, walikosea kwa kutowashirikisha na ingekuwa vizuri kabisa tuthibitishiwe hapa, najua hili Azimio litapita au vinginevyo, lakini Kamati husika, Serikali kwa ujumla wake na *TANAPA*, waonane na wananchi wa maeneo husika, kwa maana ya Kijiji cha Moya Mayoka ili wananchi waweze kujiona kwamba *they have been taken on board*, ni sehemu pia ya uhifadhi wa wanyamapori na kupanua Hifadhi ya Lake Manyara. Vinginevyo, tutakosa ushirikiano ambao unatakiwa uwepo kati ya *TANAPA* na wanakijiji, kama ambavyo kwa muda mrefu sasa hivi tumekuwa tukishirikiana. Jambo dogo kama hili la utambuzi linapoleta madhara, nina uhakika kabisa kwamba, suala la kukosa amani linaweza likazaliwa na mazingira kama haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kukubali kwangu hoja hii ni katika kufafanua jambo hili na msisitizo katika ile ahadi ambayo Waziri ameitamka humu ndani katika hotuba yake ili tufikie uamuzi huu kwa pamoja, kila mmoja akiwa ameridhika kama mdau katika zoezi zima. Baada ya kusema hayo, nasubiri majibu mazuri ya Waziri, sambamba na hayo, hoja inaweza ikapita kwa kuungwa mkono na Mbunge wa Babati Vijijini. Ahsante sana.

MHE. ALOYCE B. KIMARO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi, nami nichangie hii hoja ya Kuridhia Azimio la Bunge la Upanuzi wa Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme wazi kwamba, mimi ni mdau wa Utalii na ninaunga mkono vizuri sana upanuzi wa eneo hili la Ziwa Manyara, ili kuweza kuhifadhi wanyama ambao wanahama au kufa ili vizazi vyetu viweze kufaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili la vijiji vitatu vya Moya Mayoka, Mdori, Magara, nalifahamu sana. Sidhani kama wananchi wana mgogoro mkubwa kiasi hicho, kwa sababu haya mashamba; Namba 1, Namba 2 na Namba 3, yote sasa hivi ni msitu mnene sana. Msitu wa Marang ni mnene na una chemchemi nzuri sana za maji moto. Kwa hiyo, wananchi wa maeneo hayo, hawana mgogoro mkubwa kama tunavyozungumza hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitashukuru sana, kama Mheshimiwa Waziri atanishirikisha na mimi niende huko tukaongee na wale wananchi mambo ya uhifadhi.

Sasa hivi Tanzania imetenga maeneo makubwa na mazuri kwa ajili ya uhifadhi. *Percent* 25 ya eneo la Tanzania ni eneo la uhifadhi. Vilevile ni vizuri tukatumia maeneo hayo vizur, kwa ajili ya faida ya wananchi na faida ya vizazi vijavyo. Pia ni vizuri kuwashirikisha wananchi, tukae nao, waelewe faida ya uhifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji hiki cha Moya Mayoka, kama Waziri atatimiza ahadi yake ya kuwapa shamba ambalo alilitoa Prince Bernard kwa ajili ya uhifadhi; Serikali inasema inaweza kulitoa hilo eneo kuwapa hawa wanavijiji wa Moya Mayoka na Magara. Ni bahati iliyoje wananchi hawa wanapata shamba; kwanza siyo shamba bado ni msitu, lakini ni shamba la uhifadhi. Kwa kuwa Tarangire inaungana na Manyara na njia mpya itafunguliwa, unaweza kuingia Manyara sasa kwa kutokea Kusini na watalii kutoka Tarangire, wanaweza sasa kwenda moja kwa moja Manyara, badala ya kuzunguka kurudi Mto wa Mbu.

Hawa wanavijiji kama watapata shamba hilo, wakalitumia kwa uhifadhi, wanaweza kuvutia wawekezaji ambao watajenga hoteli na watafaidika. Isipokuwa natoa angalizo kwamba, Wizara ihakikishe kwamba, wanaokuja kuwekeza maeneo haya, angalau *percent* 40 ya uwekezaji wa maeneo hayo iwe ni kwa ajili ya wazawa. Pasiwepo na mgeni ambaye atachukua maeneo huko *100 percent*. Lazima tushirikiane na wazawa, kwa sababu sasa hivi wapo wazawa wengi kabisa wenye uwezo, wanahitaji kushirikishwa na kuelezwaa kwamba maeneo hayo yapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi badala ya kuendelea kulumbana hapa kuhusu hilo eneo, Msitu wa Marang ni Msitu wa Serikali, Shamba Namba 1, Namba 2 na Namba 3 ni mali ya Serikali, kwa maana ya TANAPA na ni misitu sasa hivi. Mimi niwaombe wananchi wa eneo hilo, wakubali kupokea hilo shamba alilotoa Prince Bernard, pamoja na kwamba, nasikia kuna mtu aliyepewa ambaye ni kama amepata hati bandia. Niombe Wizara ya Ardhi nayo, itoe tamko kuhusu shamba hilo ili mgogoro huo uishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niongelee vilevile kuhusu wananchi, ambao wanaishi maeneo hayo ambayo yana wanyama. Kwa mfano, ndugu zetu Wahadzabe wao chakula chao ni mizizi, nyama na asali. Wahadzabe wapo Yaeda Chini mpaka Jimbo la Iramba Mashariki. Leo hii tuna sheria ambazo zinasema kwamba, kama ukitaka mnyamapori, lazima ukalipie na upate kibali. Maeneo haya ya Wahadzabe ni maeneo yao ya asili. Hawa Wahadzabe wanafahamiana wenyewe kwa wenyewe tu, hawafanyi biashara, hawaendi mjini, wanakaa huko kwenye misitu yao.

Nataka ufanuzi kutoka kwa Waziri; hawa wanapowinda wanyamapori kwa ajili ya chakula chao, wanahitaji kupata kibali kutoka kwa nani ili ielevi kwa sababu na wao wana haki? Hawana pesa kwa sababu hawafanyi biashara wala hawawasiliani na watu wengine wowote, isipokuwa wanawasiliana wao kwa wao. Kwa hiyo, tunataka nao haki zao zilindwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifungua hiyo *corridor* kutoka Manyara inaingia Mbulu, inazunguka inakwenda Karatu kule Mang'ora wanakolima vitunguu, *then* wanyama wanaweza wakapita sasa vizuri kutoka Manyara, eneo ambalo linachukuliwa,

wanakwenda Mbulu, wanazunguka wanakwenda Mang'ora huko, wanazunguka wanakwenda Ngorongoro, wanakwenda Serengeti, wanatalii wanakwenda mpaka Masai Mara, halafu baadaye wanarudi. Hiyo ndiyo tunaita *migration*. Sasa tutakuwa tumefungua *migration* kutoka Masai Mara mpaka Tarangire.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jukumu la Serikali kuwaeleza wananchi hali halisi na kama kuna maeneo ambayo walishajenga ama walishaishi kwa muda mrefu, Serikali inao uwezo wa kuwafidia vizuri na kuwapa maeneo mengine ili maeneo hayo yatumike kwa uhifadhi. Jambo hilo si geni na vilevile tukubali kwamba, tulisema hapa Bungeni kwamba, ili tuweze kulinda hifadhi zetu na maeneo ambayo yanakuwa *enclosed* na wananchi, lazima tuchukue hatua nyingine ambazo zitakuwa ni ngumu na zitauma, ndiyo maana hata wananchi waliokuwa kule Ihefu tuliwahamisha. Utaratibu huo unaendelea kuwahamisha hata wananchi wanaoishi milimani. Ukiangalia sasa hivi Ziwa Manyara, linajaa udongo kwa sababu wananchi wamelima kule yanakotoka maji. Kwa hiyo, mvua zinaponyesha zinahamisha udongo, zinakuja kujaza Ziwa Manyara, kwa hiyo maji yanajaa, yanasambaa, badala ya kutulia, yanasambaa maeneo ambayo yalikuwa siyo ya Ziwa wakati huo. Wanyama kama Pofu na Kongoni, hawakai kwenye maji ndiyo maana wametoweka kule Lake Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naunga mkono Azimio hili na naunga mkono vilevile kwamba, Timu iende, iongee na hawa wananchi. Najua ni wananchi amba ni wahifadhi vile vile, kwa sababu pesa wanazopata nyingi zinatokana na kushirikiana na watalii na hata wengine wana makampuni ya utalii. Ukienda kule Mdori, utakuta watoto wa wenyeji waongoza watalii. Ukienda mpaka Burunge, wameanzisha *Wildlife Management Area*, utakuta kuna *Wildlife Management Area* nyingine ambayo inaitwa Juhudi. Kwa hiyo, zote hizo ni juhudzi za wananchi, kwa kuelewa kwamba na wao wanapaswa kushiriki katika uhifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati mimi nilikuwa nakwenda Kihansi, ukienda Kihansi unapita Milima ya Udzungwa; kuna maeneo ambayo wananchi wanaishi, amba walishaelezwa ni nini maana ya uhifadhi. Wakati huo tulipokuwa tunapita, mvua zikanyesha nyingi sana, kwa hiyo, njia ikajifunga kwa sababu miti ilianguka. Tuliporudi nyuma, tukakuta mto amba tulishauvuka, ulikuwa hauna maji nao umejaa, kwa hiyo, tukawa *stranded* katikati pale.

Tukarudi pale ambapo miti ilianguka, tukawaomba wanakijiji watusaidie kukata ile miti ili tuweze kupita. Nilikuwa wakati huo na Mheshimiwa Qaresi, wananchi wakasema huku kwetu kukata miti ni marufuku. Kwa hiyo, hatuwezi kuukata mti huu mpaka uende kwa Mwenyekiti wa Kijiji akubali tuje tuukate, tuuhamishe. Ilibidi twende kwa Mwenyekiti wa Kijiji kutoa taarifa ule mti ukakatwa na sisi tukaweza kupita. Sasa huo ndio ushirikishwaji wa wananchi, mpaka waelewe. Sidhani kama Watanzania sasa hivi hawana uwezo wa kuelewa nini maana ya uhifadhi na nikihifadhi nitapata nini na Serikali itapata nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maneno hayo machache, naomba kuunga mkono hoja na naomba wale amba wanaona kwamba, hii hoja inawakwaza, wasiwe na

wasiwasi, Timu itakwenda itazungumza na wananchi na naamini wananchi wa sasa hivi ni wahifadhi na mambo yatakwenda sawa sawa. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. OMAR S. KWAANGW': Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nitumie nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye Azimio hili la kupanua Hifadhi ya Ziwa Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, niseme kwa dhamira yangu siungi mkono kabisa hoja hii. Lazima niseme wazi, mimi ni mtu ambaye napenda kusema wazi. Kwa dhamira yangu, siungi mkono na si kwa sababu sipendi uhifadhi endelevu, hapana ni kwa sababu ya njia zinazotumika kuchukua ardhi na kuleta migogoro kwa wananchi, hiyo ndiyo sababu yangu. Kwa hiyo, nitaunga mkono siku mambo hayo yote yatakapokuwa yamekamilika. Kwa hiyo, kwa sasa nataka kusema kwamba, kwa dhamira yangu kabisa siungi mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu mimi nimekuwa Mbunge kwa miaka kumi kwenye eneo hilo, matatizo ambayo yalitokea kule ninayajua vizuri sana. Sina tatizo na watu hapa ambao wanapigia debe shughuli zao na nini, wala sina tatizo na aliyekuwa mtumishi katika maeneo ya hifadhi au na nini, kwa sababu ni lazima wangesema hivyo tu, lazima wangeunga mkono. Kwa sababu walikuwa watumishi au mtu anapigia debe mambo yake, wala hatuna matatizo, sina shida na maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niseme kwamba, karibu asilimia 30 ya Hifadhi za Taifa, pamoja na Mbuga na wanyamapori na nini, kwa kweli ndiyo maeneo yaliyotengwa na nchi hii. Sina hakika kama kuna eneo kubwa kiasi hiki katika nchi yoyote, ambayo imetengwa kama Tanzania ilivyotenga eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tungetaka kupanua Hifadhi ya Ziwa Manyara, tungeifanya wakati huo mwaka 1971, ambapo *TANAPA* walikuwa wanatafuta, wanaweka mikakati ya kununua mashamba. Kulikuwa hakuna tatizo, eneo lilikuwa kubwa, mashamba yale ya ugolo yalikuwa mengi sana. Manyara Ranchi mpaka Makuyulu kule kote kulikuwa hakuna tatizo lolote. Ule ndio ulikuwa wakati wa kupanua Hifadhi, siyo leo ambapo sasa kumeshakuwa na matatizo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa kijiji cha Mayoka kinachosemwa sasa ni watu walioomba kuhama kutoka Mbulu kwa Mheshimiwa Marmo, waliomba ardhi huku Wilaya ya Babati wakati ule ilikuwa Hanang. Hawa ni watu waliokuwa wamehamishwa kutoka kule na Serikali yenye, ndio wakapelekwa pale Mayoka na waliahidiwa rasmi kabisa kwa barua ambayo ninayo hapa na ambayo nimeitaja hata wakati wa kufanya marekebisho kwenye jedwali ambalo sihangaike nalo sasa. Wamepewa kabisa na Serikali imeonyesha nia kwamba, wahamie *Unit No. 4* na *Unit No. 1* na ipo na ndio leo kijiji cha Mayoka kipo *No. 4*. Kwamba, *No. 1* wananchi wale walishindwa kukaa kwa sababu tayari ilikwishesheuka wanyama. Huyu Bwana Bakker aliyekuwepo pale alishindwa kulima pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashamba hayo matatu yanayotajwa, ndio yaliyokuwa yanalisha uliokuwa Mkoa wa Arusha kwa chakula, anayetaka kupinga aniambie kama alikuwepo. Sisi tunajua hayo maeneo, kwa hiyo ni lazima tuzungumze matatizo ya msingi ya wananchi katika maeneo ambayo tunayafahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *style* hii ya kutaka kutatua matatizo ya wananchi ndio tatizo kwa Serikali. Ndio tatizo, wala wananchi hawana tatizo, wanaelewa kabisa yote hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka wa 1971, ambapo *TANAPA* ilianza mikakati ya kutaka kununua mashamba na hii *style* ya kununua mashamba halafu unapanua Hifadhi, ipo siku utanunua shule, utanunua hospitali ukitaka kupanua hifadhi. Juzi tu hapa, Mkuu wa Mkoa nadhani alikwenda kwenye eneo hilo la Vilima Vitatu au katika maeneo hayo, wananchi walimwambia maisha bora kwa wanyama na siyo kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maneno kama haya kwa nini yatoke kwa wananchi; ni kwa sababu staili yetu ya kutatua matatizo ndio yenye shida. Staili ya kusikiliza kero za wananchi ndio ina shida. Leo ni mwaka 2008, *TANAPA* ilipoanza kutafuta haya mashamba kulikuwa na maeneo mengi tu, leo ni miaka 37 vijana waliokua ambao sasa wana miaka 37 unasema usiwashirikishe katika maamuzi ili waseme wanapata matatizo gani ili walau washiriki katika uhifadhi endelevu hutaki. *TANAPA* ilipofanya mbinu za kuhakikisha kuwa, inapata shamba hilo kuitia Serikalini na Serikali ikapuuza maagizo yake yenye au barua yake ya kuwaambia wananchi kwamba, mtakaa na Unit Namba Moja, *TANAPA* wakafanya utaratibu na Serikali wakapata hilo eneo mwaka 1974. Hati miliki ya haya maeneo imetolewa miaka ya 1990.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini hatujiulizi miaka 16 baadaye ndio wanatafuta hati miliki; kwa nini na hawa vijana ambao sasa wana miaka 16 tangu hati hizo zitolewe miaka ya 1990 hawana haki ya kujua nini kinatendeka katika eneo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependa kuwa wazi kwamba ni vizuri tujifunze kutatua matatizo kwa njia zilizo sahihi, kutokushirikisha mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Babati ni tatizo. Mpaka sasa Baraza la Madiwani ndio lenye uwezo kwa mamlaka ya mambo ya ardhi. Serikali ya kijiji ina uwezo wake, mamlaka ya Wilaya ina uwezo wake na Wizara ina uwezo wake, lakini hawakushirikishwa. Haya ndio matatizo yangu, tulianzisha mchakato wa ushirikiano, ameutaja Mheshimiwa Nakei pale, ilikuwa tukutane wakati ule tukasema tuendelee kukutana mpaka tumalize jambo hili, lakini haikutokea mpaka wananchi walipochoka ndio wakaenda mahakamani. Kuhusu kesi nadhani imeshatajwa pale; kama kweli Serikali imeshinda kesi, mashamba yote haya ni mali ya Serikali. Imethibitishwa hivyo na Jaji Mkuu, Mheshimiwa Waziri, aweke nakala ya hukumu pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichofanyika ni kesi ilielekezwa iende Baraza la Ardhi na wananchi walikuwa wanaendelea kusubiri jambo hili ili waendelee kufanya mazungumzo sasa wamekatishwa tama. Kwa hiyo, Serikali ikafuta hiyo kesi kwa sababu

kwanza haikuwahi hata kusikilizwa, ilifutwa kwa sababu wananchi walikuwa wanasubiri hayo maelewano yaendelee. Kwa kuwa inahusu ardhi, ilielekezwa ipelekwe kwenye kitengo cha ardhi cha Mahakama Kuu ndiyo kinachohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba, katika kubadilisha matumizi, lazima sheria za ardhi zizingatiwe na lazima mchakato huu uhusishe watu. Unaposema unainua hadhi ya Msitu wa Marang, sina tatizo kwa sababu ni msitu wa Serikali, lakini lazima kulikuwa na maslahi ya kawaida ambayo wananchi wanapata. Msitu ulipokuwa katika *management* ya kawaida, ukishaweka kwenye hifadhi, hautakanyaga hata hatua moja, kwa sababu sheria za hifadhi ni kwamba, hata mti ukikauka pale ukianguka una kazi; itakuwa chakula cha sisimizi na wadudu wengine wote.

Huwezi kuokota mti kwa ajili ya kuni haiwezekani, lakini hawa wananchi walikuwa wanapata maslahi yao madogo madogo kwenye msitu huo wa kawaida kama kuokota kuni, nyasi, maji na vitu vingine. Sasa ukiupandisha hadhi ni lazima uelewane, kwa sababu Kijiji cha Mayoka, watu ambao hampajui ni kwamba, hata shule ipo kwenye mpaka na kijiji. Hapo hapo kwenye mpaka wa Msitu wa Mara. Lazima kufanyike utaratibu wa maelewano, kitu gani kifanyike; vinginevyo hawa watu hawataweza kuishi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Shamba la Prince Bernard, Serikali ndiyo iliyotengeneza hati mbili, hati juu ya hati. Shamba hili lilikuwa na hati na yeye mwenyewe alisema natoa urithi uende kwenye hifadhi, lakini baadaye Serikali ikatangeneza hati na ikamuuzia mtu. Nadhani ana hati kama sikosei ya miaka 33 au 13, lakini inaweza ikapatikana. Nilikuwa na hizo documents wakati ule leo sina, lakini ni hati juu ya hati. Mpaka sasa ukafute, nina hakika fidia ilikuwa karibu bilioni mbili wakati Fulani, leo haiwezi kuwa chini ya bilioni tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, lile ni shamba, mimi namshangaa ndugu yangu mmoja anasema eti ni pori. Shamba la Prince Benard ni shamba ambalo linatoa mazao mengi sana pale na yule bwana ana vifaa vingi sana; matrekta na kadhalika. Kwa hiyo, lile ni shamba linalozalisha mazao, sehemu ya msitu ipo lakini ni kidogo. Katika ile hati miliki ni lazima uonyeshe eneo hili ni la msitu na hili ni la kilimo, lakini ni shamba la uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli Serikali itaweza kufidia hilo shamba kwa haraka iwezekanavyo, kama Waziri alivyokuwa anasema, sijui mimi nitashukuru ili jambo hilo hilo lifanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli Serikali inakwenda kufanya hayo, hebu waende kujaribu, najua TANAPA walijaribu; kwa nini walishindwa kufidia, kuna matatizo ya kisheria pale. Sawa shamba lile limefutwa na Rais wa Awamu ya Tatu, baada ya kuonekana kwamba, kuna matatizo ni hati juu ya hati, sasa ukifuta yule ambaye ulimpa ni lazima umfidie tena; unamwondoaje ana vifaa na kadhalika?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli Serikali mna nia nendeni mkaongee na wananchi, ndiyo maana mimi siungi mkono Azimio hili mpaka mfanye hayo. Futeni hili, wapeni wananchi wawaachie hiyo ambayo walikuwa wameahidiwa na Serikali; Namba Moja ili mchukue 1, 2, 3 wananchi wapewe hilo. Sina hakika kama itakuwa chini ya miaka mitano, mimi sijui lakini kama mna fedha sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, lipo tatizo; Kamati ya Bunge ilikwenda, lakini ilikwenda ikaongea tu na wafanyakazi wa hifadhi. Kama mlivysokia kwenye maoni hapa, wamesema kwamba, tulisikia mgogoro hivi Kamati ya Bunge ikisikia kuna mgogoro inawezaje kuamua kusema hili jambo liridhiwe, badala ya kusema twendeni sasa huko kwenye mgogoro tukawahoji; mbona kwenye Miswada mingine tunaita *Public Hearing* tunawauliza watu, tunajadiliana nao halafu tunakubaliana nao? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo zito linalogusa ardhi ama maisha ya watu linaachwa, Kamati ya Bunge ilirudia upande mmoja tu huko, ndiyo maana mimi nilipopata nafasi nilienda kwenye Kamati na kusema jamani nendeni; hivi kukaa mpaka Bunge la Januari litakapokuja kunaharibika nini; hiyo hifadhi itakufa kesho kutwa, imekaa miaka yote mpaka leo; kwa nini tusimalize jambo hili? Nendeni mkapate na upande wa pili ili matatizo haya yamalizike, Kamati mmekiri wenyewe hamkwenda, mmebaki upande wa *TANAPA* mmesikiliza huko, mkaachana huko.

Mnajua kabisa, suala la migogoro ni lazima Kamati ya Bunge iwe *balanced*, ndiyo kazi ya Bunge hapa. Unaishauri Serikali namna gani na unaismamia namna gani, tutapitisha mambo ambayo yatakuwa na makosa hapa halafu itakuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina tatizo kama nilivyosema, lakini haya ni lazima yaangaliwe. Yapo matatizo mengi sana na mambo madogo madogo haya, ndiyo yanayojenga chuki kati ya wananchi na Serikali, lakini ukiweza kulitatua mapema wala hakuna tatizo.

Jambo hili lingekwisha zamani, lakini wenzetu wa hifadhi ndiyo wamelifikisha hapa na kuishauri Serikali sasa sijui muangalie na hivyo vyombo vyenu vinakaaje, lakini vinaweza vikatuletea matatizo ya chuki bure kati ya wananchi na Serikali yao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mkitaka hiso hati juu ya hati, kama mkitaka kwenda kuzihangaikia mtakamatana wenyewe uchawi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, bado nasema siungi mkono hadi Serikali itakapokamilisha hayo mengine. Siku yakikamilika, nina imani nitakuwa Mbunge kama sitakuwa Mbunge, basi nitakuwa raia ambaye anaona kwamba, kama mmelitekeleza basi raia wale watakuwa wanaishi vizuri. Hatuna sababu ya kuongeza migogoro, njia rahisi ni kutatua migogoro. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Hifadhi za Taifa sehemu nyingi sana kuna migogoro, kwa sababu ya staili hiyo tu. Hata kule Talangire kuna migogoro kwa sababu ya staili hii ya kuacha kuwasikiliza wananchi vizuri. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu kwenye hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nataka kutoa pungezi zangu za dhati kwa Wizara, kwa kuileta hoja hii mbele yetu. Ninaamini wameileta katika wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapata wakati mgumu, kwa sababu ninazungumza baada ya mchangiaji ambaye amepinga kabisa Azimio hili. Sasa naona hali ya hewa imechafuka, nitajitahidi kuzungumza yale ninayofikiri yanaweza kusaidia ili hoja hii iweze kupita kama ilivyokusudiwa toka mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kitaaluma ni Mwanasayansi wa Zoolojia ama Elimu ya Viumbe na nimebobea kabisa katika hilo. Ninajivuna sana kwamba, nipo katika nchi ambayo imejitahidi sana kuhifadhi viumbe kwa ajili ya wananchi wake na kwa ajili ya mataifa mengine. Tanzania ni nchi ambayo kwa kweli tunajivunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii toka mwanzo wananchi wake walilazimishwa kuhifadhi wanyamapor. Naweza kusema kwamba, huko mwanzoni Serikali ya ukoloni ilikuwa inalazimisha, ndiyo maana tukapata haya mapori kama ya Selous na kadhalika. Nilitaka kusema kwamba, wakati ule ilikuwa ni nguvu tu inatumika, lakini katika kutumia nguvu hiyo leo hii Watanzania tupo kifua mbele tunaringa kwamba, lile walilolifanya Wakoloni kwa kulazimisha imekuwa ni faraja kubwa kwa wananchi wengi wa Tanzania. Mimi nakumbuka mwaka 1987, wakati nipo Uhlanzi, tulitembelewa na Hayati Mwalimu Nyerere na tukawa na mazungumzo naye.

Katika mazungumzo alisema, hakuna kitu alichokuwa anakichukia kama ukoloni, lakini kama angeambiwa ni aina gani ya ukoloni ambao ulikuwa na manufaa kwa Tanzania angesema Ukoloni wa Mjerumani. Ukoloni wa Kijerumani siyo kwamba ulifanya mambo mazuri, lakini ukiangalia kabla ya mwaka 1918, walifanya mambo makubwa ya ajabu; walitujengea reli kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma na reli ile wamejenga wazee wetu kwa fimbo. Walikuwa wanalazimishwa kubeba mawe na kadhalika. Hayo ndiyo yaliyowapata wazee wetu, lakini Mwalimu akasema leo jamani si tunashukuru reli ipo na wenzetu katikati mpaka magharibi, wananaufaika na reli hii. Akasema kwamba, jamani kuna wakati mwingine kuna baadhi ya mambo yanaweza yakafanya tukayaona mabaya, lakini kama yakiwa na manufaa kwa nchi, basi tushikilie yale manufaa. Natoa mfano huu, kwa sababu katika suala la wanyamapor, maeneo mengi yaliyohifadhiwa yalianza wakati wa mkoloni na wala hakutuuliza na sisi wengi tumepata hasara kwa kuwahifadhi hawa wanyama, lakini leo tunashukuru kwamba, hatua zile zilichukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, huku *Selous* unaweza ukaiingiza nchi ya Ujerumani, Uholanzi na Ubelgiji, zote hizo ndani ya pori moja la Selous. Wananchi katika maeneo yale, walikuwa wanahitaji mabonde yao ili walime na kufanya shughuli nyingine za kawaida. Wasingekubali kuachia kwa ajili ya hifadhi ya wanyama, leo hii wanyama hawa wa porini wasingekuwepo; hivyo hiyo ilikuwa ni *sacrifice* waliyojitolea. Mkoa wa Lindi mnaousikia, mpaka sasa hivi una watu kama milioni moja, zaidi ya asilimia 98 ya eneo ni Pori la Selous; hawa wananchi wamejitolea kwa ajili ya Tanzania.

Mhehimiwa Naibu Spika, tunapokuja kuangalia suala hili nashukuru, kwa sababu kuna wananchi wanantisikiliza pale na wenzetu wanaotoka katika eneo hilo la Manyara, nawaomba waelewe kama tulivyoelewa sisi katika maeneo mengine, tukayatoa kwa ajili ya kuhifadhi hawa wanyama. Tulifanya hivyo kwa ajili ya nchi yetu Tanzania (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya matatu yametolewa ni mali ya Serikali, sasa kinachoombwa wala hakuna mgogoro hapa na wenzetu wengine wanaofahamu sehemu zile wanasesma ni mapori tu. Sasa jamani kwa nini tusikubali kama walivyokubali wenzetu katika maeneo mengine? Leo hii tunazungumzia juu ya Ruaha inataka kuwa mbuga kubwa, sasa haiwezi kuwa mbuga kubwa Tanzania hii bila watu wengine kujitolea kutoa maeneo yao kwa ajili ya wanyama na wamefanya hivyo. Kwa hiyo, nawaomba wenzangu wa Mkoa wa Manyara na hasa Viongozi wa Siasa, naomba waelewe na wawaeleweshe wananchi kwamba, tunahitaji maeneo haya kwa ajili ya uhifadhi wa wanyama kwa ajili ya kizazi hiki na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri Manyara inajulikana sana Dunia nzima, hivi leo kuongeza kiasi kidogo tu cha ekari; hivi kuna tatizo kweli? Mheshimiwa Kwaangw' kama ardhi haitatosha huko, karibuni Kusini, tuna maeneo makubwa na tunasema hakuna wasiwas, lakini katika maeneo hayo ambayo ni mazuri kwa ajili ya wanyama, hebu tuwaachie wanyama. Kama tulivyoelezwa kwamba, kuna duma na kongoni, wote hawa wanatoweka kwa sababu ya jitihada za binadamu katika kuendeleza makazi haya. Kwa hiyo, mimi ningeomba kwanza hili tulielewe sisi viongozi na tuwaeleweshe wananchi, wakishaelewa nadhani hatutakuwa na matatizo yoyote. Mwanzo wake ni katika kuitisha Azimio hili, kwa sababu lisipopita itaanza migogoro na inaweza ikaenea nchi nzima, kwani maeneo mengine watu nao watasema kwa nini na sisi maeneo yetu tuyatoe kwa wanyamapor wakati tunayahitaji. Naomba Manyara isije ikawa kiini.

Juu ya Azimio hili, ninashauri hayo na ninaamini wenzangu watanielewa vizuri na wananchi nao wataelewa ili Hifadhi yetu ya Manyara iweze kuwa kubwa na ya kusifika ulimwenguni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mrope. Msemaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Ole- Sendeka.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya kupanua Hifadhi ya Ziwa Manyara. Wakati Waziri anamalizia kuwasilisha hoja yake, alisema maneno yafuatayo; naomba kunukuu kwa ruhusa yako: “Naomba Waheshimiwa Wabunge, muunge mkono hoja hii ili kuokoa Hifadhi Taifa ya Ziwa Manyara katika hatari ya kutoweka kabisa, jambo ambalo litaiweka doa nchi yetu katika sura ya Kimataifa.”

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kauli yake hiyo inayothibitisha dhamira yake ya kuhifadhi wanyamapori, ambao kwa niaba yetu na kwa niaba ya nchi yetu, amepewa dhamana ya kusimamia sasa kwa kuteuliwa na Rais Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri huyu pia anastahili pongezi kwa kasi ya kuthibitisha dhamira hiyo na kwa kazi anazozifanya toka aingie kwenye Wizara hiyo, kwa nia ya kuokoa hifadhi zetu na rasilimali za nchi yetu. Laiti angelikuwa Waziri mara tu baada ya tamko la Baba wa Taifa, Mwalimu Kambarage Nyerere, maarufu kama *Arusha Manifesto*, ambayo ilithibitisha dhamira ya Serikali ya Tanzania, Serikali ya TANU kwa wakati ule na dhamira ya Serikali ya CCM kwa sasa ya kuihifadhi wanyamapori, ambayo kwa ruhusa yako Baba wa Taifa alisema hivi, naomba kwa ruhusa yako ninukuu sehemu chache za tamko la *Arusha Manifesto*: “*The survival of our wildlife is the matter of grave concern to all of us in Africa, in accepting the trusteeship of our worldlife will solemnly declare that we will do everything in our power to make sure that our children and grandchildren will be able to enjoy this rich and precious inheritance.*”

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema laiti ungelikuwa Waziri, haya ungeyafanya miaka mingi iliyopita na migogoro tuliyonayo leo tusingekuwa nayo. Bahati mbaya sana katika muda wa miaka hiyo ya 1970 kuelekea 2008, mambo mengi yamefanyika kiasi kwamba, njia za wanyamapori zimeathirika na hifadhi zetu baadhi ya wanyama wamepotea na hii hatuwezi kukwepa lawama wale ambao walipata dhamana ya kuisimamia Wizara hii kwa nyakati tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo kinachothibitisha dhamira ya baadhi yetu kutokusimamia haya tunayoyasema ni pale ambapo Prince Bernard alitoa shamba, akaandika wosia kwamba, mimi nikifariki eneo hili la shamba langu litumike kwa ajili ya uhifadhi. Sisi tuliokuwa watendaji wa Serikali, baadhi yetu walitoa shamba hilo kwa mhindi mmoja anayeitwa Ganji na ambaye anamiliki leo hati juu ya hati. Eneo hili lilitolewa kwa ajili ya kupewa *TANAPA* kwa minajili ya uhifadhi.

Mimi sina haja ya kurudia sana yale ya Moyamayoka, lakini nataka kusema machache tu. Serikali kama inadhamiria kuwaahidi Wananchi wa Mayamayoka Shamba hilo Namba Tano la Prince Bernard, Serikali ichukue hatua za haraka kumfidia huyo mwekezaji aliyepo hapo ili wananchi hao wasiachwe bila kuwa na sehemu ya kuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhifadhi wa wanyamaporini chini, hatukufundushwa hata siku moja na Wazungu. Hii ni tabia na hulka yetu Wamasai wa Ngorongoro wanaoishi na wanyama pale eneo la Mamlaka ya Ngorongoro. Hakuna *tuition* waliliyowahi kupewa na Wazungu. Tilitenga maeneo ya uhifadhi kama kule kaskazini eneo la *Tarangire National Park*, *Manyara National Park*, tukatenga Serengeti, ikatengwa *Arusha National Park* na *Kilimanjaro National Park*. Sidhani kama kuna Mtanzania alichapwa kiboko, ilikuwa ni hulka ya wazazi wetu kulinda na kuhifadhi na ndiyo maana *Arusha Manifesto* iliyotolewa mwaka 1961 na Mwalimu Nyerere, ilikuwa ni dhamira ya Mwalimu mwenyewe, hakupata shinikizo wala fundisho la Mzungu yejote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa tu niishauri Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kwamba, inapotaka kufanya mabadiliko ya matumizi ya ardhi yoyote, iwashirikishe wananchi wanazunguka. Hii ni dhahiri kwamba, Mashamba Namba Moja, Mbili, na Tatu yaliyokuwa yanazungumziwa hapa, yaliyokuwa yanapandwa mahindi, maharagwe na mazao mengine. Sasa inapotokea kwamba, wewe uliye jirani yangu mimi nipo Shamba Namba Nne ambako ninafuga ngo'mbe na kulima, wewe umeamua kufanya sasa si shamba tena la mahindi kama ilivyokuwa mwanzo, bali ni shamba la simba, chui, tembo na pofu!

Nadhani busara inadai kwamba, sisi tunaopakana tushirikiane kwa pamoja, mabadiliko unayoyafanya tujiandae sote na haya yanayotokea, kwa sababu shamba na pofu haliwezi kuwekwa pamoja na shamba la mahindi na maharagwe. Hili ni jambo ambalo Serikali inapaswa kuliangalia, inapofanya matumizi hayo, hata kama ina uwezo wa kununua mashamba mengi. Kwa hiyo, nilikuwa naishauri Serikali iangalie mambo haya, inapotaka kufanya mabadiliko ili kuweka uhusiano mzuri kati ya Hifadhi zetu za Taifa na wananchi wanaozunguka maeneo hayo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia baada ya kutoa ushauri huo, kusema kwamba, hata ile kesi iliyoelekezwa iende kwenye Baraza la Ardhi ni vizuri basi mkawawahi wale wananchi mzungumze nao. Kama ulivyo sema, muwaahidi eneo la kuwapeleka ili wasiendelee kwenda kwenye Baraza la Ardhi na kukwamisha utekelezaji wa Azimio letu la Bunge iwapo litapita. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia katika kujadili suala hili la Hifadhi za Taifa, nigosie baadhi ya maeneo mengine yanayozunguka Hifadhi zetu za Taifa. Mimi natoka Wilaya ya Simanjiro, ambako tunapakana na Hifadhi ya Tarangire na eneo la *Mkungunero Game Reserve*. Bado ipo haja ya *TANAPA* kujenga uhusiano mwema zaidi na majirani wanaowazunguka. Hii itatusaidia sana na hata tunapoanzisha hizi *game reserves* na *National Parks* ni vizuri kushirikisha vijiji vilivyo. Leo kuna mgogoro kule Kimotoro katika Wilaya ya Simanjiro na *Mkungunero Game Reserves*, kuna mgogoro katika Kijiji cha Rikiushiba Wilayani Kiteto na *Mkungunero Game Reserve*, bado namshauri sana Waziri mwenye dhamana atafute muda wa kukaa na wananchi wa maeneo hayo ili ombi tulilompelekea Mheshimiwa Rais, sasa liweze kutekelezwa na kubadilisha mpaka wa *Mkungunero Game Reserve*, kwa kuzingatia mahitaji ya vijiji ambavyo shule zao na makazi yao ya kudumu yapo katika eneo hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tunazungumzia suala zima la uhifadhi, niruhusu pia nigosie baadhi ya mambo ambayo ni muhimu katika eneo letu la Hifadhi ya Mamlaka ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sheria ya Kuanzishwa kwa Mamlaka ya Ngorongoro, mamlaka ilipewa majukumu makubwa mengi tu lakini nitataja mawili au matatu. Kwanza, kwa mujibu wa sheria hiyo ni uhifadhi, naomba kunukuu inasema:

- (a) *The functions of authority shall be to conserve and develop the natural resources of the conservation area.*
- (b) *Inazungumzia promotion of tourism.*
- (c) *To safeguard and promote the interest of the Masai citizens of The United Republic engaged to cattle, ranching and dairy industries within the conservation areas.*

Nataka niseme suala la kwanza ni uhifadhi, la pili ni utalii, lakini la tatu ni kulinda maslahi ya wale Watanzania wa Jamii ya Kimasai, wanaoishi katika eneo la Mamlaka ya Ngorongoro. Kwa nini nimeamua niligosie hili la mamlaka?

Mabadiliko yanajitokeza kadiri dunia inavyobadilika. Mamlaka ya Ngorongoro sina haja ya kurudia yale niliyoyazungumza kwenye semina, nategemea Waziri alinielewa na aliniambia kwamba, atayafanya kazi baadhi ya mambo ambayo yana migongano ya maslahi yaliyopo pale. Katika *General Management Plan* ya Mamlaka ya Ngorongoro na kwa jinsi Bodi ilivyokaa na kutangaza baadhi ya maeneo kwa ajili ya ujenzi wa *lodges*, maeneo kama vile Embakai, Likapus, Maseki, Esiri wa kule Endulen ni maeneo ambayo yameamuliwa kujengwa *lodge* kwa ajili ya watalii watakaokuja katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa tu kuishauri Serikali kwamba, ipo haja ya kuwa na *building code* katika eneo la Mamlaka ya Ngorongoro kwenye *General Management Plan*. Kwa sababu kuna Wamasai wanaishi pale, hamuwezi kutarajia kwamba, tangu mwaka 1959 Wamasai walioko pale wataendelea kukaa kwenye nyumba za tembe zile bila kuruhusiwa kujenga nyumba za kisasa halafu tukasema kwamba hawa tunawatendea haki.

Hawa ni Watanzania, ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaelezea haki ya kuishi na wao kufaidi rasilimali za nchi yao na kuishi kama binadamu wengine ni haki yao pia ya msingi, hata hawa walioko kwenye Mamlaka ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningependa kuishauri Serikali, ifanye marekebisho kwa kutumia Bodi ya Mamlaka ya Ngorongoro kwenye *General Management Plan* ili kuweka *Building Code* itakayosema kwamba, watu hawa wanaoishi

kwenye eneo la mamlaka, watajenga nyumba zinazofanana na mazingira hayo. Hata hao wanaojenga *lodges* hizo, Mheshimiwa Waziri asikubali wajenge bila kwanza kukamilisha utaratibu wa *building*, uweze kujua kabisa kwamba, zitajengwa nyumba za aina gani ambazo hazitaathiri uhifadhi katika eneo la mamlaka ya Ngorongoro.

Ukishafanya hivyo, basi tutakuwa na uhakika kwamba, siyo mwine anawenda ghorofa ya 50 mwine ghorofa ya tano, mwine anajenga vibanda vibanda pale, halafu tunajikuta tumeruhusu ujenzi holela ndani ya eneo la mamlaka na kuathiri masuala hayo.

Kubwa ninalolizungumza ni ujenzi wa makazi ya wenyeji, wanaoishi katika eneo la Mamlaka ya Ngorongoro. Lazima sasa waambiwe mnajenga nyumba za kisasa, lakini wapeni aina ya ujenzi utakaofanyika ili wasiendelee kukaa kwenye nyumba za tembe, ambazo hewa ni ndogo eti kwa kisingizio kwamba wana hifadhi.

Mnaohifadhi pale ni wanyamapor kwa faida ya watalii, kwa faida ya taifa na faida ya vizazi vijavyo. Wale Wamasai wa Ngorongoro nao wanahitaji wabadike, waishi nyumba za kisasa, walalie magodoro na wapate nyumba zenye hewa ya kutosha ya kuingia pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampungeza Waziri, nilimweleza juu ya tatizo la kampuni moja ile ambayo anajua ya Usangwa, ambayo ilikuwa imekamatwa na nyara za Serikali. Mheshimiwa Waziri, alichukua hatua pale pale, ndiyo napata imani kabisa na Mawaziri wa Serikali ya Kikwete wanapochukua hatua wakati kero zinapojitokeza kama alivyofanya Mheshimiwa Mwangunga.

Ni imani pia kwamba, yale niliyoyazungumza ya migongano ya maslahi Ngorongoro, utayashughulikia na hayo mengine ili kufikia Januari wakati wa kujadili Muswada ule mwine, zisiwepo hizo kero; vinginevyo hapa mambo yatakuwa mazito kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, namkumbusha tena Mheshimiwa Waziri, aelegeze nguvu zake katika suala la mahusiano na hasa anapotaka kufungua njia ile ya wanyama kupitia Isilale, Losilwa, Kambi ya Simba, Mwaya Mayoka, Minjungu ili wananchi wa maeneo hayo katika Wilaya ya Monduli, Wilaya ya Babati na Wilaya nyingine zinazopakana ambazo mapalii ya wanyama yanapita, basi waweze kushiriki na wao waweze kunufaika na rasilimali hiyo.

Hata sisi wengine ambao tupo katika eneo ambalo wanyama wote wa Talangire wanakuja kuzalia kwenye mbuga ile ya Simanjiro, Vijiji vya Emboret, Leborosoit, Terati, Kimotoro, Lebosileti na Lakau, ambako ndiyo wanyama wote wanakuja kuzalia, basi na ninyi muweke nguvu kuhakikisha kwamba, mniamwelekeza Mkurugenzi wa TANAPA aweze kuelekeza fedha kidogo kuweka mabwawa kule ili wanyama hawa wanaotoka huko wawe na uhakika wa maji na ng'ombe wa Simanjiro walioko pale wanywe maji.

Hiyo siyo hisani, kutoa chakula kwa mtoto wako anayeishi kwangu, utakuwa umechangia tu kumwezesha awepo. Asipomaliza maji ya ng'ombe wangu, amalize na

malisho ya ng'ombe wa Wananchi wa Simanjiro akirudi pale Talangire mimi nikiingiza mbuzi nakamatwa.

Kwa hiyo, nataka nishauri kwamba ni vizuri tujenge mahusiano mema kati ya hifadhi zetu na wananchi. Baada ya kusema hayo ni imani yangu kwamba, Waziri atashughulikia suala hilo la Moyomayoka kuhakikisha kwamba, wale wananchi wanapata shamba ambalo litakidhi matarajio yao.

Baada ya kusema hayo na mimi nataka kusema ...

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)

NAIBU SPIKA: Unaunga mkono hoja?

MHE. CHRISTOPHER O. OLE – SENDEKA: Nitafikiria baadaye. Naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ruth Msafiri, dakika kumi tu ulizoomba.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nilifikiri umeniambia nitachangia kesho, nikaanza kukusanya zana kwamba nitachangia kesho. Lakini kwa muda huu ambaو umenipa nitajitahidi kuutumia kadiri inavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa lengo la kutaka kuunga mkono hoja iliyoko mbele yetu kwamba, turidhie Azimio hili la Upanuzi wa Hifadhi ya Taifa Ziwa Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza mtoa hoja kwa uwasilishaji wake hodari. Mimi napenda niseme kwamba, Taifa letu la Tanzania limepata sifa kubwa sana, kwa miaka mingi ya uhai wake, kwa jinsi ambavyo Serikali imeweza kuhakikisha kwamba, imetunza maliasili ya Watanzania hasa wakiwemo wanyamapori ambaو tumeendelea kuwa nao miaka hadi miaka.

Vilevile ni ukweli ambaو haupingiki kwamba, taifa linaloendelea kama la kwetu tunazaliana, tunaongezeka, kwa vyovyyote vile mahitaji ya ardhi yamekuwa ni makubwa pia. Kwa hiyo, kwa sasa hivi linapokuja suala zima la kutaka kuongeza upanuzi wa hifadhi, haliwezi kupita bila kuwa limepata hoja mbalimbali hasa zinazozingatia mahitaji ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la kutunza mazingira sasa ni suala la dunia nzima, hakika hatuwezi kulikwepa. Kwa hiyo, hata wenzetu ambaو wanakaa karibu na hiyo mbuga ni kipindi ambapo sasa suala hili limejitokeza kwao.

Kwa kuwa suala hili linagusa maisha ya wananchi, ipo hoja ya kwenda nao karibu kuweza kuhakikisha kwamba, kwa kadiri inavyowezekana, hazitakuwa hoja zote lakini zile zilizo kubwa za msingi zinazowagusa walio wengi, ziweze kupata majibu yaliyo sahihi ili hifadhi yetu ambayo tunaiheshimu sana, inatuletea heshima ya taifa, basi iendelee ikiwa inapendwa na wale wanaokaa karibu nayo ili wageni watakaotembelea pale wapate mapokezi mazuri, urafiki uwepo tangu inavyopanuliwa mpaka itakapokuwa imeendelea kuwepo. Kwa ajili hiyo, suala zima la kuwashirikisha wadau au majirani wa eneo hilo, haliwezi kuepukika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema suala la kutunza wanyama amba ni hifadhi ya taifa letu, ni letu sote. Tutaendelea kulisimamia na tutakuwa karibu na Serikali ili kuona kwamba, pale ambapo lengo ni kutaka kuhakikisha kwamba inaboresha hifadhi zetu, basi iende sambamba na kuona hali za Watanzania zinakuwa nzuri, vilevile zipo katika hali ambayo si ya manung'uniko wala malalamiko makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama nilivytangulia kusema, sikuwa na mengi ya kuzungumza lakini nilipenda na mimi niunge mkono jambo hili. Ila nilikuwa na angalizo moja tu; katika uwasilishaji na michango ya Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kuchangia, inaonyesha kwamba, licha ya kwamba hapa kuna hifadhi na linapendekezwa eneo liongezwe kwa ajili ya wanyamapor, lakini hapa pia kuna maliasili nyingine ya misitu mikubwa. Imetajwa misitu mikubwa na mimi narudia kusema misitu mikubwa.

Misitu mikubwa Tanzania, wakati fulani ilituletea matatizo. Kwa hiyo, napenda nitoe kama angalizo kwamba, tusikusudie kutunza wanyama lakini wakatokea wajanja wachache wakainuka na ubinafsi kuifanya sasa misitu ile ni yao wenyewe kesho.

Kesho kutwa tena tutapata tatizo la magogo makubwa kuanza kusafirishwa kutoka katika hii hifadhi yetu nzuri, tutaanza tena kupata matatizo ambayo hakika siyo yaliyokusudiwa.

Tunaomba na naishauri Serikali kwamba, misitu hii itunzwe sambamba na wanyama hawa si kwa ajili ya mtu mmoja, siyo kwa ajili afisa mmoja, kwa sababu nalisema hili kwa uhakika kabisa Mheshimiwa Waziri, hahusiki na baadhi ya maafisa wengine hawahusiki, lakini wapo maafisa wake kwenye Wizara yake, siyo waaminifu sana katika suala la kutunza misitu yetu. Wamekuwa wanajimilikisha, wanaitoa bila vibali inasafirishwa bila vibali, hali ambayo haijatupa heshima.

Mimi nimeona hili siwezi kunyamaza, lazima nizungumze kwamba, ninaomba dhamira yetu ya ndani iendelee kusimama. Tunahitaji hifadhi hii kwa ajili ya kuongeza njia za wanyama, mazingira yawe mazuri, tuboreshe kwa ajili ya Watanzania wote. Si maana yake sasa tukishakuwa tumefikia hatua hiyo, basi watokee wengine kutaka kuondoa makusudio haya yaliyokuwa mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nirudie kwamba, ninaunga mkono hoja na ninashauri wananchi waonwe na matatizo madogo madogo yanayozungumzika

yamalizike. Kama kuna kesi iondoke mahakamani, kwa sababu hatuwezi kufanya kazi vizuri wakati kuna malalamiko makubwa.

Lolote ambalo linaweza kuwa kikwazo, lililo ndani ya uwezo wetu, linaweza likaondosheka na kazi hii ikafanyika vizuri, wananchi wa Tanzania wakabaki na amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwa lengo ni kwamba, wananchi wasitelekezwe bali waheshimiwe na waweze kupewa haki yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, nasema naunga mkono hoja ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa siku ya leo. Huu ni uwanja kila mtu anatoa maoni na maoni ni kujenga hoja ambayo inaweza kuwafanya watu wengine wakaelewa zaidi. Kwa hiyo, tutaendelea kesho asubuhi na Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Profesa Mwalyosi, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Anthony Diallo, Mheshimiwa Lekule Laizer na Mheshimiwa Kaika Telele. Baada ya hapo ataitwa mtoa hoja, halafu tutakuwa tumemaliza suala hili.

Waheshimiwa Wabunge, sina matangazo mengine, napenda kuahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 01.53 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,
Tarehe 07 Novemba, 2008 Saa Tatu Asubuhi*)